

# Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

## BUNGE LA TANZANIA

### MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 6 Mei, 2014**

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

### WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wabunge Waliiimba Wimbo wa Taifa)

### D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

### KIAPO CHA UTII

Wajumbe wafuatao waliapa Kiapo cha Utii na kukaa katika nafasi zao Bungeni:-

Mhe. Godfrey William Mgimwa  
Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete

### TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Ninapenda kuchukua nafasi hii, kuwapongeza Mheshimiwa Godfrey Mgimwa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, kwa kuchaguliwa na kujunga na sisi katika Bunge hili. Tunaamini kwamba, tutapata ushirikiano unaostahili. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wa Kumi na Nne, Bunge lilipitisha Miswada ya Sheria minne iitwayo; Muswada wa Sheria wa GEPF ya Mfuko wa Mafao ya Wastaafu wa Mwaka 2013 (*The GEPF Retirement Benefit Fund Bill, 2013*); Muswada Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba Tatu wa Mwaka 2013 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Number Three Bill, 2013*); Muswada Sheria ya Kura ya Maoni (*The Referendum Bill, 2013*); na Muswada wa Sheria ya Marekebisho Kodi ya Ushuru wa Mwaka 2013 (*The Excise Management and Tariffs (Amendment Bill), 2013*).

Kwa Taarifa hii, ninapenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba, Miswada hiyo imekwishapata kibali cha Mheshimiwa Rais na kuwa Sheria za nchi zitiwazo; Sheria ya Kwanza ni Sheria ya GEPF ya Mafao ya Mfuko wa Mafao ya Wastaafu Namba Saba ya Mwaka 2013 (*The GEPF Retirement Benefit Fund Act Number Seven of 2013*); Sheria ya pili ni Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba Nane ya Mwaka 2013 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Number Three Act Number 8 of 2013*); Sheria ya Tatu ni Sheria ya Kura ya Maoni Namba Kumi ya Mwaka 2013 (*The Referendum Act Number 10 of 2013*); na Sheria ya nne ni

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Sheria ya Marekebisho ya Kodi ya Ushuru Namba Kumi na Moja ya Mwaka 2013 (*The Excise Management and Tariff Amendment Act Number 11 of 2013*).

Kwa sasa hizi ni Sheria kamili zinaweza kutumika kadiri nchi inavyotaka.

Katibu, hatua inayofuata.

### **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

#### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):**

Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na Hotuba ya Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka 2014/2015.

Randama za Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**SPIKA:** Bado kuna moja; Randama tayari nyingine bado, Hotuba ya Waziri Mkuu. Tunaendelea, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa niaba yake Mheshimiwa Fakharia.

#### **MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**SPIKA:** Mwenyekiti wa Kamati wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa! Wale wote wenye Hati za Kuwasiliisha wasogee mbele.

#### **MHE. DKT. HAMISI ANDREA KIGWANGALLA - MWENYEKITI WA KAMATI YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya TAMISEMI kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

#### **MHE. DUNSTAN L. KITANDULA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

### **MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MASUALA YA UKIMWI):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya masuala ya UKIMWI kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

### **MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU):**

Taarifa ya Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha kwa Ofisi ya Waziri Mkoo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

### **MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):**

Taarifa ya Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani juu ya Ofisi ya Waziri Mkoo (TAMISEMI) kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Waziri Mkoo (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**SPIKA:** Ningependa kuwataarifu kwamba, hizi taarifa mbili za Kambi ya Upinzani, hazipo Mezani kwangu, kwa hiyo, by the time mnatakiwa muwe mmegawa.

Tunaendelea, Katibu hatua inayofuata.

### **MASWALI NA MAJIBU**

Na.1

#### **Ujenzi wa Kituo cha Afya Shelui**

**MHE. MARTHA M. MLATA (K.n.y. MHE. DIANA M. CHILOLO)** aliuliza:-

Katika Kampeni ya Uchaguzi Mkoo Mwaka 2010 Mheshimiwa Rais aliwaahidi Wananchi wa Kata ya Shelui kuwa Serikali itajenga Kituo cha Afya Kata ya Shelui na kwa sababu hiyo Wananchi wameanza kuchangia fedha kwa ajili ya ujenzi huo:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Ujenzi wa Zahanati na Vituo vya Afya huibuliwa na Wananchi wenyewe kupitia Mpango wa Fursa na Vikwazo Katika Maendeleo (O and OD) na kutekelezwa kwa ubia kati ya Wananchi na Halmashauri.

Halmashauri huchangia gharama kidogo za utekelezaji wa Miradi hiyo kwa kuwezesha upatikanaji wa vifaa pamoja na usimamizi. Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kwa kushirikiana

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

na Wananchi, imeanza ujenzi wa Kituo cha Afya cha Shelui ambapo vifaa yakiwemo matofali 3,000 na mifuko ya saruji 70 vimeandaliwa.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais, Halmashauri katika bajeti ya mwaka 2013/2014, ilitenga shilingi 80,000,000 kutoka katika Mfuko wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) na shilingi 70,000,000 zilitengwa katika mapato ya ndani ya Halmashauri. Hadi sasa shilingi 36,717,500 zimetumika katika ujenzi wa kituo hicho cha afya kutokana na mapato ya ndani ya Halmashauri. Aidha, Halmashauri imetumia shilingi milioni tatu kutoka katika Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2014/2015, Halmashauri imetenga tena shilingi 75,872,000 kutokana na fedha za MMAM na shilingi milioni 65 zimetengwa kutokana na mapato ya ndani ya Halmashauri ili kuendelea na ujenzi huo. Aidha, Halmashauri imewasilisha Hazina maombi maalum ya shilingi milioni 350 ili kuongeza kasi ya ujenzi wa Kituo hicho cha Afya.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba itaendelea kutoa fedha kila mwaka kadiri zitakavyopatikana ili kukamilisha ujenzi wa Mradi huo.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Martha Mlata, swali la nyongeza!

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri.

Ni kweli kwamba Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wa Mbunge wa Jimbo umekuwa ukisaidia pamoja na Halmashauri. Ukingalia sasa hivi ni takribani miaka minne bado tunasusua kumaliza Kituo kile na Wananchi walijitolea wanaonekana kukata tamaa. Ni kweli Halmashauri ya Wilaya ya Iramba imejitahidi. Mimi swali langu Rais ni kwamba:-

Mheshimiwa Rais anapotoa ahadi na Wananchi wakaitikia kwa kasi na kwa nguvu zote kumuunga mkono, lakini bajeti inayotengwa kupeleka kwenye Halmashauri na kuwa haikidhi agizo hilo:-

Je, kwa nini Serikali isianzishe mpango au mchakato maalum kwamba, ahadi zote za Rais zikatengewa zikawa na Mfuko Maalum ili kutekeleza ahadi zote ambazo zinakuwa zimeahidiwa na Mheshimiwa Rais? Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi. Naomba majibu yawe mafupi na maswali yawe mafupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, kuhusu hii Constituency Development Catalyst Fund anayoizungumzia hapa, mimi napenda sana kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Mcemba, Mbunge wa Jimbo hili, amejitolea sana, ametoa hizo fedha tulizosema hapa shilingi milioni tatu, lakini pia amenunua na ambulance kwa ajili ya kusaidia katika Kata hii inayozungumza hapa.

Sasa kuhusu ahadi za Mheshimiwa Rais, sisi Rais akishatoa ahadi hakuna mjadala. Huwa hatukai tena tukaanza kusema zitatoka wapi. Ndiyo maana hapa kuna maombi maalum na tunawasiliana na Hazina ya shilingi milioni 350. Wakati huo huo ninapozungumza kwenye hii

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

current budget, utaona tumetenga shilingi milioni 80, milioni 75, mpaka hela za Local Government Capital Development Grant tumetenga kwa ajili ya Kituo hiki.

Namwomba Mheshimiwa Martha Mlata, aamini kwamba, tunafanya kazi hiyo. Katika jambo ambalo tumegeombana sana na Iramba ni kuhusu ahadi ya Rais na Mkurugenzi Mtendaji huko aliko anajaua ninachosema hapa. Kwa hiyo, awe na hakika kwamba tutafanya hivyo, sasa hivi tume-commit shilingi milioni 36 ndizo zitafanya kazi hiyo na kituo hicho kitajengwa kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kibona, naomba maswalil yawe mafupi la sivyo watauliza watu watatu tu!

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Katika llani ya Chama cha Mapinduzi, Wananchi walihidiwa kwamba katika kila Kijiji na katika kila Kata kutakuwa na Zahanati na Vituo vya Afya.

Nilitaka kufahamu mpaka sasa hivi Serikali imejipanga vipi kutimiza ahadi hizo kabla ya uchaguzi ujao?

**SPIKA:** Nilikuwa na wasiwasi utauliza habari ya lleje, kumbe ni zuri. Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kibona, Mbunge wa lleje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hii Programu ambayo anaizungumza ipo nchi nzima na ni maelekezo ya Serikali tuhakikisha kwamba, tunakuwa na zahanati katika kila kijiji. Pale vijiji vinapoonekana vipo vingi karibu karibu wanawenza wakaamua wakatafuta kituo kimoja ambacho watajenga.

Pili, kuhusu Vituo vya Afya navyo, hivyo hivyo tunashirikiana na Wizara ya Afya kuhakikisha vinajengwa. Progress Report yake ni kwamba, mpaka sasa hivi tunakwenda vizuri lakini hatujapiga hatua kubwa sana katika jambo hili. Sisi tunabeba dhamana hii ya kuhakikisha kwamba, tunaendelea kuhimiza ili tunapomaliza kipindi hiki cha miaka mitano tuone kwamba tumefikia lengo hilo liliowekwa.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Gekul, swali lingine la nyongeza!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa fedha ambazo Naibu Waziri amekuwa akizitaja katika mpango wa ujenzi wa zahanati ni fedha za Mpango wa Afya ya Msingi (MMAM), lakini fedha hizi zimekuwa hazipelekwi takribani miaka mitatu iliyopita, mfano, katika zahanati yangu ya Nakwa kule Babati, tunatenga kila mwaka shilingi 36,000,000 lakini hata kwenye Halmashauri nydingi wakati tunapitia bajeti za TAMISEMI, fedha hizo hazipelekwi.

Mheshimiwa Naibu Waziri, unaweza ukatuambia kwa nini fedha hizo zime-stop na haziendi kwenye Halmashauri hizo?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Gekul, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Gekul ni kweli kwamba, tumekuwa tunakutana na yeye mwenyewe yupo kwenye Kamati hii ya TAMISEMI, anachosema ni kweli hatuwezi kubishana.

Mheshimiwa Waziri Mkoo, kipindi fulani alionesa kabisa kwamba, hata OC zili kuwa haziendi, ingawa sasa kidogo kidogo tunaona jitihada za Serikali, hela hizi zimeanza kupatikana.

Sisi tunachofanya sasa hivi bado bajeti hii tunayozingumzia, kuna miezi mitatu ipo hapa katikati, tunachokifanya kikubwa tunawasiliana na Wizara ya Afya pamoja na Treasury, kuhakikisha hela hizi zinapatikana. Tutafanya jitihada kama anavyoshauri Mheshimiwa Mbunge, kuhakikisha kwamba, fedha hizi zinapatikana ili kazi zilizokusudiwa ziweze kufanyika. Hela hizi ndizo zinazotumika kwa ajili ya ukarabati wa zahanati, vituo, hata vile vifaa tiba na vitu vingine vinapatikana kuto kana na hela hizi.

**SPIKA:** Mnaona tumejibu kwa kifupi, naweza kumwita hata Mheshimiwa Mtutura, nafasi bado dakika tano zile zile.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Afya, michoro ya zahanati sasa hivi zinatakiwa takribani 800,000,000 ili uweze kukamilisha zahanati na kituo cha afya takribani bilioni 1.2; na kwa kuwa Serikali imetuwa ikitoa fedha kidogo kidogo, kwa mfano, shilingi 80,000,000 katika kuwezesha ujenzi wa Vituo vya Afya; kwa utoaji huo maana yake Kituo hiki cha Afya kitajengwa takribani kwa miaka kumi na tano.

Je, utekelezaji wa Sera hii utaweza kukamilika kwa wakati kama ilivyo elekezwa na Serikali yetu?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo, naomba kujibu swali la nyongeza la Abdallah Mtutura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kidogo imeni-confuse, yaani michoro tu shilingi milioni 800 mpaka 1.2 billion! Napata shida kidogo, ndicho anachokisema pale, siyo ujenzi anazungumzia michoro. Naomba anifafanulie kidogo maana nimeshindwa kuelewa anachozungumza ni nini!

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtutura!

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, michoro ambayo imetolewa na Wizara ya Afya ili itekeleze kujenga Vituo vya Afya na Zahanati inagharimu shilingi 800,000,000 kwa zahanati, ujenzi na Kituo cha Afya ni takribani bilioni 1.2 ndipo Kituo cha Afya kiweze kukamilika.

**SPIKA:** Anachosema siyo michoro peke yake, yaani ramani ile ndogo sana ni 800,000,000 na Kituo cha Afya ndio bilioni hizo, kwa hiyo, siyo mchoro.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, nimeelewa.

Nashukuru kwa ufanuzi huo, lakini jambo hili itabidi tukakae na watu, hatuna hizo! Jengo la zahanati si ni jengo moja tu kama darasa hivi na vyumba vingine vya Madaktari. Ninaomba kitu kimoja, kwanza, hatuna hizo takwimu, normally huwa inakwenda kwenye 30,000,000, sasa tunashangaa tunaposikia hili, lakini tuombe kwa sababu Mheshimiwa Abdallah Mtutura amelileta hapa na Mheshimiwa Seif na Naibu wake wapo hapa, tuta-compare notes ili kuweza kupata exact figure, lakini siyo hizi Mheshimiwa anazungumzia. Tuta-compare halafu tutampa figure kamili katika jambo hili.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na swali lingine.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona kila Mbunge ana viti viwili viwili msije mkadhani vipo wazi, maana waandishi wa habari watasema viti vipo wazi hapana, kila Mbunge ana viti viwili safari hii. Kila Mbunge ana viti viwili lakini ana microphone yake. Kwa hiyo, naomba ielewewe hiyo. (Kicheko)

Mheshimiwa David Kafulila, kwa niaba yake Mheshimiwa David Machali!

Na. 2

#### **Uhaba wa Vitabu na Madawati Shulen**

**MHE. MOSES J. MACHALI (K.n.y. MHE. DAVID Z. KAFULILA)** aliuliza:-

- (a) Je, ni kwa kiasi gani Shule za Tanzania zinakabiliwa na uhaba wa vitabu na madawati kwa ujumla?
- (b) Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo hili na litagharimu fedha kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, shule za msingi nchini zinahitaji madawati 3,302,678, yaliyopo sasa ni madawati 1,837,783 na upungufu ni 1,464,895. Kwa shule za sekondari, mahitaji ya madawati shule zote ni 1,648,858, yaliyopo sasa ni 1,231,440 na tuna upungufu wa madawati 417,418. Hali ya vitabu katika shule za msingi kwa sasa imefikia uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi watatu na kwa upande wa sekondari kitabu kimoja kwa wanafunzi watano.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa inatenga fedha na kupeleka katika Halmashauri zetu kwa ajili ya ununuzi wa vitabu na utengenezaji na madawati. Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 na Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, shilingi bilioni nne zilipelekwa katika

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Halmashauri zote kwa ajili ya madawati, ambapo Mkoa wa Kigoma ulipata shilingi milioni 174.9. Aidha, Serikali imeshaanza kusambaza katika Halmashauri mbalimbali sehemu ya madawati yaliyonunuliwa kwa fedha zilizotokana na fidia ya ununuzi wa rada.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kumaliza tatizo la vitabu na madawati shulen iifiko mwaka 2016. Katika kufikia azma hii, vitabu vinanunuliwa kwa pamoja (*centrally*) kupitia fedha za uendeshaji (*Capitation*), zinazotolewa kila mwaka na kuvisambaza mashulen. Aidha, shilingi bilioni 302 zinahitajika ili kufikia uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi katika kila somo kwa upande wa shule za msingi na shilingi bilioni 173 upande wa sekondari ili kila mwanafunzi awe na dawati. Aidha, pamoja na Mikakati ya Kitaifa inayoendelea, Halmashauri zimehimizwa kuweka kipaumbele cha madawati katika mipango na bajeti za kila Halmashauri kwa mwaka ili kukamilisha mahitaji ya madawati nchini.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Machali, swalii la nyongeza!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa kiasi cha takribani bilioni 302 zinahitajika ili kuweza kutatua matatizo ya vitabu na madawati ambalo lipo hivi sasa na limekuwa la muda mrefu; Serikali haioni ipo haja ya kuziagiza Halmashauri zote kwa kutoa Waraka Maalum kupitia own sources; na kwa kuwa pengine tumepega hatua sasa hivi sasa mpango ni kuhakikisha Halmashauri zote zinatenga asilimia 60 ya own sources kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ili kusudi tatizo hili tuweze kulimaliza kwa muda. Serikali ipo tayari kutoa Waraka huo mara moja kwenye Halmashauri zote?

(ii) Kwa kuwa ukiangalia kwenye shule mbalimbali hapa nchini wanafunzi wanakaa chini, tatizo la vitabu limedumu tena kwa muda mrefu sana na mmetuambia sasa hivi mnanunua vitabu centrally; mnaweza mkatueleza ni sababu gani zimefanya mnunue vitabu kwa pamoja nchi nzima na ni kwa nini msizipeleke kwenye Halmashauri uwezo pengine unaweza ukawa mdogo kwa sababu manpower inaweza kuwa ndogo pengine kwenye level ya Kitaifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibuu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Machali, kama ifuatavyo:-

Upo Mpango na Mkakati Endelevu unoaoendelea na Halmashauri zote nchini ambaa uliagizwa kwa Waraka wa kutumia own sources zao katika kila Halmashauri kwa ajili ya ununuzi wa madawati. Pia Halmashauri zote zenye misitu, wamepewa ridhaa ya kutumia misitu yao kutengeneza madawati ili kupunguza gharama na kupunguza tatizo la madawati katika Halmashari.

Mheshimiwa Spika, nilitaka pia kuchukua nafasi hii kuzipongeza Taasisi mbalimbali ambazo zinajitahidi sana kusaidiana na Serikali kupunguza tatizo la upungufu wa madawati nchini ikiwemo na Benki ya NMB, Taasisi ya Hassan Maajar Foundation, TEA, Taasisi ya WAMA, Airtel, lakini pia hata Wabunge kupitia Mifuko yao ya Mfuko wa Bunge, inasaidia sana kupunguza jambo hili. Kwa hiyo, tunaamini baada ya kipindi kifupi tatizo hili kwa kushirikiana na Serikali pamoja na Taasisi hizi tunaweza kupunguza tatizo la madawati.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, sababu za kununua vitabu centrally kwa fedha tulizokuwa tunapeleka kama *capitation shuleni*, kumekuwa na upungufu wa ununuzi wa vitabu hivi pindi tunapopeleka fedha kwa Walimu Wakuu kwenye shule zetu. Kwa kuwa mahitaji yetu sisi ni kupata vitabu na kwa kuwa Wizara tume-practise kununua vitabu centrally na tumepata mafanikio kwa kila shule kupata vitabu, tunaamini kwa utaratibu huu na kwa kuwa mahitaji ni ya vitabu, tutanunua vitabu centrally na tutavipeleka shuleni ili tuwe na control nzuri ya kujua tumepeleka vitabu vingapi, mahitaji yetu ni kiasi gani na tuna upungufu wa kiasi gani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Msabaha, swali la nyongeza!

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tuliambiwa chenji ya rada na rada ni suala la Muungano na kule Zanzibar watoto wana tatizo pia la madawati wanakaa chini. Je, Zanzibar nao wamenufaika vipi na hii chenji ya rada?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):**  
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Jambo hili limeshazungumzwa sana Bungeni, suala la chenji ya rada na suala la Muungano, lilishafafanuliwa kwamba, fedha za rada hazina uhusiano na suala la Muungano. Hii ndiyo sababu jambo hili lilikuwa limeshatengwa kwa ajili ya shughuli zetu Tanzania Bara. Mipango hii imeendelea kupangwa hapa Bungeni mpaka utekelezaji, tukiwa tunajua kabisa vitabu hivi na madawati haya yataenda kwenye shule zilizoko Tanzania Bara pekee.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata, Wizara ya Nishati na Madini. Mheshimiwa Mendrad Kigola, atauliza swali hilo.

Na. 3

### **Hitaji la Umeme Kituo cha Afya Nyololo**

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kituo cha Afya cha Nyololo ambacho kinahudumia watu wengi wa Jimbo la Mufindi Kusini, Maduma, Bunilasinga, Njonjo, Malangali na Nziri?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibuu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijiji (REA), imekamilisha mpango wa kupeleka umeme kwenye Kituo cha Afya cha Nyololo chini ya Mpango Kabambe wa Umeme Vijiji Awamu ya Pili. Mradi huu utakaotekelze na Mkandarasi aitwaye Sengerema

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Engineering Group Limited, utahusisha pia Vijiji vya Kiliminzowo, Mtambula, Udumuka, Lugolofu na Ihomasa.

Mheshimiwa Spika, itabidi unisamehe haya majina ni magumu sana.

Mheshimiwa Spika, kazi za mradi huu zinahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33, yenye urefu wa kilomita 60, ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 25 na ufugaji wa transfoma 11, pamoja na kuwaunganisha wateja wa awali wapatao 420.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa awali Mradi ulianza mwezi Aprili, 2014 na kazi zilizokamilika ni pamoja na survey na usanifu wa michoro kwa ajili ya ujenzi wa njia ya umeme. Kazi za uchimbaji wa mashimo na usimikaji wa nguzo inatarajiwa kuanza mwezi huu wa Mei, 2014. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2015 kwa gharama ya shilingi bilioni 2.7.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, naishukuru Serikali kwa kutoa majibu mazuri kwamba, Vijiji vya Kilimenzoo, Mtambula, Lugolofu na Ihomasa wanaweza kupewa umeme.

(i) Kwa majibu haya, kwa sababu Wananchi wale hawana umeme kule na hawatusikii saa hizi. Je, upo tayari kwenda kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini kufanya mukutano na kuwaeleza haya uliyowaambia leo?

(ii) Mpango wa Mwaka 2013/2014 ilipangwa kupeleka umeme katika Kata ya Malangali na umeme huo Serikali ilisema itachukua *line* ya Makambako ambapo Vijiji vya Nyigo, Iramba, Kinengembasi, Mbalamaziwa, Idetero, Ihawaga, Kiterewasi, Malangali hadi pale Ihowanza na walipangiwa 1.9 bilioni na kazi hii ilitakiwa iwe imeshaanza tangu mwaka jana mpaka sasa hivi bado kazi haijaanza. Je, unaweza ukawathibitishia Wananchi wale kwamba hela yao ile ambayo walipangiwa bdo ipo na kazi hiyo itaanza mara moja?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, suala la kwenda na yeye nadhani halina matatizo, tutapanga tu tuone ni kwa namna gani tunaweza tukaenda kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kata ya Malangali vilevile ipo katika mpango mwaka huu. Nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, muda utakapofika, fedha zitapelekwa na ujenzi utaanza mara moja.

**MHE. OMAR R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Kwa kuwa umeme na taratibu ambazo Serikali ilijiwekea kusambaza umeme vijijini, ingesaidia sana kupata umeme katika vituo vingi vya afya na zahanati ambazo Serikali inazitengeneza...

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**SPIKA:** Waziri wa Ujenzi na Mheshimiwa Njwayo, mbona mnavunja taratibu? Naomba mrudi mlilotoka. Mheshimiwa Nundu endelea.

**MHE. OMAR R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali iliweka utaratibu wa kusambaza umeme vijiji ambao ungesaidia sana kutatua matatizo katika vituo vya afya na zahanati. Mwaka juzi nilipouliwa swali kuhusu vijiji ambavyo vinapitiwa na umeme unaokwenda vijiji vingine kuwa vijiji hivyo navyo pia vingepatiwa umeme; ninataka kujua juhudzi za Serikali katika suala hilo zimefikia wapi na kwa kiasi gani vijiji ambavyo vinapitiwa na umeme unaokwenda kwenye vijiji vingine vimepatiwa umeme na hasa ukizingatia vijiji vilivyopo Mabokweni na Chongoleani ambavyo vinapitiwa na umeme unaokwenda katika Wilaya jirani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni Sera ya Serikali kwamba, maeneo yote yaliyo nyeti ikiwemo vituo vya afya, shule za sekondari, shule za msingi, mahali ambapo kuna shughuli za kijamii, Mradi wowote unaodhaminiwa na REA utafikia katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba, maeneo ambayo ameyataja wakati wa utekelezaji wa Mradi huu Awamu ya Pili yataweza kuangaliwa na kuhakikisha yanapatiwa umeme.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Akunaay, swali la nyongeza!

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, ningependa kupata ufanuzi wa Naibu Waziri kuhusu Miradi ya REA iliyopitishwa, REA ina uwezo gani kibajeti maana miradi ni mingi sana?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, sote hapa tulipitisha bajeti kupitia mafuta ili REA iweze kupata hela kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Umeme Vijiji. Hivyo, uwezo wa REA siyo tu kwa ajili ya hizo hela ambazo zimetokana na mafuta, vilevile REA inapewa hela na Serikali kiasi fulani cha kuweza kutekeleza Miradi hiyo. Vilevile kuna wafadhili wa nchi za nje ambao wanaisaidia REA kuhakikisha kwamba, tuatekeleza Miradi yetu.

Mheshimiwa Spika, REA ina uwezo wa kutekeleza Miradi, lakini haitatekeleza kwa siku moja, Miradi itakuwa inatekelezwa awamu kwa awamu kulingana na uwezo wa pesa itakavyokuwa inapatikana.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Assumpter Mshama!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Spika, nami sipo mbali na Mheshimiwa Kigola. Kwa namna ya pekee katika Jimbo langu la Nkenge, tulipewa vijiji 24 kwa ajili ya kupewa umeme tangu bajeti ya mwaka 2012, mpaka leo ni vijiji vitatu tu vimeweza kupatiwa umeme. Katika vijiji hivyo, niliomba priority katika Kata ya Isozi ambayo ina Shule ya Sekondari ya Tweyambe tumepata wafadhili kutoka

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Uingereza wakatupatia kompyuta zaidi ya mia moja, wametupatia kituo cha kompyuta, tuna *internet* na kuna kituo cha afya cha kung'oa meno. Naomba kuuliza ni lini tutapata huo umeme kwa ajili ya kusaidia na kuwatia moyo waliotusaidia?

**SPIKA:** Hilo swali kwa swali la nyongeza siyo sahihi, labda kwa sababu Waziri anajua, labda na yeze alienda kutolewa meno huko basi ajibu. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli hatutapeleka umeme sehemu wanapong'oa meno. Kwa sababu ameniuliza ni kwamba, katika Mkao wa Kagera, Mkandarasi anaitwa Alban, tayari amesharipoti kwa Mkuu wa Mkao na vilevile ameripoti kwenye Wilaya mbalimbali na ataendelea kutekeleza Mradi kama tulivyokubaliana katika Mkataba tuliosainiana naye kupitia Wakala wa Umeme Vijijini. Hivyo, awe na subira tu na nina uhakika kabisa umeme utafika katika maeneo mbalimbali kulingana na Mkataba ambao tumesaini na huyu Mkandarasi anayeitwa Alban.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa tuendelee na swali linalofuata,, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi.

Na. 4

### **Walimu Waliopolekwa Gabon Kufundisha Kiswahili**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Je, Tanzania imepeleka Walimu wangapi kufundisha Kiswahili nchini Gabon?

**SPIKA:** Kwanza kabisa, naomba nitumie nafasi hii, kuwapongeza Naibu Mawaziri na Mawaziri walioteuliwa katika kipindi ambacho hatukuwepo, hii ni mara yao ya kwanza ninawaongeza wote na ninawatachia utendaji mzuri wa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele yako na kujibu maswali katika nafasi hii mpya niliyopewa, naomba uniruhusu kwa dakika moja, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa Baraka alizotujalia katika Jimbo la Peramiho na katika familia yangu. Kwa namna ya pekee, nimshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniamini na kunipa majukumu haya ya kusaidiana na Waziri wangu, Dkt. Shukuru Kawambwa, lakini na Serikali kwa ujumla kufanikisha majukumu ya Wizara ya Elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013, Rais wa Jamhuri ya Watu wa Gabon, Mheshimiwa Omar Bongo, alikutana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, akamwomba Tanzania ipeleke Mhadhiri wa Kiswahili ili akafundishe Kiswahili nchini Gabon.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilipokea ombi hilo kutoka Serikali ya Gabon kuitia Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa nia ya kupatiwa Mhadhiri mmoja wa kufundisha Kiswahili katika Vyuo vya Elimu ya Juu nchini Gabon. Wizara iliwasiliana na Uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuagiza Uongozi utengeneze mchakato wa kupata Mtaalam wa Kiswahili aliye tayari kwenda kufundisha nchini Gaboni. Uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ulikamilisha taratibu zote zinazotakiwa na kufanikiwa kumpata Mhadhiri Mwandamizi na Mtaalam wa Fasihi za Lughya ya Kiswahili atakayekwenda kufundisha Gabon.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wakati taratibu za kushughulikia kibali zikiendelea, Mhadhiri huyo alipata fursa ya kwenda kunoa ubongo (Sabbatical Leave) nchini Ujerumani. Kwa mantiki hiyo, Wizara imeshakiagiza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kumpendekeza Mtaalam mwingine ili achukue nafasi hiyo. Wizara inasubiri uteuzi huo ambao utazingatia uzoefu na sifa nyiningine na mara baada ya kukamilika na kupokelewa kwa uteuzi huo, Serikali itahakikisha inamalizia mchakato na kumpeleka Mtaalam huyo nchini Gabon.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa nchi ya Gabon ilianza kutumia Lughya ya Kiswahili kufundisha kuanzia shule za msingi, sekondari na vyuo. Tanzania kupata nafasi moja ni ndogo sana. Je, Serikali imejipanga vipi sasa kuchangamkia fursa hizo ili kupunguza tatizo la ajira nchini mwetu?

(ii) Je Serikali imefanya juhudhi gani ya kuwaunganisha Wataalam wa Kiswahili wa Tanzania na nchi nyiningine za Kiafrika ili waweze kubadilishana uzoefu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Mariam Kisangi, mwalimu mwenzangu, kwa jinsi anavyoshughulikia masuala ya ajira kwa walimu hata nje ya mipaka ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahakikisha inaongeza fursa za walimu wa Kiswahili kufundisha nje ya nchi. Imeanza na mkakati wa kuongeza udahili wa wanafunzi ambao watajifunza shahada katika Vyuo vyetu Vikuu inayohusiana na Lughya ya Kiswahili. Tunao wanafunzi takribani mia nne sabini na nne tu ambao wanaendelea na mafunzo haya ya lugha katika nchi yetu ya Tanzania. Hivyo, tunatakiwa kuongeza idadi kwanza ya Wanafunzi watakaojifunza lugha katika Vyuo Vikuu ili tuweze kuwatafutia hizo fursa.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeshafanya mkakati wa kutosha wa kuwasiliana na Ofisi za Balozi zetu ambazo zinafanya kazi ya mahusiano ya kimataifa nje ya nchi yetu ya Tanzania na wao wameendelea kututengenezea fursa mbalimbali, ambazo zitatumika pia kuwahusianisha walimu wa Kiswahili na hitaji la ufundishaji wa Lughya ya Kiswahili katika nchi zitakazokuwa zinahitaji Wataalam wa namna hiyo.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina swali moja dogo la nyongeza:-

Wakati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizindua Bunge la Tisa, alisema kwamba, kuna fursa nydingi za kufundisha Kiswahili katika nchi mbalimbali na akasema wakati huo alikuwa na maombi ya Walimu au wafundishaji 500 kutoka nchini Libya. Kwa majibu ya

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Waziri sasa hivi kwamba nafasi moja tu ya Gabon imechukua zaidi ya miaka tisa hajijatekelezwa; je, Serikali kweli ipo serious katika ku-promote Kiswahili na kuendeleza Kiswahili katika nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa nchi ya Libya ilikuwa na mahusiano ya karibu sana na nchi yetu ya Tanzania na kwa kipindi kirefu sana tumekuwa tukipeleka Wataalam wetu katika nchi ya Libya ili kusaidia kufundisha Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, hali tete inayoendelea katika nchi ya Libya, ilifanya hapa katikati speed yetu ya kupeleka wataalam ipungue. Hali itakapotengemaa na kuwa salama zaidi, mpango ule tuliokuwa tunautumia wa kupeleka Walimu wetu nchini Libya utaendelea na hatuna tatizo la mahusiano ya ufundashaji katika nchi ya Libya na tumeendelea kuagiza Balozi nyininge watuhusianishe na nchi nyininge na tutaendelea kufanya hivyo.

**SPIKA:** Ahsante. Naomba tuendelee na swali linalofuata, Mheshimiwa Joseph Selasini, atauliza swali hilo.

Na. 5

### **Mikopo ya Elimu ya Juu**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI** aliuliza:-

Pamoja na Serikali kuboresha Mifuko ya Mikopo ya Elimu ya Juu bado wanafunzi wengi hawajanufaika na mfumo huo:-

(a) Je, ni wanafunzi wangapi waliokopeshwa wamepata kazi na wamemaliza kulipa mikopo yao?

(b) Je, Serikali ina mpango gani kwa wanafunzi waliokopeshwa lakini hawajapata kazi baada ya kumaliza masomo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014 jumla ya Wanafunzi 293,765 wamekopeshwa mikopo yenye thamani ya shilingi 1,741,674,673,677.58. Idadi hii inajumlisha wanafunzi 95,864 wanaendelea na masomo mwaka huu wa 2013/2014, wanafunzi 34,620 walioko katika kipindi cha matazamio (*grace period*) ya mwaka mmoja na wanafunzi 163,281 ambao wamemaliza kipindi cha matazamio. Aidha, kiasi cha shilingi 512,450,044,089.75 za mikopo ya wanafunzi 163,281 tu ndiyo imeiva kwa kuanza kurejeshwa na mikopo ya shilingi 1,229,224,669,187.83 ya wanafunzi 130,484 haijaiva kwa kurejeshwa kwa sababu wanafunzi wengine waliopata mikopo hiyo bado wanaendelea na masomo wakati wengine wako kwenye kipindi cha matazamio cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha mikopo ambayo inatakiwa kuwa imerejeshwa hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014 ni mikupuo yenye thamani ya jumla ya shilingi 86,529,873,106.38, sawa na

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

asilimia 16.88 ya mikopo iliyociva. Hadi kipindi hicho, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imekusanya kiasi cha shilingi 47,349,582,373.11, sawa na asilimia 55 ya mikopo ambayo ilipaswa iwe imesharejeshwa. Kati ya mikopo hii iliyorejeshwa, jumla ya wanufaika waliomaliza kulipa mikopo yao ni wanufaika 8,454. Aidha, kutokana na mfumo wa ajira tulionao nchini, wanufaika 52,549 wameajiriwa katika sekta rasmi na zisizo rasmi na wanarejesha mikopo yao, wakiongozwa na waajiriwa wa Serikali za Mitaa wapatao 17,521.

(b) Mheshimiwa Spika, Sheria Na. 9 ya Mwaka 2004, ilioanzisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, inamtaka mnufaika wa mkopo aanze kurejesha mkopo baada ya mwaka mmoja wa matazamio ili aweze kujipanga vizuri. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, mkopo haujafungamanishwa na mnufaika kupata ajira bali imezingatia kuwa shahada anayopata mnufaika ni mtaji tosha hivyo anawajibika kulipa mkono huo. Hata hivyo, wanafunzi wanaopewa mikopo ya kuwawezesha kusoma katika Taasisi za Elimu ya Juu, huwa wanapata stadi za kuwawezesha kujajiri au kuajiriwa, ikizingatiwa kwamba soko la ajira ni huru. Aidha, Serikali imekuwa ikiandaa mazingira wezeshi ili kuwasaidia wahitimu kujajiri au kuajiriwa pindi wamalizapo masomo yao.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kumekuwa na manung'uniko mionganoni mwa Wananchi kwamba, wanufaika wa mikopo ya Wanafunzi walio wengi ni watoto wa baadhi ya vigogo na baadhi ya wenyewe uwezo:-

(i) Kwa kuwa Bunge hili mara kadhaa limekuwa likiagiza Serikali kuisimamia vyema Bodi ya Mikopo ili kuhakikisha watoto wa maskini wanufaika pia na mikopo hii. Je, Serikali imetekeleza vipi agizo hili?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa kuwa, gharama za elimu ya juu ni kubwa sana hapa nchini na zinatofautiana kati ya Chuo kimoja na kingine. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba, gharama hizi zinafanana na zinakuwa nafuu, ili kuweza kuwasaidia watoto wengi wa nchi hii kuweza kupata elimu ya juu?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA JUU:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Selasini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taratibu za kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu zimefanyiwa marekebisho mara kadhaa kufuatana na mahitaji kama ambavyo wawakilishi wa wananchi, kwa maana ya Bunge lako Tukufu, lilivyoishauri Serikali mara kwa mara. Kigezo kikubwa sasa hivi cha kupata mikopo hii ni uhitaji, kwa maana yule anayetaka mkopo ni yule ambaye hawezi kugharamia elimu ile, kigezo hiki ndio kikubwa. Zaidi yake tumeweka ulemavu kama moja katika vigezo, ama ulemavu wa mwanafunzi au ulemavu wa mzazi au mlezi, lakini pia namba tatu ni vipaumbele vile vya fani ambazo Taifa hili linataka lizijenge kama vile Ualimu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika hali hiyo hakuna mtoto wa kigogo ambaye anaweza akajitekeza humo kuchukua mikopo hii na kwa ujumla Bodi inafanya kazi nzuri kuhakikisha kwamba, haya yanatekelezwa na tunakwenda vyema. Shida yetu kubwa sasa hivi ni kupata tu pesa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa swalii la pili ambalo linahusu ada katika vyuo mbalimbali, kwa bahati zoezi hili mwaka huu tumelikamilisha. Tume-commission timu ambayo imeangalia na kuchunguza katika vyuo vyetu gharama halisi ya kumfundisha mwanafunzi katika programu mbalimbali katika vyuo vyote nchini mwetu. Ripoti imekamilishwa, tumetambua na umewekwa utaratibu maalum wa kukokotoa ada katika programu mbalimbali katika vyuo vya Serikali na

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

visivyo kuwa vya Serikali. Sasa hivi vyuo vyetu vyote vindelekezwa namna ya kutumia program hiyo, ili kukokotoa ada kwa hivyo, hakutakuwa na tafizo kubwa kuhusu ukokotoaji wa ada.

**SPIKA:** Tunaendelea. Katika Kipindi cha Bajeti, muda wa Maswali ni saa moja, lakini kwa sababu tumetumia muda kwa mambo mengine, kuapisha na kuwasilisha nyaraka nyingi, naongeza muda wa dakika 20.

Sasa nawaita Wizara ya Maji, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh?

Na. 6

### **Utaratibu wa Uvunaji wa Maji ya Mvua**

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH** aliuliza:-

Mabadiliko ya tabianchi yamesababisha kuwa na vipindi virefu vya ukame na wakati mwagine kunyesha mvua kubwa sana na kusababisha mafuriko katika maeneo mbalimbali ya nchi:-

- (a) Je, Serikali imefikia hatua gani katika mkakati wake wa kujenga mabwawa ya kuhifadhi maji yatakayosaidia kutunza maji ili yasipotee bure?
- (b) Elimu ya uvunaji wa maji ya mvua kwa wananchi imeleta mafanikio kwa kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mkakati wa kuhakikisha maji ya mvua yanahifadhiwa na kutokopotea bure, Serikali inaendelea na ujenzi na ukarabati wa mabwawa katika maeneo mbalimbali nchini. Utafiti kwa ajili ya ujenzi wa miradi mikubwa ya mabwawa yakiwemo mabwawa ya Farkwa, Lugoda na Kidunda kwa ajili ya matumizi mbalimbali, yakiwemo kuzuia mafuriko, umeanza.

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Kidunda litajengwa katika Mto Ruvu kwa ajili ya kuhakikisha Mto Ruvu unatiririsha maji mwaka mzima, ili kukabiliana na upungufu wa maji kwa wakazi wa Jiji la Dar-es-Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani.

Bwawa la Lugoda/Ndembera litajengwa katika Mto Ndembera kwa ajili ya kuhakikisha Mto Ruaha unatiririsha maji katika mwaka mzima. Bwawa la Farkwa litajengwa katika Mto Babu kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa maji katika Mji wa Dodoma.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuwaelimisha wananchi juu ya faida za uvunaji wa maji ya mvua. Hadi mwezi Machi 2014, Serikali kuitia Halmashauri imejenga jumla ya matenki ya mfano 675 ya uvunaji wa maji kwenye maeneo mbalimbali zikiwemo taasisi kama shule na zahanati. Teknolojia hii imewezesha wananchi kuvuna maji kwa ajili ya kilimo, mifugo na matumizi ya nyumbani katika maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Wizara, Serikali inawashauri Waheshimiwa Wabunge kwa kushirikiana na Halmashauri husika kuwashamasisha

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wananchi kujichimbia malambo madogo madogo kwa ajili ya matumizi yao mbalimbali kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zilizopo.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, mabadiliko ya tabianchi yanasaababisha maafa makubwa ya mafuriko na hata kusababisha vifo kwa wale wananchi wanaoishi mabondeni. Pia wakati mwiningine wananchi hawa wanakaidi amri halali ya Serikali ya kuwataka wahame katika maeneo yale. Je, Serikali ina mkakati gani mahsus wa kuwalazimisha wananchi hao kuhama mabondeni, ili kunusuru maisha yao na maisha ya watoto wao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kumetokea mafuriko mbalimbali na wanaoathirika zaidi ni wale ambao wanaishi mabondeni. Nitumie fursa hii kuwaomba wananchi hao kuelewa tu kwamba, majanga haya yataendelea kutokea mwaka hadi mwaka na kuendelea kung'ang'ania kukaa katika maeneo haya kutaleta maafa makubwa zaidi. Serikali itatoa ushirikiano na kuwahamasisha wananchi hao kuweza kuhama katika maeneo hayo bila kutumia nguvu, lakini waelewe athari kubwa itakayopatikana kwa mafuriko yatakayoendelea kutokea.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Ningependa nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri, ameainisha kwamba, ujenzi wa Mabwawa ya Lugoda na Kidunda, hivi ni lini Serikali mtalipa jambo hili kwa umuhimu wa hali ya juu kujenga Bwawa la Kidunda?

Mheshimiwa Spika, athari iliyoweza kutokea katika eneo la Ruvu, watu wamekaa pale zaidi ya siku tatu, siku nne, maji yamejaa pale, kama bwawa lingekuwa limejengwa maji haya si yangeweza kuhifadhiwa? Hatuna tatizo la maji, tuna tatizo la water management, kwa nini hamlichukulii hili jambo kuwa lina umuhimu?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mangungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, mpango ya ujenzi wa Bwawa la Kidunda umechukua muda mrefu kwa sababu mradi wenyewe ni mkubwa na unahitaji fedha nyingi pamoja na mahitaji katika kufanya utafiti juu ya athari za mazingira na za kijamii. Hata hivyo, kazi hii imekamilika ya awali na sasa hivi Serikali inashirikiana na Benki ya Dunia ili kuhakikisha kwamba, bwawa hilo linajengwa.

Katika hatua ya hivi sasa tunatengeneza barabara kutoka barabara kuu ya Dar-es-Salaam – Morogoro kwenda mpaka kwenye bwawa na tumeweka katika bajeti yetu hii inayokuja fedha kwa ajili ya matayarisho ya awali ya ujenzi wa bwawa hilo.

Na. 7

### **Mradi wa Maji wa Nyang'hangaa – Buhumbi**

**MHE. RICHARD M. NDASSA (K.n.y. MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU)** aliuliza:-

Mradi wa maji wa Nyang'ahanga – Buhumbi tangu uanze mwaka 2001 ni visima virefu viwili tu vimekamilika hadi leo na katika Mradi huu Mheshimiwa Waziri wa Maji aliahidi kutoa Shilingi milioni mia mbili (200,000,000/=) ili awamu ya kwanza ya ujenzi wa tenki la kuhifadhiwa maji uweze kuanza.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Je, ahadi hiyo imetekelozwa kwa kiwango gani na kama bado ni lini itatekelezwa?

### **NAIBU WAZIRI WA MAJI** aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu Swalil la Mheshimiwa Dokta Festus Bulugu Limbu, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Magu ilianza utekelezaji wa mradi wa maji ya Nyng'hanga – Buhumbi mwaka 2001. Visima virefu viwili vyenye uwezo wa kuzalisha jumla ya lita 17,000 kwa saa vilichimbwa kati ya visima vinne vilivyokuwa katika mpango. Mwaka 2009 ulifanyika usanifu wa kusambaza miundombinu ya kusambaza maji kwa visima vilivyochimbwa, hata hivyo ujenzi wake haukufanyika kutohana na kukosekana kwa fedha. Katika mwaka 2013 Serikali ilioa ahadi ya kuapatia Mradi huo shilingi 200,000,000 ili kuendeleza utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya ahadi hiyo, Mradi huu umefanyiwa mapitio ya usanifu na kubainika kuwa unagharimu shilingi milioni 954.6 na unalenga kuwapatia huduma ya maji safi na salama wananchi wapatao 10,097 katika Vijiji vya Nyang'hanga – Buhumbi na Iseni.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka 2014/2015 Wizara itashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Magu kujenga tenki lenye ujazo wa mita 225 na Vituo 14 vya kuchotea maji. Kazi nyingine zitakazotekelozwa katika mradi huu ni pamoja na ununuzi na ufungaji wa pampu, ujenzi wa Kituo cha Kusukuma Maji, ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya usambazaji maji eneo la mradi. Kazi hizi zitatekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha. Mradi huu utaendelea kutekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nisahihishe kwa sababu, majina haya ni ya Kisukuma ndio maana Mheshimiwa Waziri anashindwa kuyatamka vizuri; ni Kijiji cha Nyang'hanga na Buhumbi.

Mheshimiwa Spika, swali; kwa sababu Vijiji vya Nyang'hanga, Buhumbi na Iseni ni vijiji ambavyo viko mbalimbali, lakini Mheshimiwa Waziri katika jibu lake amesema kwamba, watajenga tenki lenye ujazo wa mita 225 kwa Vituo 14; Vijiji hivi viko mbalimbali, tenki lina ujazo wa mita 225. Ningependa kujua hilo tanki litajengwa katika Kijiji gani Nyang'hanga, Iseni, Buhumbi au Nyashoshi?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Itabidi mumkaribishe. (Kicheko)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli, kwamba tume sema katika majibu ya msingi kwamba, Vijiji vinavyolengwa ni Nyang'hanga, Buhumbi na Iseni. Kwa hiyo, ni kwamba, mradi huu unagharimu shilingi milioni 954.6 na hizi ni cubic metre zinazoelezewa hapa 225. Lakini fedha ambazo zimetengwa kwa mwaka huu kwa kuanzia ni kama milioni 323 kwa hiyo, wakati wa Bajeti zikipitishwa, kazi zitakazoanza kufanywa ni hizi ambazo nilikuwa nimezitaja na vituo hivyo 14.

**SPIKA:** Naomba tuendelee na swali lingine kwa sababu muda wenye wewe unakwisha.

Na. 8

### **Mpango wa Kuwasogezea Wananchi Huduma za Afya Karibu**

**MHE. FAKHARIA SHOMARI KHAMIS** aliuliza:-

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Serikali ilikuwa na mtazamo mzuri wa kuwasogezea wananchi wake huduma za afya karibu kwa kuwajengea uwezo mzuri wa matibabu ya ndani badala ya kwenda kutibiwa nje na kupambana na maradhi yanayoathiri na kuua kwa kuongeza Wajuzi na Madaktari:-

- (a) Je, Serikali imefanikiwa kiasi gani katika utekelezaji wa jambo hilo?
- (b) Je, ni Madaktari wangapi wamesomeshwa katika vyuo vilivyopo nchini na wangapi wamesomeshwa vyuo vya nje ya nchi?

### **NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa vile na mimi ni mara ya kwanza nasimama mbele hapa kujibu maswali baada ya uteuzi. Shukrani zimwendee sana Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia kufika hapa, lakini pia Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Tanzania, kwa uteuzi alioufanya. Wanaserengeti kwa muda huu nina hakika kwa ajili ya majukumu, naomba uvumilivu waliokuwa nao uendelee na tutaendelea kuwa pamoja, lakini nashukuru sana kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Spika, pia wewe mwenyewe binafsi, Waheshimiwa Mawaziri, Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano wenu mzuri ambao mmeutoa katika muda wote na familia yangu kwa uvumilivu mkubwa waliokuwa nao.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2007 Serikali kupitia Wizara yangu imekuwa ikitekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), mpango huu ni wa miaka 10 (2007 – 2017). Lengo kubwa la mpango huu ni kusogezeka huduma za afya karibu na wananchi na kuimarisha mfumo wa utoaji wa huduma za afya kwa kujenga na kukarabati vituo vya kutolea huduma, kuwa na Wanataaluma wanaotosheleza katika kila ngazi ya kutolea huduma na kuboresha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kuimarisha mfumo wa rufaa.

(a) Mheshimiwa Spika, mafanikio ya utekelezaji wa MMAM ni katika maeneo yafuatayo:-

- Vituo vya kutolea huduma vimeongezeka kutoka 5,379 mwaka 2006 hadi 6,663 mwaka 2012; hivyo kuwepo na ongezeko la vituo vipatavyo 1,284.
- Ili kuongeza idadi ya Wataalam wa Afya Nchini, limekuwepo ongezeko la Wanafunzi watarajali (Pre-Service) wanaojiunga na Vyuo vya Afya kutoka 3,025 mwaka 2007 hadi 7,956 mwaka 2013.
- Vibali vya ajira kwa Wataalam wa Afya vimeduwa vikiongezeka, ili kutoa fursa ya kuongeza watumishi wanaotoa huduma ya afya. Vibali vimeongezeka kutoka 6,437 mwaka 2007 hadi 8,602 mwaka 2013. Katika kipindi hiki idadi ya vibali vilivyotolewa ni 43,399 vikiwemo vya mwaka huu ambavyo ni 11,221.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(b) Mheshimiwa Spika, kama ilivyo katika fani nyingine za afya, udahili wa wanafunzi wanaochukua mafunzo ya Uadtari umekuwa ukiongezeka kutoka wastani wa wanafunzi 50 waliokuwa wanajunga na Chuo pekee cha Muhimbili katika miaka ya 80 hadi kufikia wanafunzi 1,077 mwaka 2012.

Ongezeko hili limetokana na ongezeko la Vyuo Vikuu vinavyotoa mafunzo ya Uadtari kufikia nane pamoja na ongezeko la udahili katika vyuo hivyo. Mwaka 2012 walihitimu Madaktari 617 hapa nchini, aidha wastani wa Madaktari 40 kufuzu Shahada zao za kwanza za Uadtari nje ya nchi. Pia, Wizara imekuwa ikifadhili mafunzo ya uzamili kwa Madaktari ndani na nje ya nchi katika mwaka wa masomo 2012/2013, jumla ya Madaktari 417 wamekuwa wakiendelea na mafunzo, 384 ndani ya nchi na 33 wakiwa nje ya nchi.

**MHE. FAKHARIA SHOMARI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyyoatoa kwa faida ya Watanzania, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, lengo kuu la Wizara kujenga nyumba kila Wilaya 10 na tayari baadhi ya Wilaya wameshajenga na baadhi Mikoa mingine imo katika ratiba ya kujengwa, lakini kuna baadhi ya mikoa haijaaishwa bado kujengwa. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuniambia na Mikoa hiyo mingine itajengwa lini au itajengwa na nani wakati kwenye Ratiba haimo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa usomeshaji wa Madaktari unakuwa kwa kasi katika Wizara ya Afya. Sasa nina swali dogo tu la nyongeza kwamba, kila Daktari atahudumia Wagonjwa wangapi kwa siku ili kuokoa afya za Watanzania? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Fakharia kwa maswali mawili ya nyongeza, naomba niyajibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu masuala ya nyumba, ili kuwabakiza Watumishi wa Afya katika sehemu zao za kazi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Mradi wa Kupunguza Vifo vya Akinamama kutokana na Uzazi inaendelea na ujenzi wa nyumba za watumishi katika Mikoa ya Mara, Tabora na Mtwara kwa kutumia fedha kutoka African Development Bank. Aidha, kupitia Mradi wa Global Fund nyumba 90 kati ya 310 zimejengwa katika kipindi cha mwaka 2011/2012; nyumba 50 zimejengwa Mikoa wa Mtwara na nyumba 40 zitajengwa Mikoa wa Rukwa. Nyumba zinazosalia zitajengwa Mikoa ya Lindi, Morogoro, Singida, Manyara na Pwani.

Mheshimiwa Spika, lengo la mpango huu ni kujenga vyumba 10 kila Wilaya na Vituo vya Serikali na Mashirika ya Dini.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa wastani ambao Mtanzania, mto Huduma ya Afya anapaswa kutoa huduma ni kati ya wagonjwa 30 mpaka 50 wakati wa zamu akiwa kazini. Kwa hiyo, hicho ndio kiwango ambacho kimepangwa katika mustakabali wa nchi yetu.

**SPIKA:** Ahsante, tuendelee na swali linalofuata, nakwenda na muda, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo!

Na. 9

**Kujenga Hospitali ya Rufaa kwa Mikoa ya Kusini**

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Serikali imekuwa ikiwaahidi wananchi wa Mikoa ya Kusini kuwa itawajengea Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mtwara:-

Je, maandalizi na maendeleo ya ahadi hii yamefikia hatua gani?

### **NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote Wizara inapenda kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa Mradi huu wa kujenga Hospitali ya Rufaa katika Mikoa ya Kanda ya Kusini, Manispaa ya Mtwara – Mikindani.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ipo katika hatua za utekelezaji wa mradi huu ambapo hadi sasa hatua zifuatazo zimekamilika. Moja, katika mwaka huu wa fedha 2013/2014, mradi huu umetengewa bajeti ya shilingi milioni mia saba ambayo sasa Hazina imeshatoa kiasi cha shilingi milioni mia nne kwa mwaka wa fedha. Pia kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 shilingi bilioni tatu zimekwishatengwa kama Bunge litakuwa limepitisha bajeti ijayo.

Pia kutohana na ufinyu wa bajeti Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iliamua kutekeleza mradi huu kwa awamu hadi sasa awamu ya kwanza ambayo ni kujenga uzio kuzunguka eneo lote la hospitali tayari kilomita 2.7 zimeshakamilika.

Mheshimiwa Spika, tatu, mwaka huu wa fedha 2013/2014, Serikali inaendelea na awamu ya pili inayohusisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje yaani OPD (*Out Patient Department*) kazi zinazoendelea zinahusisha ujenzi wa msingi, jamvi, nguzo na ngazi ambao utagharimu jumla ya shilingi bilioni 1.7 kazi ambayo imeshaanza na inaendelea. Kazi za awamu nyingine zitahusisha ujenzi wa idara nyingine kulingana na uhitaji na uwezo wa kifedha wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha kutohana na mtiririko mdogo wa fedha kasi ya ujenzi ni ndogo na kwa kuliona hilo kama nilivyoeleza hapo juu, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni tatu katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2014/2015. Vile vile Serikali iko katika jitihada mbalimbali za kutafuta vyanzo vingine vya fedha ili Hospitali hii ikamilike na kutoa huduma zinazotarajiwा.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa uamuzi wa kujenga Hospitali hii ya Rufaa ya Kanda ya Kusini pale Mtwara ulifanywa wakati wa Serikali ya Awamu ya Kwanza, Serikali iliyongozwa na Marehemu baba yetu wa Taifa Mzee Nyerere na jambo hili lilitangazwa hapa Bungeni yaani kwenye taratibu za Bunge na aliyekuwa Waziri wa Afya wakati huo Dkt. Leader Strling, lakini jambo hili limekuwa linachukua muda mrefu na pole pole sana.

Mheshimiwa Spika, naweza kutoa mifano, kwanza mchakato wenyewe umekuwa mrefu lakini hata kutengwa kwa bilioni tatu zinazotarajiwा kwa mwaka huu wa fedha wakati gharama halisi ni bilioni sabini. Je, Serikali haioni kwamba haiwatendei haki wananchi wa Mikoa ya Mtwara na Lindi ambao wamekuwa wakitumia gharama kubwa kusafiri kufuata huduma ya Hospitali ya Rufaa Muhimbili? Tangu juzi kuna wagonjwa pale maeneo ya Manzese Kilwa wamekwama kwa sababu barabara ile ni chafu na hiyo pengine wanaweza kupata hata matatizo ya vifo pale na magonjwa mengine wakazidiwa pale.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa jambo lolote linalopangwa na Serikali hasa miradi inakuwa na wakati maalum wa utekelezaji yaani *timeframe*. Je, Serikali inatuambia nini sasa mradi huu utakamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ni ile awamu ya kwanza ya ujenzi wa Hospitali hii, ni kweli mchakato umekuwa unachukua muda mrefu kwa sababu ya hali halisi ya upatikanaji wa kifedha na kama nilivyojibu katika jibu la msingi Serikali upo mpango wa kuanza kuangalia uwezekana wa kupata wadau wengine kwa ajili ya kusaidiana na bajeti ya Serikali. Ndiyo sababu hii shilingi bilioni tatu ambayo tumeomba na imekuwa *ring fenced* na imekingwa iweze kuanza kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaona dhahiri kwamba, mahitaji ya huduma ya afya kule ni kubwa kama tulivyojionea sisi wenyele tulivyojionea na Kamati mwezi wa Pili pale site Mikindani na kweli *influx* ya wagonjwa ni kubwa na wengine hata wanatoka nje ya nchi kule Msumbiji na suala hili lipo mpaka kule Masasi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala hili Serikali imedhamiria kwa dhati kwa hali halisi au muongezeko wa wananchi kule kwa ajili ya fursa kubwa ambayo imejitokeza ya uwekezaji wa mafuta na gesi na pia ujenzi wa viwanda vikubwa ikiwemo Kiwanda cha Saruji cha Dangote. Kwa hiyo, Serikali imedhamiria kwa dhati kabisa kujenga hospitali hii.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba, ni lini mradi huu utakamilika katika maelezo yangu ya awali katika jibu la msingi kulingana na upatikanaji wa fedha na wadau mbalimbali ambaao Serikali ina mpango wa kufanya mazungumzo ya karibu, itasaidia sana kufikia ujenzi wa Hospitali hii iweze kutoa huduma katika Kanda hii ya Kusini na tunawashukuru sana wananchi wa Kusini kwa sababu wanao mpango vile vile wa kuongeza Mkoa. Hii yote ni dhahiri kwamba, katika mpango wa Serikali ni lazima kuongeza huduma za afya katika eneo hilo.

**SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge muda umekwisha na tumeongeza dakika ishirini na tano na maswali pia yamekwisha.

Naomba niwatambue wageni tulionao katika Gallery ya Spika; kwanza kabisa ni wageni wafuataa:-

Wageni wa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ambaao ni familia yake; yupo Mheshimiwa mama Salma Kikwete, ahsante sana, hili siyo Bunge la Katiba la kupiga kelele, tunapiga makofi kwa namna ya Ubunge, siyo hivyo mnavyofanya, naombeni sana. Ahsante mama kwa kuja. (*Makofi*)

Tuna Dokta Rehema Nchimbi yeye ni Mkuu wa Mkoa wetu hapa Dodoma, asante sana tupo katika nchi yako hapa.

Tuna ndugu Arafa Kikwete, mke wa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, ahsante karibu madam, mtunze mume wako aweze kufanya kazi ya siasa, maana yake wewe ndiyo wajibu wako.

Pia yupo ndugu Stephen Kazidi, huyu ni Katibu wa CCM Mkoa.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Halafu yupo ndugu Miraji Kikwete, ahsante sana, yuko ndugu Seleman Kikwete, yuko ndugu Waziri Mbeyu, yuko ndugu Mkono Steven, yuko Khalfan Kiwamba, karibu sana, yuko ndugu Kibwana Matokeo, yuko ndugu Omary Masola na yupo ndugu Ramadhani Said ahsante sana. (Makofij)

Hawa ni wale waliokaa kwenye viti vya Mheshimiwa Spika, lakini kuna wageni wake wengine themanini wa Mheshimiwa Ridhiwani kutoka Jimbo la Chalinze, naomba hapo mlipo msimame wote, asante sana na hongereni kwa kazi nzuri ya kuweza kumpitisha kijana wetu kuingia katika Bunge letu. Ahsanteni sana. (Makofij)

Sasa nina wageni wengine wa Mheshimiwa Godfrey Mgimwa ambaa ni familia yake nao ni ndugu Jane Kipongo Mgimwa, mama yake, yupo ndugu Robby Mgimwa, mke wake, karibu sana. Nikutakieni kazi njema na yupo ndugu Flora Mgimwa, dada yake, ahsante sana nafurahi kuwaona. (Makofij)

Pia yeye anao wageni wengine hamsini kutoka Jimbo la Kalenga Iringa. Naomba wasimame walipo, hongereni nawashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya ya kuweza kuhakikisha bwana Mgimwa anaweza kuwa Mbunge katika Bunge letu. (Makofij)

Pia nina mgeni mwininge anaitwa ndugu Haruna Mbeyu, yeye ni kiongozi wa Watanzania wanaoishi Uingereza. Ahsante sana tunawatakatia mafanikio huko mliko. (Makofij)

Vile vile wageni wengine wote ambaa hatukuwataja hapa, lakini wote mnakaribishwa kwa sababu Bunge ni la kila mtu anayeweza kupata nafasi anaingia, karibuni sana.

Matangazo ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo kitakachofanyika katika ukumbi wa Hazina Ndogo, nafikiri mnakufahamu.

Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Andrew Chenge, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo saa saba na robo mchana kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo. Kikao hicho kitafanyika katika ukumbi wa Msekwa B. kwa hiyo, hawa ni wachache ambaa wameomba wafanyiwe kazi.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba hatujapata *briefing* yetu wenywewe ya namna tutakavyofanya kazi katika kipindi hiki cha bajeti. Kwa hiyo, tunalazimika sasa hivi baada ya kuahirisha kikao hiki tukutane katika ukumbi wa Msekwa, tukaweze kufahamishana mambo ambayo ni muhimu kwetu katika kuendesha kikao hiki. Kwa hiyo, nikahirisha kikao hiki tunakwenda ukumbi wa Msekwa, halafu tutorudi tena jioni saa kumi na moja kumsikiliza Waziri Mkuu kwenye hotuba yake.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge kutokana na maelezo haya na kwamba sina tangazo lingine, naomba niahirisha kikao cha Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(Saa 4.30 Asubuhi Bunge lilahirishwa Mpaka  
Saa 11.00 Jioni)  
(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

### HOJA ZA SERIKALI

#### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama ambavyo tumeshauriana katika kikao cha briefing, Bunge letu hili la bajeti ni tofauti na Mabunge mengine, muda wake umepungua sana kutokana na muda wa mwezi mzima ambao ulitumika katika kushughulikia Bunge Maalum la Katiba.

Kwa kawaida Bunge la Bajeti baada ya mabadiliko tuliyoyafanya mwaka jana lilipaswa kuanza tarehe 6 Aprili, ndiyo Waziri Mkuu angesoma Hotuba yake, lakini kama utakavyoona tunaanza leo tarehe 6 Mei, kwa hiyo, ni mwezi mzima umepita. Kwa maana hiyo, ni kwamba kazi rasmi za kujadili hotuba moja, moja za sekta mbalimbali ukiacha bajeti hotuba yenyewe, siku za kazi ni 26 tu. Kwa hiyo, kwa busara mliyoifanya leo tumekubaliana kubadilisha muda wa kuanza, tunaanza saa tatu na kubadilisha muda wa kumaliza.

Pia tumekubaliana kubadilisha muda wa kuongea na tumekubaliana pia kuongeza siku ya Jumamosi ifanyike kazi. Kwa hiyo, ili tufanikishe yale tuliyozungumza kwenye kikao cha briefing ni lazima tutengue kanuni na kwa hiyo, namwona Mheshimiwa Waziri wa Nchi, afanye kazi hiyo.

### HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo ya kutengua kanuni za Bunge chini ya Kanuni ya 153(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013.

KWA KUWA Mkutano wa 15 wa Bunge wa kushughulikia bajeti ya mwaka 2013/2014, pamoja na shughuli nyingine za Bunge zilizopangwa, umepangwa umalizike tarehe 27 Juni, 2014;

NA KWA KUWA ratiba ya shughuli zilizopangwa kufanyika katika Mkutano huu zimepangwa kwa kuzingatia kalenda ya Mikutano ya Bunge na Kanuni za Bunge, Toleo la 2013. Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni ya 108, Bunge liwe limeshakamilisha kazi ya kujadili na kupitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka unaohusika kabla ya tarehe 30 Juni, kila mwaka.

NA KWA KUWA kutohana na kuwa na Bunge Maalum la Katiba mwezi Aprili, Bunge la Bajeti limelazimika kuanza mwezi Mei, hivyo kuwa na muda mfupi wa kushughulikia bajeti. Jambo linalolazimu Bunge kuhitaji muda mwingi wa kufanya kazi.

NA KWA KUWA katika kikao cha Kamati ya Uongozi wa Bunge kilichofanyika tarehe 4, siku ya Jumapili, Wajumbe wote wa Kamati hiyo waliohudhuria waliazimia kuliomba Bunge likubali kufanya kazi kwa muda zaidi ya uliowekwa kikanuni ili kuhusisha siku zote za Jumamosi pamoja na kupunguza muda wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya Wizara mbalimbali na Bajeti ya Serikali kwa lengo la kupata muda mrefu wa kushughulikia bajeti na wachangiaji wengi zaidi.

NA KWA KUWA ili kuwezesha Bunge kufanya kazi kwa muda zaidi ya uliowekwa kikanuni, kufanya kazi siku za Jumamosi na kupunguza muda wa uchangiaji, ni lazima kutengua kanuni ya 28(2) ya nne (4) na 15, kanuni ya 99(12) na kanuni ya 106(1) kwa mujibu wa kanuni ya 153(1).

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa 15; kanuni ya 28(2), ya nne (4) na ya 15 na kanuni ya 99(12) na kanuni 106(1) zitenguliwe kama ifuatavyo:-

(i) Kanuni ya 28(2) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba, Bunge litakutana hadi saa saba mchana ambapo Spika atasitisha shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika hadi saa 11 jioni, itenguliwe na badala yake Bunge likutane hadi saa saba mchana na Spika asitishe Bunge hadi saa kumi jioni.

(ii) Kanuni ya 28(4) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba, Bunge litaendelea kukaa mpaka saa 1.45 litenguliwe na badala yake Bunge likae mpaka saa mbili kamili usiku.

(iii) Kanuni ya 28(15) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Bunge halitakutana siku ya Jumamosi, Jumapili na siku za mapumziko itenguliwe na badala yake Bunge likutane siku za Jumamosi kuanzia saa tatu mpaka saa saba mchana na baadaye saa kumi mpaka saa mbili usiku, isipokuwa kwamba hiyo haitakuwa na kipindi cha maswali.

(iv) Kanuni ya 96(12) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba, Mbunge anayejadili makadirio ya matumizi ya Wizara mbalimbali ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika kumi itenguliwe na badala yake utumike muda usiozidi dakika saba na kanuni ya 106(1) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba, Mbunge anayetaka kujadili hoja ya bajeti ya Serikali ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika kumi itenguliwe na badala yake utumike muda usiozidi dakika saba.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**SPIKA:** Nadhani walioafiki wameshinda, kwa hiyo kuanzia sasa tutakuwa tunaanza kazi saa tatu asubuhi mpaka saa saba; saa kumi mpaka saa mbili ya usiku na tutafanya kazi pia siku ya Jumamosi. Pia tutatumia dakika saba; tutapiga kengele ya kwanza baada ya dakika tano, ya pili baada ya dakika mbili zinazofuata.

Halafu Waheshimiwa Wabunge pia nadhani mmeshapewa maelekezo, naomba mkachukue fomu za kujaza Wizara mnazotaka kuchangia katika kipindi hiki. Wizara unayopenda kuchangia kwanza inakuwa namba moja, ya pili mpaka ya sita. Kwa hiyo, hiyo itatusaidia sisi tunapopanga ratiba ya wachangiaji, tunajua nani waliongea katika Wizara gani na nani waanze kuchangia.

Nadhani hizo fomu mmepewa, kama hamjapewa naomba mchukue kwa sababu msipojaza zile fomu hakuna mahali hapa mezani utatuletea kikaratasi. Kwa hiyo, naomba mfanye hiyo kazi nadhani leo mfanye hivyo kwa sababu tutaanza kujadili ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara zinazofuatana. Kwa hiyo, nadhani uzoefu wa mwaka jana, leo mtafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu mtoa hoja! (Makofi)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa katika Bunge lako Tukufu na Wenyeviti wa Kamati za Bunge, Sheria na Utawala,

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kamati za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara na Kamati ya Masuala ya UKIMWI zilizochambua bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2013/2014 na mwelekeo kwa mwaka 2014/2015. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu; Ofisi ya Waziri, Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali, Taasisi zilizo chini yake pamoja na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote na kwa masikitiko makubwa naomba nichukue fursa hii kutoa salamu za pole kwako na Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na Wabunge wawili Mheshimiwa William Augustao Mgimwa, aliyekuwa Mbunge wa Kalenga, aliyefariki tarehe 1 Januari, 2014 na Mheshimiwa Said Ramadhan Bwanamdogo aliyekuwa Mbunge wa Chalinze ambaye alifariki tarehe 22 Januari, 2014.

Mheshimiwa Spika, aidha, niwape pole wananchi wa Mkoa wa Mara kwa kifo cha Mheshimiwa John Gabriel Tupa, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa huo kilichotokea tarehe 25 Machi, 2014 na kwa wananchi wa Wilaya ya Urambo kwa wananchi wa Wilaya ya Urambo kwa kifo cha Mheshimiwa Anna Magoha, aliyekuwa Mkuu wa Wilaya hiyo kilichotokea tarehe 24 Septemba, 2013.

Vile vile natoa pole kwa wananchi wa Wilaya ya Ukarambo, kwa kifo cha Mheshimiwa Moshi Mussa Chang'a aliyekuwa Mkuu wa Wilaya hiyo aliyefariki tarehe 21 Aprili, 2014. Naomba pia niwape pole Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote waliofiwa na ndugu na jamaa zao kutokana na majanga na matukio mbalimbali tangu nilipowasilishwa bajeti yangu ya mwaka 2013/2014. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu wote mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kuwapa pole wahanga wote wa majanga mbalimbali yakiwemo mafuriko na ajali za barabarani na niwashukuru kwa dhati wote waliotoa misaada ya hali na mali wakati wa ajali na maafa hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2013/2014, Bunge lako Tukufu limepata Wabunge wapya watatu ambaa ni Mheshimiwa Yusuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani; Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete Mbunge wa Chalinze. Nawapongeza kwa kuchaguliwa kuwasilisha wananchi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nawaomba watumie fursa waliyoipata kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wa pili tangu tuanze utaratibu wa mzunguko mpya wa bajeti ambaa unatuwezesha kukamilisha mjadala wa bajeti ya Serikali ifikapo tarehe 30 Juni. Taarifa za awali zinabaini kwamba utaratibu umeanza kuonesha mafanikio ya haraka katika utekelezaji wa kazi zilizopangwa.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii imeendelea kutayarishwa kwa kuzingatia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010; awamu ya pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania, MKUKUTA II; Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Mwaka 2011 hadi 2015/2016; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015 na Mfumo wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa (Big Results Now - BRN).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya kipaumbele iliyoainishwa kwenye Mipango hiyo ya Kitifa ili kuleta maendeleo endelevu na ya haraka yatakayowanufaisha wananchi wa Tanzania.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge lako Tukufu, kwa mchango wao mkubwa wakati wa uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali Zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kazi waliyofanya kubwa na ambayo imetuwezesha kukamilisha maandalizi ya bajeti ninayoiwasilisha leo. Maoni na ushauri wao utazingatiwa wakati wa kukamilisha mjadala wa Bajeti ya Serikali na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya siasa nchini ni tulivu na Vyama vya Siasa vinaendelea kutekeleza majukumu yao. Nchi yetu inapitia kwenye kipindi cha mpito ambapo tunaandika Katiba mpya itakayoweka mustakabali wa mwelekeo wa Taifa letu kwa miaka mingi ijayo. Nawashiwanasi na wananchi wote kwa ujumla, kutoa ushirikiano mkubwa wakati wa maandalizi ya Katiba hiyo ambayo baadaye wananchi wote wataipigia kura ya maoni. Nawaomba tushindane kwa nguvu ya hoja na si hoja ya nguvu katika kuandaa Katiba hii ambayo itatuongoza sasa na vizazi vijavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kukuza na kuimarishe demokrasia ya Vyama Vingi nchini, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imeratibu shughuli ya Vyama vya Siasa kwa kuhakikisha kunakuwepo na fursa sawa katika shughuli za siasa nchini. Hadi Aprili, 2014 idadi ya Vyama vya Siasa vyenye usajili wa kudumu imefikia 21 baada ya Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMA), kupata usajili wa kudumu mwezi Juni, 2013.

Mheshimiwa Spika, aidha, Chama cha Alliance for Change and Transparency Tanzania, Chama cha Wananchi na Demokrasia (CHAWADE) na Chama cha Maridhiano Uwiano (CMU) vimepata usajili wa muda, ingawa leo nimeona kwenye gazeti Chama kimoja kati ya hivi nadhani ACT naona walikuwa wanakabidhiwa hati. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nirejee wito wangu kwa viongozi na wanachama wa Vyama vyote vya Siasa, kuendeleza utamaduni wa kuvumiliana na kutohamasisha siasa za chuki na vurugu ambazo zinaweza kutugawa na kuhatarisha amani, utulivu na umoja wa Taifa letu tulilolijenga kwa miaka mingi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, usalama wa raia, nchi yetu imeendelea kudumisha amani na utulivu kama tunu ya Taifa iliyojengwa na kuimarishe tangu tulipopata uhuru. Katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Polisi limeendelea kutekeleza program ya maboresho ya Jeshi na mkakati wa kupunguza uhalifu ambavyo vimeongeza ushirikiano wa wananchi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi hilo limeongeza vikundi 1,778 vya ulinzi shirikisho na kufikia vikundi 6,798 kwa mwaka 2013 kwa nchi nzima. Vikundi hivyo vimechangia kupunguza vitendo vya uhalifu nchini kutoka asilimia 4.3 mwaka 2012 hadi asilimia 2.8 mwaka 2013 na hivyo kuchangia kupungua kwa makosa makubwa na madogo ya jinai kutoka makosa 566,702 mwaka 2002 hadi makosa 560,461 mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, mauaji ya wanawake, pamoja na juhudzi zinazofanywa na Serikali na kushirikiana na wananchi katika kuimarishe ulinzi na usalama wa raia, hivi karibuni kumetokea wimbi la mauaji ya kikatili dhidi ya wanawake. Katika kipindi cha Januari, hadi Aprili, 2014, wanawake wanane wameuawa kikatili katika Kata za Mugango, Etaro, Nyakatende na Nyegina Wilayani Butiama.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi uliofanyika umebaini kwamba mauaji hayo yamefanyika mchana na kwa mtindo unaofanana wa kunyonga na khanga au kamba na mili yao kufikiwa

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwenye mashimo mafupi au kufichwa vichakani. Mara zote walengwa ni wanawake wanapokuwa kwenye shughuli zao za kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inalaani vitendo hivyo visivyokubalika katika jamii na itawachukulia hatua kali za kisheria wale wote watakaobainika kuhusika kwa namna yoyote. Serikali imechukua hatua kadhaa za kudhibiti vitendo hivyo vya mauaji, ikiwa ni pamoja na kuwakamata watuhumiwa 26 na kati yao 13 wamefikishwa Mahakamani.

Vile vile Jeshi la Polisi limeunda kikosi kikazi kwa ajili ya kudhibiti hali hiyo na kufanya mikutano ya kuhamasisha jamii kuhusu kuanzisha na kuimarisha vikundi vya Polisi Jamii. Nitoe wito kwa wananchi wema wenyewe upendo na nchi yetu kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu kwenye vyombo vya usalama ili sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, ajali za barabarani zimeendelea kuwa tishio kwa maisha ya watu na mali zao, takwimu za Jeshi la Polisi zinaonesha kuwa, katika mwaka 2013 zilitokea ajali za barabara 24,480 zilizosababisha vifo 4,091 na majeruhi 21,536 ikilinganishwa na ajali 23,604 zilizosababisha vifo vya watu 4,062 na majeruhi 20,037 mwaka 2012. Kwa upande wa pikipiki pekee mwaka 2012 zilitokea jumla ya ajali ya 5,763 na kusababisha vifo 930 na majeruhi 5,532.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013 zilitokea ajali 6,831 na kusababisha vifo 1,098 na majeruhi 6,578. Aidha, katika kipindi cha Januari, hadi Machi, 2014 zimetokea ajili 1,449 na kusababisha vifo 218 na majeruhi 1,304. Ajali hizi nydingi na zinasababisha vifo vingi na majeruhi ambaeo wengi wao ni nguvukazi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, ni vyema ikumbukwe kwamba Serikali iliruhusu matumizi ya pikipiki kwa nia njema ya kupunguza matatizo hususan maeneo ya vijijini. Hata hivyo, fursa hiyo imeambatana na changamoto ya ajali nydingi barabarani. Hivyo ni wajibu wa madereva wote kuzingatia sheria za barabani na kukidhi vigezo vyote vya kuwa na vibali halali za kufanya biashara hizo pamoja na leseni za udereva.

Mheshimiwa Spika, SUMATRA, Jeshi la Polisi, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mamlaka nyininge zinazohusika, zinatakiwa kukaa pamoja ili kuweka mkakati wa kukabiliana na ajali hizo ikiwa na pamoja na kuhakikisha kwamba, Kanuni za Leseni za Usafirishaji wa Pikipiki na Bajaji za Mwaka 2010 zinatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, hali ya mipaka ya nchi; Serikali imeendelea kuliwezesha Jeshi la Wananchi wa Tanzania kutimiza majukumu yake ya kulinda mipaka ya nchi yetu na raia wake. Katika mwaka 2013/2014, Serikali imewezesha wanajeshi wetu kupata mafunzo mbalimbali katika vyuo vya ndani na nje ya nchi, pamoja na kushiriki katika mazoezi ya ushirikiano kikanda. Aidha, jeshi limeshiriki katika operesheni mbalimbali za kulinda amani zinaongozwa na umoja wa Mataifa huko Darfur (Sudan); Lebanon, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo na Sudan Kusini.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, Jeshi limefanya kazi kubwa, nzuri na kwa weledi mkubwa, nidhamu na kujituma, hivyo kuendelea kuipatia heshima kubwa nchi yetu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuwapatia za Askari mazingira mazuri ya kuishi, Serikali imeanza kutekeleza awamu ya kwanza ya mradi wa ujenzi wa nyumba za askari ambapo ujenzi wa majengo 191 kati 664 unaendelea katika vikosi mbalimbali vya Jeshi nchini.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa; mwaka 2013/2014 ni wa tatu tangu Serikali iliporejesha utaratibu wa kuwachukua vijana wanaohitimu Kidato cha Sita kujunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa mujibu wa sheria. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2013, Jumla ya vijana 15,167 wamehitimu mafunzo ya JKT wakiwemo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu. Mafunzo hayo yamewapatia vijana hao fursa ya kujifunza juu ya ulinzi, usalama na ukakamavu, uzalishaji mali, uzalendo na umoja wa Kitaifa. Katika mwaka 2014/2015 Serikali itachukua vijana zaidi kujunga na JKT kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, katika 2013/2014 Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilisimamia na kuendesha chaguzi ndogo za Wabunge katika Majimbo matatu na Udiwani katika Kata 53 nchini. Chaguzi hizo zimefanyika kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo vifo na baadhi ya Waheshimiwa Madiwani kukosa sifa za kuendelea na nyadhifa hizo. Katika uchanguzi wa Ubunge uliofanyika katika Jimbo la Chambani Zanzibar CUF ilishinda kwa kupata asilimia 84% ya kura zote. CCM ilipata kura asilimia 12.4%, ADC ilipata kura asilimia 3.5% na CHADEMA ilipata asilimia 0.4% ya kura zote. (Makof)

Katika Jimbo la Kalenga Iringa, CCM ilishinda kwa kupata asilimia 79.3% ya kura, CHADEMA ilipata kura 20.2% na CHAUSTA ilipata asilimia 0.5%.

Katika Jimbo la Chalinze, Pwani, CCM ilishinda kwa kupata asilimia 86.61%, CHADEMA ilipata kura asilimia 10.58%, CUF ilipata kura asilimia 1.98%, AFP ilipata kura asilimia 0.59%, na NRA ilipata asilimia 0.25% ya kura zote. Aidha, katika chaguzi za Madiwani zilizofanyika katika Kata 53 CCM ilishinda viti 40, CHADEMA viti 12 na NCCR-Mageuzi kiti kimoja. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaendelea na maandalizi ya kupata vifaa vya kisasa kwa ajili ya zoezi la kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Katika awamu hii ya uboreshaji wa Daftari, mfumo wa *biometric voter registration* utatumika tofauti na mfumo wa awali wa *Optical Mark Recognition* ambao ulikabiliwa na changamoto nyingi za utendaji. Mfumo huu wa kisasa unawezesha uandikishaji na uchukuaji alama za vidole kwa haraka zaidi na hatimaye mwananchi kupatiwa kitambulisho cha kupiga kura kwa muda mfupi. Hii itasaidia sana kuokoa muda na kupata takwimu sahihi za wapiga kura watakaoshiriki kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuwaomba Viongozi wa Vyama vya Siasa kuhamasisha wanachama na Watanzania wote wenye sifa kujandikisha kwenye Daftari hilo na kupata kitambulisho halali cha mpiga kura pale zoezi hilo litakapoanza rasmi. Aidha, natoa wito kwa wananchi wote wenye sifa kujitokeza kujandikisha. Ni imani kwamba tukitumia fursa hii kikamilifu, tutaondoa malalamiko ya majina ya baadhi ya wapiga kura kutokuwepo kwenye orodha wakati wa chaguzi. Ni muhumi tukumbuke kwamba, ni wananchi wenye sifa tu ndio watakaoandikishwa.

Katika mwaka 2014/2015, Tume itakamilisha zoezi la kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kusimamia kura ya maoni kwa ajili ya Katiba mpya na kuendelea kutoa elimu ya mpiga kura kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi Julai, 2013 hadi Aprili, 2014, Ofisi ya Bunge imeendesha Mikutano mitatu ya Bunge na Mikutano mitatu ya Kamati za Bunge. Maswali ya msingi 410 pamoja na maswali 73 ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa. Aidha, Miswaada minane ya Sheria ilipitishwa na Bunge.

Pia Bunge limekamilisha ukarabati wa Ukumbi wa Bunge na miundombinu yake kuwezesha Mikutano wa Bunge la Katiba kufanyika na Ujenzi wa Ofisi za Wabunge umeendelea kufanyika. Vile vile Ofisi ya Bunge imewajengea uwezo Wabunge na Watumishi wake kupitia

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

semina mbalimbali katika masuala ya Utawala Bora katika mwaka 2014/2015. Ofisi ya Bunge itaendelea kuratibu Mkutano ya Bunge, Vikao vya Kamati za Bunge za Kudumu pamoja na kuimarisha miundombinu na majengo ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, tarehe 26 Aprili, 2014 tumeazimisha miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Miaka 50 kwa lugha yoyote ile siyo kipindi kifupi. Tumeweza kufika hapa tulipo kutohama na misingi imara ya Muungano iliyowekwa na waasisi wetu na kuendelezwa na Viongozi waliongoza Taifa letu katika awamu zilizofuatia. Tunajivunia kwamba Muungano wa Tanzania umejengeka kwenye historia ya muda mrefu ya ushirikiano wa watu wa pande hizi mbili. Jamii hizi zina uhusiano wa damu, kifikra na mapambano ya pamoja dhidi ya Wakoloni waliotawala kwa vipindi tofauti.

Walichofanya Waasisi wetu mwaka 1964 ni kurasimisha ushirikiano wetu kwa muda mrefu. Nichukue fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Watanzania wote kwa kuadhimisha miaka 50 ya Muungano. Aidha, nawashukuru kwa dhati viongozi wote walioongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar tangu kuasiwi kwa Muungano.

Kwa namna ya kipekee, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wao ambao umezifanya pande mbili za Muungano kuwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Spika, tumeadhimisha miaka 50 ya Muungano tukiwa na takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012. Takwimu hizo zinaweka jambo moja wazi kwa Muungano wetu, kwamba zaidi ya asilimia 90 ya Watanzania wote wamezaliwa baada ya Muungano. Hivyo, tuliozaliwa kabla ya Muungano ni chini ya asilimia 10. Kwa mujibu wa Takwimu hizo, Tanzania nzima ina watu 44,926,923. Kati yao, watu 40,640,425 sawa na asilimia 90.6 ni wa umri wa siku moja hadi miaka 50.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania Bara idadi ya watu ilikuwa 43,625,354. Kati ya hao, watu 39,456,065 sawa na asilimia 90.5 wamezaliwa baada ya Muungano. Kwa upande wa Zanzibar kulikuwa na watu 1,303,569 ambapo watu milioni 1,184,360 sawa na asilimia 90.9 wamezaliwa baada ya Muungano. Takwimu hizo zina maana kwamba asilimia 90.6 ya watu wote wamezaliwa ndani ya Muungano na nchi wanayoifahamu ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sote tunawajibika kuwatendea haki watu hawa kwa kuulinda, kuimarisha na kuudumisha Muungano wetu. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, tuna kila sababu ya kuadhimisha miaka 50 ya Muungano kwa furaha. Katika maadhisho ya mwaka huu tulianaa maonyesho maalum, mkongamano na shughuli nyingine ambazo zilisaidia wananchi kuelimishwa kuhusu masuala ya Muungano. Aidha, kimeandalishi kitabu Maalum kinachoelezea historia, utekelezaji wa mambo ya Muungano, mafanikio, changamoto, fursa na matarajio ya Muungano kwa miaka ijayo. Kitabu hicho kitatumika kama rejea kwa kizazi chetu na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuulinda Muungano wetu kwa nguvu zote tukiwa na uelewa kwamba katika kipindi cha miaka 50 iliyopita Watanzania wameishi kwa amani na kufanya kazi zao za kujiletea maendeleo wakiwa upande wowote wa Muungano. Tunatambua changamoto zilizopo na tumeweza utaratibu mzuri wa vikao ili kuzitafutia ufaumbuzi changamoto hizo. Vikao hivyo vitaendelea kufanyika katika ngazi ya wataalam, Watendaji Wakuu na Viongozi wa Kitaifa.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Ni imani yangu kwamba Muungano huu utaendelea kudumu na watu watapata maendeleo makubwa kwani Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina fursa nyigi zinazoweza kutumika kwa manufaa ya wote. Sote tukumbuke kuwa Utanzania wetu ni Muungano wetu; hivyo, tuulinde tuimarishe na kuudumisha. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Desemba, 2013, Tume ya Mabadiliko ya Katiba ilikamilisha Rasimu ya Pili ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuikabidhi kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dokta Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Napenda kuishukuru Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliyokuwa ikiongozwa na Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba kwa kuandaa Rasimu ya Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Rasimu hiyo imeliwezesha Bunge Maalum la Katiba kuanza Mjadala. Nitumie fursa hii kuwashukuru Watanzania wote kwa kutoa maoni yaliyowezesha Tume kuandaa Rasimu hiyo ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, Bunge Maalum la Katiba linaundwa na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge wa Baraza la Wawakilishi na Wajumbe 201 walioteuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, 2011. Naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Wajumbe wote wa Bunge Maalum la Katiba kwa kupata fursa hii ya kuwakilisha Watanzania katika kuandaa Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni dhahiri kuwa dhamana hii ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Bunge Maalum la Katiba lilianza kazi rasmi tarehe 18 Februari, 2014 kwa kumchangua Mwenyekiti, Mheshimiwa Pandu Ameir Kificho kuwa Mwenyekiti wa muda wa Bunge hilo. Nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Pandu Ameir Kificho kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kulisimamia Bunge Maalum hadi kuwezesha kupatikana kwa Kanuni za kuliendesha Bunge hilo. (Makofij)

Aidha, niwapongeze Mheshimiwa Samweli John Sitta kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba. Nampongeza Katibu wa Bunge la Katiba, Bwana Yahaya Hamad Khamis na Naibu wake Dkt. Thomas Kashilillah pamoja na Wajumbe wote waliochaguliwa kuwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati 12 za Bunge Maalum.

Baada ya kukutana kwa muda wa siku 67, Bunge Maalum limeahirisha Mkutano wake tarehe 25 Aprili, 2014 ili kupisha majadiliano ya mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2014/2015. Ni matumaini yangu kwamba Bunge Maalum la Katiba litakaporejea, litakamilisha kazi hiyo kwa umakini na kupata Rasimu ambayo hatimaye itapelekwa kwa wananchi kwa ajili ya kura za maoni.

Mheshimiwa Spika, vitambulisho vya Taifa; katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2013/2014 nilielezea dhamira ya Serikali ya kutoa Vitambulisho vya Taifa kwa wananchi wake. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imekamilisha usajili na utambuzi wa watu Upande wa Zanzibar, Watumishi wa Umma na Vyombo vya Ulinzi na Usalama pamoja na wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam. Serikali pia imekamilisha Ujenzi wa Vituo vya kuingiza na kuhakiki taarifa. Kituo cha kutengeneza vitambulisho na kuhifadhi kumbukumbu pamoja na kituo cha uokozi na majanga ya taarifa na takwimu.

Katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea na zoezi la utambuzi na usajili wa Watanzania katika Mikoa mingine ili kwa pamoja tuweze kunufaika na vitambulisho vya Taifa katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kiusalama.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, sensa ya watu na makazi; katika mwaka 2013/2014, Serikali imeendelea kutoa machapisho mbalimbali ya matokeo ya Sensa ya watu na Makazi ya mwaka ya mwaka 2012. Machapisho hayo yanajuimusha taarifa ya mgawanyo wa watu na maeneo ya utawala. Mgawanyo wa watu na kwa umri na jinsia na taarifa za msingi za kidemografija, kijamii na kiuchumi.

Taarifa hizo zimebaini kuwa katika miaka 10 iliyopita kumetokea mabadiliko makubwa ya kuichumi na kijamii katika nchi nchi yetu. Kiwango cha watu wanaojua kusoma na kuandika kimeongozeka kutoka asilimia 69 mwaka 2002 hadi asilimia 78 mwaka 2012. Aidha, uandikishaji halisi katika Shule za Msingi umeongezeka kutoka asilimia 69 mwaka 2002 hadi asilimia 77 mwaka 2012. Idadi ya watu wanaoishi kwenye nyumba zenye kuta imara ni asilimia 74 na asilimia 65.4 wanaishi kwenye nyumba zilizozekwa bati.

Hata hivyo, pamoja mafanikio hayo, hali ya utegemezi nchini ni kubwa kutohana na ukweli kuwa kati ya Watanzaia milioni 44.9 asilimia 50.1 ni watoto wenye umri chini ya miaka 18. Aidha, takwimu zimebainisha kuwa asilimia 7.7% ya Watanzania ni watoto yatima. Kutohana na hali hiyo, ni jukumu letu kama Taifa kuweka mipango madhubuti ya kukabialiana na changamoto katika Sekta za Huduma ya Jamii ili hatimaye kila mwenye uwezo wa kufanya kazi achangie ipasavyo katika kukuza uchumi na maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pato la Taifa mwaka 2013 lilikua kwa asilimia 7.0 likilinganishwa na ukuwji wa asilimia 6.9 mwaka 2012. Ongezeko hilo limetokana na ukuaji mzuri wa shughuli za huduma za mawasiliano, viwanda ujenzi na huduma za fedha. Kutohana na ongozeko hilo, wastani wa pato la Mtanzania limeongezeka kutoka Sh. 1,250,038/= mwaka 2012 hadi Sh. 1,186,424 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 15.7.

Mfuko wa bei umepungua kutoka asilimia 9.8 mwaka 2013 hadi asilimia 6.1 Machi, 2014. Kupungua kwa mfumko wa bei kumechangiwa na kupungua kwa kasi ya kupanda bei za bidhaa na vyakula hasa mahindi, mchele na aina nyingine ya nafaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uchumi wetu kukua kwa kasi ya asilimia saba kwa mwaka 2013 na pato la Mtanzania kuongozeka, kiwango hicho siyo kikubwa sana kuwezesha umaskini wa wananchi kupungua kwa kasi. Utafiti wa kitaalam unaonyesha kwamba ili umasikini upungue kwa kasi kubwa, uchumi unatakiwa kukua kwa zaidi ya asilimia nane kwa kipindi cha miaka kumi mfululizo. Ukuaji huo pia unatakiwa kulenga sekta ambazo zinagusa maisha ya watu wengi, hususan kilimo, mifugo na uvuvi. Mwelekeo wa Serikali ni kuweka mazingira wezeshi kwa sekta za kipaumbele kukua kwa kushirikisha sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mpango wa maendeleo wa miaka mitano, 2011/2012 hadi 2015/2016 ambao unatekelezwa katika kipindi cha mwaka mmoja mmoja. Katika mwaka 2013/2014, Serikali ilitekeleza mpango huo kupitia kaulimbiu ya Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa.

Mheshimiwa Spika, msingi wa kauli hii ni kuainisha maeneo machache ya kimkakati na ya kutengea rasilimali za kutosha kusimamia na kufuatilia utekelezaji kwa karibu zaidi. Chombo maalum cha ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya kimkakati chini ya Ofisi ya Rais kinachojulikana kama *Presidency Delivery Bureau* au PDB kimeanzishwa na Watendaji Wakuu wameteuliwa.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba matunda ya utekelezaji wa mfumo huo yameanza kuonekana katika maeneo makuu sita ya kipaumbele Kitaifa ambayo ni nishati ya

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

umeme, uchukuzi, kilimo, elimu, maji na ukusanyaji wa mapato. Utekelezaj wa miradi hiyo na mafanikio yaliyoanza kupatikana yatatolewa maelezo na Mawaziri katika sekta husika.

Mheshimiwa Spika, njia ya uhakika ya kuliwezesha Taifa kuwa na uchumi imara na wa kisasa utakaohimili ushindani katika masoko ya kikanda na Kimataifa ni kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji. Katika kufikia azma hiyo, tarehe 31 Januari, 2014 nilizindua rasmi Taarifa ya Tathmini ya Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali zinazosimamia uwekezaji Tanzania. Mapendekezo ya taarifa hiyo yatatumika kuihuisha Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 1996 pamoja na Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, aidha, ili kuwawezesha wawekezaji na wafanyabiashara kupata huduma na taarifa zote muhumi kama vile sheria, kanuni na taratibu mbalimbali, kuhusu biashara na uwekezaji kwa njia ya mtandao, Serikali imezindua upya tovuti ya kituo cha uwekezaji Tanzania. Kupitia tovuti hii, wawekezaji popote duniani wanaweza kupata taarifa kuhusu usajili wa Kampuni na viwango vya kodi kwa njia ya mtandao.

Dhamira ya Serikali ni kuboresha mazingira ya uwekezaji na kupunguza ghamra za kufanya biashara nchini ili kukabiliana na ushindani mkubwa kutoka nchi nyingine zilizotekeliza maboresho ya mifumo yao ya udhibiti wa biashara.

Mheshimiwa Spika, sekta binafsi inaendelea kuperwa nafasi kubwa katika kukuza uchumi nchini. Takwimu zinaonyesha kwamba miradi iliyosajiliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania, imeongezeka kutoka 869 yenye thamani ya Shilingi bilioni 31.5 mwaka 2012 hadi miradi 885 yenye thamani ya Shilingi bilioni 141.2 mwaka 2013.

Napenda pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba nchi nyingi duniani zinaendelea kuiamini Tanzania kama kituo maarufu cha uwekezaji duniani. Mwezi Desemba, 2011 nilizindua mpango wa ushirikiano kati ya Tanzania na Uingereza unaojulikana kama *partnership in prosperity*. Mpango huo umelenga kuongeza uwekezaji kutoka sekta binafsi ya Uingereza kwenye mafuta na gesi, kilimo na nishati jadidifu. Lengo ni kuongeza uwekezaji kutoka nchi hiyo kwa zaidi ya maradufu ya kiwango cha sasa. Aidha, tumekubaliana kushirikiana kuimarisha mazingira ya biashara ili kurahisisha uwekezaji katika sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Kampuni za Uingereza tayari zimeanza kutekeleza makubaliano hayo kwenye Sekta ya Kilimo. Kampuni ya Uniliver kwa mfano, itawekeza zaidi ya Shilingi bilioni 275 kwenye Kilimo cha Chai kwa kushirikiana na wakulima wadogo. Tayari Kampuni hiyo imeanza kupanua Kiwanda cha Chai, Kibwele Mufindi na kufungua zaidi ya hektaki ya 300 za mashamba ya chai katika Wilaya ya Mufindi.

Mheshimiwa Spika, aidha, kampuni hiyo imeingiza nchini vipando lakini 250,000 vya miche bora ya chai. Pia kampuni inaanadaa zaidi ya miche milioni mbili kwa ajili ya kuwagawia wakulima wadogo Wilayani Njombe ili waongeze uzaliashaji wa chai nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 kituo cha uwekezaji kimeshirikiana na Uongozi wa Mikoa mbalimbali nchini kuratibu maandalizi ya makongamo ya uwekezaji yenye lengo la kuhamasisha, kukuza na kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo kwenye Mikoa hiyo.

Jumla ya Mikoa 11 imeshiriki kikamilifu kuandaa na kufanikisha makongamano ya uwekezaji katika maeneo yao. Mikoa hiyo ni Mwanza, Mara, Geita, Kagera, Simiyu, Shinyanga,

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Tabora, Manyara, Tanga, Kilimanjaro na Arusha. Makongamano hayo yamechangia kwa kiasi kikubwa kuzitangaza fursa za uwekezaji zilizopo kwenye Mikoa hiyo pamoja na kuzihamasisha Mikoa na Halmashauri za Wilaya ndani ya Mikoa hiyo kuiainisha na kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji. Aidha, wawekezaji wengi walioshiriki kwenye Makongamano hayo wameonyesha nia na utayari wa kuwekeza katika Mikoa husika. Jitahada hizi zitaendelezwa katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, majadiliano na sekta binafsi; kwenye hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2013/2014, nilieleza kuhusu mukutano wa kimataifa wa majadiliano ya ushirikiano kwa manufaa ya wote. Mukutano huu ulifanyika kuanzia tarehe 28 Juni hadi tarehe moja Julai, 2013 Jijini Dar es Salaam, chini ya Uwenyekiti wa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mukutano huo ulitoa fursa kwa ya kipekee kwa viongozi wa Serikali kujadiliana na kupata maoni ya makundi mbalimbali za wananchi kuhusu mbinu za kuongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Serikali imedhamiria kufanya majadiliano ya ushirikiano kwa manufaa ya wote kila mwaka kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa hadi Taifa kwa kuzingatia fursa kubwa za maendeleo shirkishi zilizopo kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Biashara lilifanya Mukutano wake wa Saba tarehe 16 Desemba 2013 chini ya Kauli Mbiu ya "Ukuaji Shirikishi wa Uchumi". Maazimio ya Mukutano huo ni pamoja na kuunda Kamati tatu ambazo zitashughulikia uwezeshaji wananchi kiuchumi, mazingira wezeshi ya biashara na matumizi endelevu ya maliasili za nchi. Kamati ya Mazingira Wezeshi ya Biashara imeanza kuishauri Serikali kuhusu mikakati ya kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje na kuongeza ushindani wa bidhaa za Tanzania. Kazi hiyo imefanyika kwa utaratibu wa Maabara chini ya Mfumo wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa.

Utaratibu huo ulianzisha maeneo sita muhimu ambayo yakishughulikiwa yataboresha mazingira ya biashara nchini. Maeneo hayo ni kuboresha Kanuni na Taasisi zinazosimamia biashara, upatikanaji wa ardhi na haki za umiliki wake na kuimarisha ukusanyaji wa kodi na kupunguza wingi wa kodi na tozo mbalimbali. Maeneo mengine ni kuzuia na kupambana na rushwa, kuboresha Sheria za Kazi na kuimarisha mafunzo na stadi za kazi pamoja na kusimamia utekelezaji wa mikataba na utawala wa sheria. Katika mwaka 2014/2015, Baraza la Taifa la Biashara litaendelea kuratibu utekelezaji wa maazimio hayo ya Mukutano wa Saba sanjari na kusimamia Mikutano ya Mabaraza ya Wilaya na Mikoa.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ya kubuni na kutekeleza Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 ni kuhakikisha kwamba Watanzania wananaufaika na rasilimali za nchi yao badala ya kubaki kuwa watazamaji tu. Kwa kutambua umuhimu wa uwezeshaji wananchi kiuchumi, katika Mwaka 2013/2014 Serikali imeanzisha Taasisi ya Ujasiriamali na Ushindani wa Kibashara yaani *The Tanzania Entrepreneurship Competitiveness Centre*. Taasisi hiyo itatekeleza jukumu la kutoa miongozo ya uandaaji wa mitaala ya ujasiriamali katika ngazi tofauti na kuhamasisha uzalishaji wa bidhaa bora zitakazohimili ushindani.

Aidha, Serikali imeendelea kusimamia Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kuongeza ufanisi wake. Hadi kufikia mwezi Februari, 2013, Mfuko wa Uwezeshaji wa Wananchi ulikuwa umepokea Shilingi bilioni 2.1 zilizotumika kudhamini mikopo ya wajasiriamali kupilia Benki ya CRDB kwa makubaliano ya kukopesha mara tatu ya dhamana ya Serikali. Kutokana na makubaliano hayo, hadi kufikia mwezi Desemba, 2013, mikopo yenye thamani ya zaidi ya Shillingi bilioni 9.5 ilikuwa imetolewa kwa Wajasiriamali 9,790 waliojunga kwenye vikundi 283 na Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) 51 katika Mikoa 12 na Wilaya 27.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mfuko wa Kuendeleza Wajasiriamali Wadogo na wa Kati, hadi kufikia Desemba, 2013, ulikuwa umetoa mikopo yenyе thamani ya Shilingi bilioni 36.39 kwa wajasiriamali 62,720.

Aidha, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ulikuwa umetoa mikopo kwa Vijana yenyе thamani ya Shilingi bilioni 1.22 kupitia SACCOS 244; na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ulikuwa umetoa mikopo yenyе thamani ya Shilingi bilioni 5.44 kwa Wanawake 500,000 nchini. Vilevile, Mradi wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (*SELF*) ulikuwa umetoa mikopo yenyе thamani ya Shilingi bilioni 57.1 kupitia Asasi 375 za kifedha ambapo Wajasiriamali 95,034 walinufaika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF III*) inatekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini zilizo katika Mazingira Hatarishi Tanzania Bara na Zanzibar. Katika kutekeleza mpango huo, utaratibu wa uhawilishaji fedha kwa kaya masikini ulifanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 22 ambapo kaya 138,032 katika Vijiji na Shehia 1,179 zilitambuliwa na kuandikishwa katika Mfumo wa Masijala wenyе walengwa 464,552. Hadi sasa, Shilingi bilioni 5.5 zimehawilishwa katika kaya hizo. Lengo ni kuziwezesha kaya hizo kupata chakula na kujiongezea fursa ya kipato.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imejenga uwezo kwa Viongozi na Wataalam kutoka maeneo ya utekelezaji wa Mpango huo. Uwezo umejengwa kwa kutoa mafunzo katika masuala ya utambuzi, uandikishaji na ukusanyaji taarifa za kaya masikini. Aidha, mafunzo ya usanifu wa miradi ya ujenzi yalitolewa kwa wataalam kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pia, Wajumbe 17 wa Baraza la Wawakilishi na Wakuu wa Mikoa na Wilaya kutoka Zanzibar walitembelea Vijiji vya Pongwe-Kiona na Malivundo (Bagamoyo) na Gwata (Kibaha) ili kujifunza kuhusu utekelezaji bora wa mpango huo. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea kufanya utambuzi na uandikishaji wa kaya masikini kufikia maeneo yote 161 ya utekelezaji wa mpango Tanzania Bara na Zanzibar. Lengo ni kutambua na kuandikisha Kaya 920,000 kutoka Vijiji, Mitaa na Shehia 9,000.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa chakula ni ya kuridhisha. Katika maeneo mengi nchini kufuatia mavuno mazuri ya msimu wa 2012/2013, uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu huo ulikuwa tani milioni 14.38 ikililinganishwa na mahitaji ya chakula ya tani 12.15 kwa mwaka 2013/2014 ikiwa ni ziada ya tani trilioni 2.3 za chakula.

Ongezeko hilo limefanya Taifa kujitosheleza kwa chakula kwa Asilimia 118 na hivyo kufanya was tani wa bei za mazao ya chakula katika masoko nchini kuwa za chini katika kipindi chote cha mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na juhudhi za kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kulingana na Mipango inayotekelawa chini ya Kaulimbi ya Kilimo Kwanza, na Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa. Katika mwaka 2013/2014, Serikali imesambaza jumla ya vocha za ruzuku 2,796,300 zenyе thamani ya Shilingi bilioni 83 kwa ajili ya mbcolea na mbegu bora za mpunga na mahindi kwa Kaya 932,100. Pia, Serikali ilitoa ruzuku ya dawa za korosho kiasi cha lita 158,845 na tani 620 zenyе thamani ya Shilingi bilioni 1.5.

Vilevile, ruzuku ilitolewa kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu bora za pamba tani 4,000 zenyе thamani ya Shilingi bilioni 4.8, miche ya kahawa 350,000 zenyе thamani ya Shilingi milioni 100 na miche ya chai 1,850,000 zenyе thamani ya Shilingi milioni 300.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, ongezeko la tija katika uzalishaji wa mazao unategemea sana huduma bora za ugani kwa wakulima. Serikali katika mwaka 2013/2014, ilioa kibali cha kuajiri Maafisa Ugani 1,452 ili kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya kuwa na Afisa Ugani wa Kilimo mmoja kwa kila kijiji. Vilevile, Serikali imeongeza Mashamba Darasa kutoka 16,330 yenye wakulima 344,986 mwaka 2012/2013 hadi 16,543 yenye wakulima 345,106 mwaka 2013/2014 ili kuimarisha utoaji wa mafunzo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kushirikisha Washirika wa Maendeleo kuchangia Programu za Kuendeleza Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania, yaani SAGCOT.

Miongoni mwa malengo ya Programu hiyo ni kuwaunganisha wakulima wadogo na mnyororo wa thamani wa kibiashara wa Makampuni makubwa ya ndani na nje ya nchi. Ili kufikia lengo hilo, Serikali imeanzisha Mfuko Chochezaji wa Uendelezaji wa Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (*SAGCOT Catalytic Trust Fund*). Mfuko huo utatoa mitaji itakayoghamaria hatua za awali za miradi inayotoa tija ya haraka ambayo imebainishwa kwenye Mpango Mkakati wa Uwekezaji.

Vilevile, Mfuko huo utahamasisha biashara inayolenga kumwinua mkulima mdogo kwa kumuunganisha na mnyororo wa thamani na kampuni kubwa kupitia madirisha makuu mawili. Dirisha la kwanza ni *Matching Grant Fund* linalolenga kuwezesha kampuni kubwa zilizoanzisha biashara ya kilimo nchini, kuimarisha mnyororo ya thamani inayowahusisha wakulima wadogo zaidi au kuanzisha kilimo cha mkataba katika wakulima wakubwa na wakulima wadogo.

Dirisha la pili ni *Social Venture Capital Fund*, linalolenga kuziwezesha biashara changa na za kati kwenye Sekta ya Kilimo au kuwezesha Kilimo cha mkataba katika wakulima wakubwa na wakulima wadogo. Tayari Bodi ya Mfuko imeteuliwa na Mtendaji Mkuu wa Mfuko ameajiriwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali kupitia Mfumo wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa, inategemea kuvutia uwekezaji na kuanzisha Kilimo cha mashamba makubwa 25 ya Kilimo cha kibiashara kwa mazao ya mpunga na miwa kwa utaratibu wa kuwaunganisha wakulima wakubwa na wadogo wanaozunguka mashamba hayo. Aidha, itaanzisha, itaboresha na kuendesha kitaalamu maghala 275 ya kuhifadhi mahindi kwa kuwaunganisha wakulima katika umaja wa kibiashara kwa ajili ya kupata masoko ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuendeleza kilimo cha umwagiliaji nchini, Sheria ya Umwagiliaji Na. 5 ya mwaka 2013 imeanza kutumika Januari, 2014. Sheria hiyo itaiwezesha Serikali kuanzisha Tume ya Umwagiliaji ambayo ni chombo cha kitaifa chenye dhamana ya kusimamia, kuendeleza na kudhibiti shughuli za umwagiliaji nchini. Sheria hiyo pia itaanzisha Mfuko wa Taifa wa Umwagiliaji utakaosaidia kutekeleza mipango ya umwagiliaji kwa kulipia gharama za umwagiliaji zinazofanywa na mkulima mmoja mmoja na wawekezaji kupitia mikopo na dhamana. Serikali pia iliendelea na ujenzi na ukabarati wa skimu 24 za umwagiliaji zilizopo katika wilaya 15 nchini. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendeleza Skimu za Umwagiliaji 39 kwa ajili ya kilimo cha mpunga.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali kupitia Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Kifedha Vijijini imekarabati kilometra 352 za barabara za vijijini kwa kiwango cha changarawe katika Halmashauri za Iringa Vijijini, Njombe Vijijini, Singida Vijijini, Mbarali, Lushoto, Same, Mbulu, Msalala na Mpanda. Halmashauri nyingine ni Maswa, Songea Vijijini, Rufiji, Karatu na Ksimba. Vilevile, imejenga maghala matano yenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 za mazao kila moja katika Halmashauri za Iringa Vijijini, Njombe Vijijini, Same, Songea na Mbarali na kukarabati maghala matatu katika Halmashauri za

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Sumbawanga, Mbulu na Kahama. Aidha, Programu hiyo imezijengea uwezo Benki tisa za wananchi/ushirika ili kuimarisha mfumo wa kifedha Vijiji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali kupitia Programu hiyo, imepanga kukarabati kilometra 434 za barabara kwa kiwango cha changarawe, kujenga maghala 14 na masoko saba katika Halmashauri 64 za Tanzania Bara na Wilaya 10 za Zanzibar.

Aidha, wazalishaji wadogo kutoka Mikoa 24 ya Tanzania Bara na Mikoa mitano ya Zanzibar watajengewa uwezo wa kuhifadhi mazao na mbinu za kufikia masoko ambapo zaidi ya wananchi 100,000 watanufaika na mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 imetungwa na imeanza kutumika Januari, 2014. Sheria hiyo itawezesha kuanzishwa kwa Tume ya Maiendeleo ya Ushirika ambayo itakuwa na majukumu ya kusimamia moja kwa moja Vyama vyote vya Ushirika. Aidha, kupitia Sheria hiyo, Serikali imetua Waraka Na.1 wa mwaka 2014 unaotoa ufanuzi kuhusu Chaguzi katika Vyama vya Ushirika. Ili kuondoa migogoro ya kimaslahi, Waraka huo umewaondoa Viongozi wa Siasa na Serikali katika uongozi wa Vyama vya Ushirika katika ngazi zote. (Makofii)

Katika mwaka 2014/2015, Serikali itaimarisha uratibu wa Vyama vya Ushirika kulingana na mahitaji ya Wananchi na kuunganisha Vyama vya Ushirika na Taasisi za fedha ili kuboresha utoaji wa huduma za kifedha kwa Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mpango wa Ruzuku ya dawa ya kuogeshea mifugo, Serikali ilitoa jumla ya lita 11,020 zenye thamani ya Shilingi milioni 181.8 na kusambazwa nchini. Vilevile ilitoa chanjo kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya mifugo ambapo dozi 150,000 za chanjo ya ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa zenye thamani ya Shilingi milioni 119 ilitolewa katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga na Dodoma. Vilevile Serikali imeimarisha Kituo cha Uhamilishaji kilichopo katika eneo la Usa River, Arusha pamoja na Vituo vingine vitano vya Kanda kwa kusimika mitambo ya kuzalisha kimiminika cha naitrojeni na kujenga Vituo vitano vya madume bora.

Vilevile ng'ombe walionenepeshwa wameongezeka kutoka 132,246 mwaka 2011/2012 hadi kufikia 175,000 mwaka 2013/2014. Ili kuboresha upatikanaji wa maziwa nchini, Serikali imeongeza uzalishaji mitamba katika mashamba yake kutoka mitamba 943 kwa mwaka 2012/2013 hadi mitamba 1,046 mwaka 2013/2014 na kusambaza mbuzi wa maziwa 9,530 kupitia Mpango wa Kopa Mbuzi lipa Mbuzi.

Jitihada hizi zimesaidia wafugaji kuongeza tija na hivyo kuchangia ongezeko la uzalishaji wa maziwa kutoka lita bilioni 1.9 mwaka 2012/2013 hadi lita bilioni 2 mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Serikali itatoa ruzuku ya dawa za kuogesha mifugo na kununua dozi milioni moja kwa ajili ya chanjo ya ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa kwa Mikoa ya Arusha, Tanga, Tabora na baadhi ya Mikoa katika Kanda ya Ziwa. Vilevile Serikali itaimarisha Vituo vya uhamilishaji, mashamba ya kuzalisha mifugo bora na yale yanayozalisha mbegu bora za mifugo pamoja na kununua mifugo wazazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali kwa kushirikiana na wadau ilihuisha Sera ya Taifa ya Uvumi ya mwaka 1997 na Sheria ya Uvumi Na. 22 ya mwaka 2003 ili ziendane na mabadiliko ya kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia. Katika kuimarisha ufugaji wa samaki, wakulima 2,604 walipewa mafunzo ya ufugaji bora wa samaki na mabwawa 64 yalichimbwa. Hatua hiyo imeongeza idadi ya mabwawa ya Samaki kufikia 20,198 yenye uwezo wa kuzalisha tani 3,029.7 za samaki ikilinganishwa na mabwawa 20,134 yaliyokuwepo mwaka 2012/2013.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Vituo vya kuzalisha vifaranga vya samaki kwa wingi kwa kutumia teknolojia ya ndani viliongezeka kutoka kituo kimoja mwaka 2012/2013 hadi kufikia vituo vitano mwaka 2013/2014 vyenye uwezo wa kuzalisha vifaranga bora wa samaki milioni 10 kwa mwaka. Serikali pia, ilijenga matanki sita yenye lita za ujazo 8,000 kila kimoja kwa ajili ya kuzalisha vifaranga vya samaki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali itaanzisha Vituo vya kuzalishia vifaranga vya samaki katika maeneo ya Bacho Dareda - Manyara, Hombolo – Dodoma, na Kigoma. Vilevile, itajenga bwawa la kufuga samaki katika Kituo cha Mafunzo ya Kilimo cha Kilimanjaro – KATC; na kutoa ruzuku kwa ajili ya kuchimba mabwawa na kuzalisha vifaranga vya samaki.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya ufugaji nyuki imeendelea kuimarika na kuchangia kuongeza ajira na kupunguza umasikini. Mwaka 2013, thamani ya mauzo ya asali nje yalifikia Shilingi milioni 287.3 ikilinganishwa na mauzo ya Shilingi milioni 262 mwaka 2012. Katika kipindi hicho, jumla ya tani 384 za nta zenye thamani ya Shilingi milioni 4,660 ziliuzwa nje ikilinganishwa na tani 277 zenye thamani ya Shilingi milioni 2,583 zilizouzwa mwaka 2012.

Nchi zilizoongoza katika ununuzi wa asali na nta ya Tanzania ni Ujeruman, Oman, China, Japan, Yemen, India, Ubelgiji, Botswana, Kenya na Marekani. Kutokana na maendeleo haya mazuri katika mwaka 2013/2014, Serikali imetenga maeneo 20 yenye ukubwa wa Hekta 58,445 sehemu mbalimbali nchini kwa ajili ya hifadhi za nyuki. Aidha, imetoa mafunzo kwa wafugaji nyuki 924 na vikundi 49 kutoka Wilaya 12 pamoja na kutoa elimu ya miongozo na sheria za ubora wa mazao ya nyuki kwa wafanyabiashara wa mazao ya nyuki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Tanzania iilishi kwenye Kongamano la Ufugaji Nyuki liliofanyika Kiev, Ukraine. Katika Kongamano hilo, mazao ya nyuki kutoka Tanzania yalikuwa kivutio kikubwa na yaliwezesha kupata medali ya Banda Bora la Asali kutokana na asali yake kuwa na viwango vya ubora na usalama vinavyokubalika Kimataifa. Aidha, kampuni mbalimbali zilionesha nia ya kuwekeza kwenye Sekta ya ufugaji nyuki nchini.

Kama ambavyo nimesisitiza mara kwa mara, Sekta ya Nyuki ina fursa kubwa ya kibiashara hapa nchini na nje ya nchi. Ni sekta inayoweza kuleta mapinduzi makubwa katika maeneo mengi kwani yanahitajika mafunzo kidogo na vifaa vichache ambavyo vinaweza kutumika kikamilifu kupata asali na mazao yake. Niendelee kusitiza kwamba, tuwahimize wananchi katika Majimbo yetu watumie fursa za ufugaji nyuki zinazopatikana katika maeneo yao ili kujiungezea kipato.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imeendelea kutoa mchango muhimu katika upatikanaji wa ajira, ongezeko la kipato na ukuaji wa uchumi. Katika mwaka 2013/2014, Serikali imefungua Vituo vya Teknolojia Mikoani kwa ajili kuhudumia Wajasiriamali wanaotengeneza mashine za kusindika mazao na kutengeneza bidhaa mbalimbali za uzalishaji mali. Vituo hivyo vimewezesha kuanzishwa kwa miradi mipy 4,127 ya uzalishaji mali kwenye Mikoa ya Lindi, Mbeya, Iringa, Arusha, Kigoma na Kilimanjaro.

Aidha, Wajasiriamali 23,546 walipatiwa mafunzo ya ujasiriamali na ujuzi maalum wa ufundu na utumiaji wa mashine za uzalishaji mali. Vilevile, huduma za ushauri na ugani zilitolewa kwa Wajasiriamali 20,769 kwenye vikundi na Vyama vyao vya Biashara kwa kuviiimarisha na kuviwezesha kujenga misingi ya kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Mkakati wa "Wilaya Moja, Bidhaa Moja" kwa kujenga uwezo wa kuzalisha bidhaa kutokana na malighafi zilizopo kwenye Wilaya husika. Kupitia Mkakati huo, Serikali imejenga uwezo wa kuongeza thamani ya mazao na bidhaa

## Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

mbalimbali, kuzalisha mitambo na vipuri pamoja na zana za kilimo ambapo viwanda vidogo 198 vilianzishwa na kuwezesha upatikaji wa ajira 1,809. Aidha, Serikali inatekeleza Mradi wa Kuendeleza Ujasiriamali Vijijini (MUVI) kwa kutumia dhana ya kuimarishe mlolongo wa thamani kimikoa kwa mazao mbalimbali. Mradi umewezesha uanzishwaji wa miradi midogo 15,580 Vijijini; urasimishaji wa Vikundi 65,308 vya uzalishaji na upatikanaji wa ajira 39,574.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia iliendelea na juhudi za kuhamasisha uwekezaji kwenye miradi mipyä katika Maeneo Maalum ya Uzalishaji (*Export Processing Zones*) na Maeneo Maalum ya Kiuchumi (*Special Economic Zones*). Hadi kufikia Desemba, 2013, kampuni 32 zilikuwa zimesajiliwa na Mamlaka ya EPZ kwa ajili ya kuanzisha viwanda vipyä kwenye maeneo hayo. Aidha, Serikali imekamilisha utafiti kwenye Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na kuthibitisha uwepo wa tani milioni 370 za makaa ya mawe katika eneo la kilomita za mraba 30 kati ya kilomita za mraba 140 zilizotengwa kwa ajili ya Mradi huo.

Aidha, utafiti huo ulithibitisha uwepo wa tani milioni 219 za madini ya chuma katika eneo la kilomita za mraba 10 kati ya kilomita za mraba 166 zilizotengwa kwa ajili ya mradi huo. Ujenzi wa mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma na madini ya chuma Liganga unatarajiwa kuanza mwaka 2014 na kukamilika mwaka 2018.

Katika mwaka 2014/2015, Serikali itajielekeza katika kuendeleza viwanda vya kuongeza thamani ya mazao na bidhaa za kilimo. Aidha, itaendelea kujenga Mradi wa Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Ngaka na Mradi wa Chuma Liganga.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutangaza fursa za utalii zilizopo nchini kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile vipeperushi, majorida, matangazo ya television na kutumia Balozi za Tanzania zilizopo nje ya nchi. Mbinu nydingine zilizotumika ni kutumia maonesho ya Kimataifa na kuweka matangazo kwenye viwanja sita vya ligi kuu ya mpira wa miguu Uingereza.

Pamoja na matangazo hayo, huduma za kitalii hususan hoteli, miundombinu ya barabara na mawasiliano zimeimarishwa na hivyo kuwashawishi watalii wengi kutembelea nchini. Kutohata na hatua hizo, idadi ya watalii walioingia nchini imeongezeka kutoka watalii 1,077,058 mwaka 2012 hadi 1,135,888 mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 5.46. Watalii hao wameliingizia Taifa Dola za Kimarekani bilioni 1.8 ikilinganishwa na Dola za Marekani bilioni 1.7 zilizopatikana mwaka 2012.

Vile vile Serikali imanzisha utalii wa usiku katika hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, utalii wa kuangalia wadudu katika hifadhi ya Taifa ya Kitulo na Hifadhi ya Amani. Utalii wa Makasia katika Hifadhi ya Arusha, Ziwa Momela na utalii wa kutembea katika Hifadhi za Mahale na Gombe.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi kupitia Baraza la Taifa la Biashara, imeandaa Mkakati Maalum wa Kukuza Sekta ya Utalii, hasa kuondoa vikwazo vinavyokwamisha kasi ya ukuaji wa Sekta hiyo. Aidha, katika kukuza utalii wa ndani Serikali inatumia fursa za maonesho na matamasha mbalimbali ya ndani kuelezea vivutio vya utalii, na imeandaa kijitabu cha utalii wa utamaduni kwa lengo la kutangaza vivutio vya utalii.

Katika mwaka 2014/2015 Serikali itatafsiri tovuti ya Bodi ya Utalii pamoja na vielelezo mbalimbali vya lugha za Kifaransa, Kijerumani, Kichina, Kihispaniola ili zitumike kutangaza utalii kwa nchi zinazotumia lugha hizo. Hatua hiyo itasaidia kupanua wigo wa utalii katika masoko hayo yenye fursa kubwa.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na juhudi za kuhifadhi wanyamaporu katika hifadhi ya mapori ya akiba nchini kwa nia ya kuwalinda na kuendeleza utalii.

Katika mwaka 2013/2014 Serikali imeendesha doria mbalimbali ndani na nje ya hifadhi zilizowezesha kukamatwa watuhumiwa 391 pamoja na silaha 73, zikiwemo bunduki 22 za kivita. Jumla ya kesi 277 zilifunguliwa ambapo kesi 123 zimemalizika na kesi 154 zinaendelea. Vile vile katika kuhamasisha wananchi wanaoishi kando kando ya hifadhi hizo kuzilinda, Halmashauri 38 zenye vitalu vya uwindaji zilipatiwa Shilingi bilioni 8.7 kama mgao wa asilimia 25 ya fedha zinazotokana na uwindaji wa kitalii kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Serikali itaanza utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa kupambana na ujangili. Mkakati huo umeainisha uwezo tulionao, upungufu uliopo na mahitaji muhimu ambayo yataimarisha uhifadhi nchini na kupunguza migongano iliyopo ya matumizi ya ardhi. Vile vile itaanisha mamlaka ya wanyamaporu Tanzania itakayosimamia shughuli zote zinazohusu hifadhi za wanyamaporu ikiwa ni pamoja na kukusanya mapato, kuendeleza hifadhi na kuimarisha ulinzi wa wanyamaporu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Serikali imeimarisha ukaguzi kwenye uzalishaji na biashara ya madini. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuweka Wakaguzi katika migodi yote mikubwa na baadhi ya mitambo ya uchenjuaji wa madini. Aidha, imeanzisha dawati maalum la kukagua madini yanayosafirishwa nje ya nchi kuitia viwanja vya ndege ili kudhibiti utoroshaji wa madini. Kutokana na jitihada hizo, madini ya dhahabu na vito yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.9 yalikamatwa na kuwasilishwa kwenye vyombo husika kwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali inathamini mchango wa wachimbaji wadogo wa madini katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Katika mwaka 2013/2014 Serikali imewajengea uwezo wachimbaji wadogo kwa kuwapatia mafunzo na mikopo ili kuongeza uzalishaji. Kutokana na juhudi hizo, jumla ya kilo 237 za dhahabu zenye thamani ya Shilingi bilioni 14.5 zilizalishwa na kuingiza mrabaha wa Shilingi milioni 519.

Aidha, Serikali imetenga maeneo mapya ya uchimbaji wa Isamilo na Iwenge Geita, Rwabasi Butiama na Saza na Itumbi 'B' Chunya. Jitihada hizo zimefanya shughuli za wachimbaji wadogo hasa katika uchenjuaji wa madini ya dhahabu kukua.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Serikali itakamilisha mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Madini ya Mwaka 2009, Sheria ya Uongezaji Thamani Madini na Sheria ya Baruti pamoja na kanuni zake.

Serikali pia itahamasisha uwekezaji kwenye Sekta ya Madini na kuziwezesha Taasisi zote kama vile *Tanzania Extractive Industrials Transparency Initiatives* na Shirika la Madini la Taifa STAMICO ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi. Vile vile itatenga maeneo zaidi kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kuwawezesha kupata mitaji na teknolojia. Pia itaboresha mfumo wa utoaji na usimamizi wa leseni za madini kwa kuanzisha huduma za kuomba leseni kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Spika, ardhi ni msingi na kichocheo muhimu cha maendeleo ikiwa itapangiwa matumizi bora, itapimwa na kusimamiwa vizuri. Ili kufanikisha azma hiyo, Serikali inachukua hatua madhubuti kuhakikisha kuwa kila kipande cha ardhi nchini kinapangwa, kupimwa, kumilikishwa na kutumiwa kwa mujibu wa sheria. Katika mwaka 2013/2014 Serikali imekamilisha sehemu ya kwanza ya ujenzi wa mfumo unganishi wa kuhifadhi kumbukumbu za

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ardhi, yaani *Integrated Land Management Information System* na kurahisisha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji na matumizi mengine.

Sambamba na hatua hiyo, Serikali inaboresha utunzaji wa kumbukumbu za upimaji ardhi kwa kuzibadili zilizopo kuwa katika mfumo wa kanzidata za kielektroniki ili ziweze kuunganishwa na mfumo unganishi wa kutunza kumbukumbu za ardhi. Hatua hiyo inalenga kurahisisha upatikanaji wa taarifa za upimaji ardhi na kuboresha utoaji huduma kwa wananchi.

Hadi mwezi Februari, 2014 kumbukumbu za ramani 5000 za Jiji la Dar es Salaam zimebadilishwa na kuwekwa katika ramani unganishi. Katika mwaka 2014 Serikali itaandaa kanzidata ya viwanja 300,000 katika Miji mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Serikali imekumbwa na tatizo la migogoro ya mara kwa mara inayotokana na matumizi mbalimbali ya ardhi hususan baina ya wakulima na wafugaji. Aidha, migogoro hiyo imekuwa ikihusisha wananchi na maeneo ya hifadhi. Vijiji kuwepo ndani ya maeneo ya hifadhi, wananchi dhidi ya wawekezaji, baina ya wananchi wenyewe kwa wenyewe. Migogoro hii imekuwa ikiongeza zaidi katika siku za hivi karibuni kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu, mifugo na shughuli za kiuchumi zinazotegemea ardhi kama vile madini, utalii, viwanda kilimo na makazi.

Migogoro ya ardhi ina athari kubwa kwa wananchi ikiwemo uvunjifu wa amani, uharibifu wa mali na hata vifo. Serikali imekuwa ikichukua hatua kudhibiti migogoro hiyo kila inapotokea. Ili kupata suluhisho la kudumu la kushughulikia migogoro ya ardhi, Serikali imeanza kusimika mifumo ya kisasa kwa ajili ya upimaji, umilikishaji na usimamizi wa Sekta ya Ardhi.

Hii ni kwa sababu uzoefu umeonesha kwamba ukosefu wa ramani, mipaka rasmi na miliki kamilifu ndicho chanzo kikuu cha migogoro inayojiteza mara kwa mara. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itatoa kipaumbele katika Sekta ya Ardhi, hasa kushughulikia maeneo yanayolenga kutatua migogoro ya ardhi kama vile upimaji wa mipaka ya vijiji, kutoa hati miliki na kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji.

Aidha, Serikali itajenga mfumo unganishi wa kutunza kumbukumbu za ardhi, kukamilisha usimikaji wa alama za msingi za upimaji, kurasimisha hati miliki na kupima mipaka Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeimarisa huduma za upatikanaji wa umeme nchini kwa kutekeleza miradi mbalimbali ili kuongeza miradi ya wananchi wanaopata umeme. Mwaka 2013/2014 Serikali imekamilisha kwa asilimia 90 awamu ya kwanza ya mradi kabambe wa usambazaji wa umeme unaotekelozwa katika Mikoa 16 nchini.

Pia mradi huo unajumuisha usambazaji wa umeme vijiji, ambapo wateja 15,305 kati ya wateja 22,000 waliolengwa wameunganishiwa umeme.

Vile vile Wakala wa Nishati vijiji imesaini mikataba 35 na wakandarasi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya usambazaji umeme vijiji kuititia mradi kabambe wa usambazaji wa umeme vijiji.

Aidha, tarehe 8 Septemba, 2013 Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua mtambo wa kufua umeme wa Megawati 60 unaotumia mafuta mazito katika eneo la Nyakato, Mwanza. Mtambo huo umeongeza uwezo wa kufua umeme kwenye gridi ya Taifa na kufikia Megawati 1,583. Mtambo huo umeimarisha upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Mwanza, Geita na Mara. Kutokana na juhudzi za kusambaza umeme mijini na vijiji, hadi mwezi Machi, 2014 zaidi ya asilimia 30 ya Watanzania

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wamepatiwa huduma hiyo na hivyo kuvuka lengo la asilimia 30 lilitarajiwa kufikiwa mwaka 2015. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukua kwa kasi kwa Sekta ya Gesi, Serikali katika mwaka 2013/2014 imeandaa Sera ya Gesi Asilia ambayo inatoa miongozo ya kusimamia rasilimali hiyo. Serikali pia inatekeleza miradi mbalimbali chini ya Sekta ndogo ya gesi, ikiwa ni pamoja na kuendelea na mradi wa ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam.

Hadi sasa, mabomba yote kwa ajili ya kutekeleza mradi huo wenyewe urefu wa kilomita 542 yamewasili na kazi ya kuunganisha inaendelea. Ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi pamoja na mitambo miwili ya kuchakata gesi inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2014, yaani mwaka huu.

Aidha, awamu ya kwanza ya mradi wa Kinyerezi utakaozalisha Megawati 150 kwa kutumia gesi asilia umeanza kutekelezwa. Katika hatua nyingine, Serikali imepitia upya miundo ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na Shirika la Umeme Tanzania kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi wa utendaji wa mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Serikali itakamilisha mchakato wa maboresho ya sera mbalimbali za nishati ikiwemo sera ya nishati ya mwaka 2003, sera mpya ya mafuta na sera mpya ya uwezeshejaji wazawa. Kukamilika kwa sera hizo kutaimarisha usimamizi wa Sekta ya Nishati kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha awamu ya kwanza na ya pili ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano wenyewe urefu wa kilomita 7,560, ambao pia unatoa maunganisho ya mawasiliano kwa nchi jirani. Awamu ya tatu ya ujenzi itakayozunganisha Unguja na Pemba na Mkongo wa Taifa imeanza mwezi Desemba, 2013 na inatarajia kukamilika katika miezi 18. Mkongo umesaidia watoa huduma kufikisha huduma za mawasiliano kwa wananchi kwa uharaka zaidi, uhakika na kwa gharama nafuu.

Hatua hiyo inaharakisha maendeleo ya Taifa kwa wananchi kupata fursa ya kutumia Tehama katika kupambana na umasikini na kujiletea maendeleo kwa kasi zaidi. Pia Serikali kwa kutumia ruzuku imeendelea kupeleka huduma za mawasiliano katika maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Katika mwaka 2013/2014, jumla ya kata 52 zenye vijiji 316 zimefikishiwa huduma za mawasiliano kuititia mpango huo. Aidha, Serikali imetia saini makubaliano na watoa huduma za mawasiliano kufikisha huduma hizo katika kata nyingine 163 zenye vijiji 922. Watu 1,211,841 watanufaika na juhudhi hizo. Katika mwaka 2014/2015 Serikali itaendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa katika maeneo ya Mijini katika Miji ya Morogoro, Arusha Mwanza na Dodoma na kuendelea kuunganisha Unguja na Pemba na mkongo huo.

Mheshimiwa Spika, mazingira mazuri yaliyowekwa na Serikali kwenye Sekta ya Mawasiliano yameonesha matokeo chanya na ya kuridhisha sana. Idadi ya watumiaji wa huduma ya mawasiliano nchini imeongezeka kutoka laini za simu za mikononi milioni 2.96 mwaka 2005 hadi milioni 27.45 mwaka 2013. (Makofij)

Watumiaji wa mfumo wa *internet* nao umeongezeka kutoka milioni 3.56 mwaka 2008 hadi milioni 9.3 mwaka 2013. Pia kuna ongezeko kubwa la huduma kuititia mawasiliano ya simu za mikononi. Huduma hizo ni pamoja na miamala ya kifedha na ununuzi wa huduma na bidhaa kwa kutumia miamala ya kibenki. Hivi sasa wananchi wanaweza kufanya malipo ya huduma

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

mbalimbali wanazozitumia kupitia simu za kiganjani. Hatua hiyo imesaidia kuokoa muda na kupunguza msongomano sehemu za kulipia na kupata huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ililahidi Bunge lako Tukufu kwamba ingesimika mfumo wa kusimamia mawasiliano ya simu nchini, lengo la kujenga mfumo huo ni kubaini takwimu zinazopita katika mitandao za mawasiliano. Mfumo huo unaweza kutoa takwimu za mawasiliano yanayofanyika ndani na nje ya nchi, kutambua mapato na miamala ya fedha, kufuatilia na kugundua mawasiliano ya ulaghai na kutambua taarifa za laini ya simu na ya kifaa cha mawasiliano.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa tayari mtambo wa kuwezesha mfumo wa kusimamia mawasiliano Tanzania umejengwa kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 25, kwa kutumia utaratibu wa ubia kati ya Serikali na sekta binafsi, yaani *Build, Operate and Transfer*.

Ili kuweza kutumia mfumo huu ipasavyo Serikali imekamilisha kanuni za uhakiki na mgawanyo wa mapato yatokanayo na simu zinazoingia nchini kutoka nje ya nchi. Mfumo huo umeanza rasmi kutumika mwezi Oktoba, 2013, na kwa kipindi cha miezi mitatu ya Oktoba hadi Desemba, 2013 umeiingizia Serikali bilioni tano.

Katika mwaka 2014/2015 Serikali itaendelea kuborehsa taarifa za kiutendaji zitakazowezesha kupunguza kasi ya udanganyifu wa simu zinazoingia nchini kwa lengo la kuongeza mapato. Vile vile Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania itasimamia miamala ya malipo ya fedha kupitia simu za mkononi yanayofanywa na Kampuni za Simu.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba Serikali ilianza kutekeleza awamu ya kwanza ya zoezi la kuhama kutoka mfumo wa utangazaji wa analogia kwenda dijitali tarehe 31 Desemba, 2012. Awamu hiyo ilihuisha miji saba ya Dar es Salaam, Mbeya, Tanga, Mwanza, Arusha Dodoma na Moshi. Uhamaji huo ulifanyika kwa mafanikio makubwa na tathmini ilifanywa ili kuweka mazingira bora zaidi ya kuendele na zoezi hilo.

Kufuatia tathmini hiyo, awamu ya pili ilianza kutekelezwa kuanzia tarehe 31 Machi, 2014 na inatarajiwa kukamilika tarehe 30 Septemba, 2014. Miji kumi itakayohusika na zoezi hilo ni Singida, Tabora, ikifuatiwa na Miji ya Musoma, Bukoba, Kigoma, Kahama, Iringa, Songea, Morogoro na Lindi. Uzimaji wa mitambo ya utangazaji wa analogia unahuisha maeneo yote yanayopata huduma za matangazo kupitia mitambo ya kusimikwa ardhini tu ambayo ni asilimia 24 ya eneo lote la nchi yetu.

Maeneo yanayopata huduma za matangazo kupitia mitambo ya satelaiti na cable hayahusiki na zoezi hilo. Serikali imelenga ifikapo mwezi Oktoba, 2014 mitambo yote ya analogia iwe imezimwa nchini. Napenda kurudia wito wangu kwamba zoezi hili ni la muhimu na lina lengo la kuifanya nchi yetu iendane na mabadiliko yanayotokea duniani ambayo hayakwezeki. Wadau wote watoe ushirikiano kwa vyombo vinavyohusika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Serikali imekamilisha ujenzi wa kilometra 505.7 za barabara kuu na kukarabati kilometra 146.6. Aidha, imejenga kwa kiwango cha lami kilometra 22.3 za barabara za Mikoa na kukarabati kilometra 145.1 kwa kiwango cha changarawe. Serikali inaendelea kukamilisha ujenzi wa madaraja ya Kigamboni Dar es Salaam na mto wa Malagarasi Kigoma.

Katika mwaka 2014/2015 Serikali itajenga barabara mpya zenye urefu wa kilometra 633 za barabara kuu na barabara za Mikoa kwa kiwango cha lami. Vile vile itakarabati kilometra 165

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

za barabara za lami na kilomita 1,150 za barabara za changarawe katika barabara kuu na barabara za Mikoa. Aidha, itaendelea na ujenzi wa madaraja 57 ya barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam umekuwa kikwazo katika utekelezaji wa shughuli za kila siku za kiuchumi na kijamii. Katika kukabiliana na tatizo hilo, mwaka 2013/2014 Serikali imekamilisha ujenzi wa barabara za lami za *Ubungo Bus Terminal* – Kigogo – Kawawa yenye urefu wa kilometa 6.4, barabara ya Jeti – Kona – Vituka - Devis Kona yenye urefu wa kilometa 10.3 na barabara ya *UbungoMaziwa - Mabibo - External* yenye urefu wa kilometa 2.25 pamoja na daraja la *External*.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya mzunguko wa Kigogo - Jangwani yenye urefu wa kilomita 2.72 na zile zitakazotumika kwa mabasi yaendayo kwa haraka unaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Serikali itajenga barabara sita Jijini Dar es Salaam kwa kiwango cha lami. Barabara hizo ni Tabata – Dampo – Kigogo kilometa 1.6, Kifuru - Kinyerezi Kilomita nne, Goba - Mbezi Mwisho Kilometra saba, Tangi Bovu – Goba Kilometra tisa, Kimara – Baruti - Msewe kilometra 2.6 na Kimara - Daraja la Maji Chumvi – *External* kilometra tatu. Tayari Serikali imesaini mikataba na wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo ambazo zinatarajija kukamilika kati ya miezi nane hadi kumi na minane.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Serikali imefanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli ya Arusha Musoma yenye urefu wa kilometa 600. Lengo ni kuimarisha usafiri na usafirishaji wa mizigo kwa Mikoa ya kaskazini na nchi jirani ya Uganda kupitia Bandari ya Tanga. Vile vile Serikali imekamilisha usanifu wa kina wa mradi wa ujenzi wa reli kwa kiwango cha Kimataifa yenye urefu wa kilometa 1,464 kutoka Dar es Salaam – Isaka – Keza - Kigali na kilometa kutoka Keza hadi Msongati.

Mheshimiwa Spika, makataba wa maelewano kati ya Tanzania na Burundi kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Uvinza hadi Msongati umesainiwa. (*Makofii*)

Kuhusu reli ya TAZARA Serikali inatekeleza makubaliano ya itifaki ya 15 iliyosainiwa mwezi Machi, 2012 kati ya Serikali ya watu wa China na Serikali ya Tanzania na Zambia ambapo ununuzi wa vichwa vinne vya treni, vichwa vinne vya sogeza umefanyika pamoja na ununuzi wa mabehewa 18 ya abiria ya reli ya TAZARA.

Katika mwaka 2014/2015 Serikali itaboresha kilometra 308 za miundombinu ya reli ya kati na vituo vya bandari kavu ya kuhifadhi makasha, vya Ilala na Isaka. Aidha, Kampuni ya Reli itakarabati vichwa vinane vya treni na kununua vichwa 12 na mabehewa 204 ya mizigo na kukarabati majengo ya Stesheni.

Mheshimiwa Spika, kijirografia nchi yetu imejaliwa kuwa na eneo kubwa la maziwa na bahari ambako limetuwezesha kuwa na bandari zinazohudumia pia nchi jirani zisizopakana na bandari. Ili kutumia fursa hii kikamilifu, Serikali katika mwaka 2013/2014 imekamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuboresha gati namba moja na saba katika bandari ya Dar es Salaam.

Vile vile inatekeleza miradi ya ujenzi wa magati kwenye bandari za Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa. Aidha, kupitia mfumo wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa mamlaka ya Bandari imevuka malengo kwa kuhudumia zaidi ya tani milioni 13 za mizigo hadi Desemba, 2013 ikilinganishwa na tani milioni 12 kwa mwaka 2012.

Vile vile Serikali imeanza kutekeleza utaratibu wa kufanya kazi Bandarini kwa saa 24 kwa siku zote za juma, ili kuongeza kazi ya uondoshaji wa mizigo inayotoka. Hatua hiyo imesaidia

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kupunguza msongamano wa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam na kupunguza malalamiko kutoka kwa watumiaji wa Bandari hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha kumekuwa na ongezeko la ufanisi katika kuhudumia wasafirishaji wa mizigo katika maeneo ya mipakani hasa Rusumo, Tunduma, Namanga, Kasumulo na Mtukula. Wasafirishaji wanatumia muda mfupi hivi sasa ikilinganishwa na hapo awali. Kwa mfano, muda wa huduma katika mpaka wa Rusumo umepungua kutoka siku tatu hadi nusu saa (dakika 30). (Makofij)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali itaanza kuboresha Gati Namba Moja (1) hadi Saba (7) ili kuwezesha Bandari ya Dar es Salaam kuhudumia mizigo tani 18,000,000 kutoka tani Milioni 13.5 za sasa. Aidha, itakamilisha ujenzi wa Magati katika Bandari ya Mtwara, kukamililisha majadiliano na kuanza ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo na kuendelea na miradi ya ujenzi wa magati kwenye Bandari za Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa. Vilevile, itakarabati meli za MV Umoja, MV Victoria, MV. Butiama, MV Serengeti, MV Liemba, MT Sangara, MT Ukerewe na meli ya MV Songea ili kuboresha usafiri na usafirishaji katika Maziwa.

Mheshimiwa Spika, Usafiri wa Anga, Serikali imeboresha miundombinu ya viwanja vya ndege nchini na kuviwezesha kutoa huduma kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za uendeshaji za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, jumla ya viwanja vya Ndege 13 ikiwemo Viwanja vya Mwanza, Musoma, Bukoba, Kigoma, Tabora, Ausha, Tanga, Lindi, Mtwara, Iringa, Songea, Nachingwea na Kilwa Masoko vilifanyiwa ukaguzi nakupata leseni ya uendeshaji. Aidha, Serikali imeanza mradi wa ujenzi wa jengo jipya la tatu la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere utakaogharimu Shilingi Bilioni 518.

Mheshimiwa Spika, Mradi huo ambaa umewekwa jiwe la msingi na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 24 Aprili, 2014 unatarajiwaa kukamilika mwezi Oktoba, 2015. Jengo hilo litakuwa na ukubwa wa mita za mraba 70,000 ambaa ni zaidi ya maea nne ya ukubwa wa jengo lililopo sasa lenye ukubwa wa mita za mraba 15,000.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa jengo hilo na miundombinu yake, Uwanja huo utakuwa na uwezo wa kuegesha ndege kubwa za abiria. Aidha, utahudumia abiria milioni sita (6,000,000) kwa mwaka ikilinganishwa na abiria milioni 2.5 kwa sasa. Vile vile, Uwanja huo, utatoa fursa mbalimbali za kiuchumi, kibiashara na kukuza utalii nchini. Aidha, utazalisha ajira mpya zaidi ya 7,000 kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha miundombinu ya usafiri wa anga ili kuimarisha huduma za usafiri nchini pamoja na kuvutia uwekezaji na utalii. Kwa kuzingatia azma hiyo, mwezi Oktoba, 2013, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alizindua rasmi Uwanja wa Ndege wa Mafia baada ya ujenzi wake kukamilika kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kuzinduliwa kwa uwanja huo kumefungua fursa za kibiashara, hususan ya utalii, katika kisiwa hicho. Vile vile, mwezi Julai 2013, Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa njia ya kuruka na kutua ndege kwa kiwango cha lami katika Uwanja wa Ndege wa Bukoba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea na ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere na kukamilisha ujenzi wa Uwanja mpya wa Kimataifa wa Ndege wa Songwe, Mbeya. Serikali pia itakamilisha ukarabati

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wa Viwanja vya ndege vya Mwanza, Bukoba, Kigoma na Tabora na kuanza ukarabati wa viwanja vya ndege vya Shinyanga, Mtwara na Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Sekta ya Elimu: (Elimu ya Msingi); ili kuhakikisha kuwa utoaji wa elimu unafuata Sera. Miongozo na Mitaala, Serikali imeendelea kupitia Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995. Aidha, kupitia Mfumo wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa katika elimu ya msingi, utaratibu wa kupima stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (K3) kwa wanafunzi wa darasa la Kwanza na la Pili umeanzishwa kwa lengo la kupima na kuweka msingi wa kuboresha stadi husika kabla ya kuingia darasa linalofuata.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha, Serikali imeajiri jumla ya Walimu 17,928 wa shule za msingi na kupangiwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kuajiriwa kwa Walimu hao kutapunguza pengo la Walimu liliopo.

Mheshimiwa Spika, katka mwaka 2014/2015, Serikali kupitia Mfumo wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa, itaimarisha elimu ya msingi kwa kuongeza uwazi wa kiutendaji, kuwajengea Walimu uwezo wa kutoa msaada wa kimasomo kwa wanafunzi wenyewe uhitaji maalum, kuinua ubora wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia, kuongeza upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuongeza uwajibikaji wa watendaji katika utoaji wa elimu.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Sekondari, katika mwaka 2013/2014, Serikali imeweka juhudu kubwa katika kuimarisha Elimu ya Sekondari hasa ujenzi wa madarasa, nyumba za Walimu, maabara, ununuzi wa madawati na vitabu pamoja na kuboresha miundombinu na mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeajiri Walimu wapya wa Sekondari 18,410 na kutoa mafunzo kazini kwa Walimu 12,476. Kati ya hao, Walimu 8,400 ni wa masomo ya Sayansi na Hisabati. Hatua hizo zimechangia kuongeza ufaulu wa wanafunzi waliofanya Mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2013 kufikia asilimia 58.25 ikilinganishwa na asilimia 43.08 mwaka 2012. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itatoa kipaumbele cha uwekezaji kwenye miundombinu ya Shule za Sekondari, Walimu, Ukaguzi na Vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo ya Ufundu Stadi, Serikali imeanza kutekeleza Mpango wa maendeleo ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi wa mwaka 2013/2014 hadi 2017/2018. Mpango huo unalenga kuongeza udahili katika ngazi mbalimbali za Elimu na Mafunzo ya Ufundu ili kujenga uwiano wa nguvu kazi katika ngazi mbalimbali kwa kila fani.

Vilevile unalenga kujenga nguvukazi yenyewe kuhimili ushindani wa soko la ajira kwa kuinua ubora wa elimu na mafunzo ya ufundu ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Ili kutekeleza mpango huo, katika mwaka 2013/2014, Serikali ilianza kutumia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 25 kutoa mafunzo ya masomo ya ufundu stadi ili kuongeza udahili wa wanafunzi. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itaanza ujenzi wa vyuo vya ufundu stadi katika Mikoa ya Rukwa, Geita, Simiyu na Njombe.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Juu, Serikali imeboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia masomo ya sayansi na teknolojia kwenye Vyuo Vikuu nchini. Katika mwaka 2013/2014, kupitia Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Serikali imekamilisha ujenzi wa vyumba 48 vya mihadhara, maabara 93 za sayansi na ofisi 302 za wafanyakazi katika Vyuo Vikuu mbalimbali vya Umma nchini.

Aidha, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na vya TEHAMA vilinunuliwa katika Vyuo hivyo na kuziunganisha Taasisi 28 za elimu ya juu katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kutoptaka na kuwepo kwa malalamiko mengi kuhusu Vyuo Vikuu nchini kutoza ada tofauti kwa mafunzo ya aina moja, Serikali imekamilisha Mwongozo wa Gharama Halisi ya Kumsomesha Mwanafunzi wa Elimu ya Juu, Mwongozo huo unatoa ukomo wa ada inayotakiwa kutozwa na chuo kwa kila program au kozi kwa mwanafunzi.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kuondoa upangaji na upandishaji wa ada kiholela kwa wanafunzi wanaosoma elimu ya juu pasipo kuzingatia gharama halisi ya kumsomesha mwanafunzi husika kulingana na kozi anayosoma. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itasimamia utekelezaji wa Mwongozo huo.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Sekta ya Afya, (Huduma ya Mama na Mtoto); Serikali inaendelea kuimarisha huduma ya afya ya Mama na Mtoto kwa kutekeleza Mpango Mkakati wa kuongeza Kasi ya Kupunguza Vifo vitokanavyo na Matatizo ya Uzazi na Vifo vya Watoto wa mwaka 2008 hadi 2015.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mkakati huo, Serikali imeandaa Mpango Kazi wa Uzazi wa Mpango Uliothaminiwa. Mpango Kazi huo unalenga kununua na kusambaza dawa na vifaa vya uzazi wa mpango nchini. Aidha Serikali imeimarisha mfumo wa rufaa kwa mama wajawazito kwa kununua vyombo vya usafiri kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii na kuvisambaza katika mikoa yenye kiwango cha juu cha vifo vya mama vitokanavyo na matatizo ya uzazi.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Serikali inatekeleza Mpango Mkakati wa Kutokomeza Maaambukizi Mapya ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ambao ulizinduliwa Tarehe Mosi, Desemba, 2012 na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya kwanza ya Mpango huo ilianza mwezi Oktoba, 2013 na kuhusisha Mikoa tisa yenye uambukizo mkubwa wa VVU kwa wajawazito. Mikoa hiyo ni Iringa, Njombe, Mbeya, Tabora, Simiyu, Shinyanga, Mwanza, Geita na Kagera. Awamu ya pili imeanza mwezi Januari, 2014 kwa Mikoa 16 iliyobakia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali itakamilisha mapitio ya Mpango Mkakati wa Kuongeza Kasi ya Kupunguza Vifo vya Mama vitokanavyo na Uzazi na Vifo vya Watoto na kutekeleza afua (*interventions*) nyingine za kipaumbele.

Aidha, kupitia Mpango wa Kitaifa wa Uzazi wa Mpango dawa na vifaa vyote vya uzazi wa mpango vitanunuliwa na kusambazwa ili viweze kuwafikia wananchi wanaovihitaji. Lengo ni kufikia asilimia 60 ya kiwango cha utumiaji wa huduma za uzazi wa mpango kama ilivyoanishwa kwenye Malengo ya Maendeleo ya Milenia.

Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa Maambukizi ya Malaria, katika kukabiliana na maambukizi ya ugonjwa wa malaria, Serikali imeendelea kugawa vyandarua shulenii na kuhimiza matumizi endelevu.

Katika mwaka 2013/2014, Serikali iligawa vyandarua 510,000 katika shule 2,302 za msingi na Sekondari za Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma kupitia Programu ya Wanafunzi Shuleni. Aidha, kupitia mikakati na afua nyingine, Serikali ilisambaza vyandarua 879,856 vyenye viuatilifu vya muda mrefu kupitia Mpango wa Hati Punguzo kwa wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Cuba, inatekeleza Mpango wa kuangamizi Viluwiluvi vya Mbu kwa kutumia njia za Kibailoja katika Jiji la Dar es Salaam. Mpango huo pia, utatekelezwa katika Mikoa mingine mitano.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau iliendelea na zoezi la kupulizia dawa ya ukoko katika kaya 838,00 zilizopo kwenye Mikoa ya Kagera, Mara na Mwanza ambapo zaidi ya wananchi 4,505,752 wamekingwa dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa malaria.

Mheshimiwa Spika, pia, Serikali imekamilisha kusambaza kipimo cha malaria kinachotoa majibu ya haraka katika vituo vyote vya kutolea huduma nchini. Vile vile jumla ya dozi 14,655,000 za dawa mseto na vitendanishi 9,853,710 vimenunuliwa na kusambazwa katika vituo vya huduma na hivyo kuimarisha upatikanaji wa dawa na vitendanishi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea kugawa vyandarua milioni 7.2 vyenye viuatilifu vya muda mrefu kupitia Mpango wa Hati Punguzo na kuendeleza kampanye maalum ya kugawa vyandarua kwa jamii katika ngazi ya kaya.

Aidha, zoezi la kugawa vyandarua kwa wanafunzi shulenii litaendelezwa kwa Mikoa ya Kusini. Sambamba na hatua hizo, mradi wa kuangamizi viluwiluvi vya mbu katika mazalia utapelekwa katika Mikoa mingine mitano kwa kutumia viuatilifu (*Biolarvicides*) vitakazozalishwa katika kiwanda kinachojengwa Kibaha, Mkoba wa Pwani ambacho kinatarajiwa kuanza kazi mwaka huu 2014.

Mheshimiwa Spika, Huduma kwa Wazee na Watu Wenye Ulemavu, Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 na Sera ya Taifa ya Huduma na Maendeleo kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2014 zinasisitiza kuwa makundi hayo yana haki ya kupata matunzo katika jamii. Katika mwaka 2013/2014, Serikali ilioa huduma za msingi kwa wazee na watu wenye ulemavu wasiojiweza wanaotunzwa na kulelewa katika Makazi 17 ya Serikali.

Jumla ya wahudumiwa 1,235 walipatiwa huduma za msingi ikiwemo chaula, malazi, mavazi pamoja na kuwapatia vifaa yakiwemo magodoro, mashuka, vitanda na nyenzo za kujimudu. Vile vile, Serikali iliratibu huduma za mafunzo katika Makazi 24 yanayoendeshwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kupunguza malalamiko kuhusu upungufu wa huduma zinazotolewa.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kusisitiza kuwa, wazee na watu wenye ulemavu na wasiojiweza wanahitaji kupatiwa matunzo katika jamii zao. Huduma zinazotolewa kwenye vituo na taasisi za Serikali na zisizo za Serikali ni hatua za mwisho pale ambapo itathibitika kuwa mzee au mlemau huyo hana mtu kabisa wa kumtunza katika familia na jamii.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa wananchi kuendeleza utamaduni wa kuwatunza wazee wetu na watu wenye ulemavu. Huu ni utamaduni mzuri sana. Aidha, nazikumbusha Halmashauri kutenga fedha za kuyahudumia makundi hayo.

Katika mwaka 2014/2015, Serikali itazindua Baraza na Mfuko wa Taifa wa Huduma kwa Watu wenye Ulemavu ili kuwajengea na kuongeza uwezo wao katika kuzifikia fursa za maendeleo na kuimarisha utawala bora.

Mheshimiwa Spika, Lishe, katika mwaka 2013/2014, Serikali imendelea kusimamia Kanuni za Uongezaji wa Virutubishi katika vyakula ambapo viwanda vikubwa sita vya kusindika unga na ngano na viwanda vitatu vya kusindika mafuta ya kula vinaweka virutubishi katika vyakula vinavotengenezwa. Takwimu zinaonyesha kuwa, takribani watu milioni 10 wanatumia unga wa

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ngano uliorutubishwa na milioni nne wanatumia mafuta ya kupikia yaliyorutubishwa na vitamin A.

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali imeandaa Mpango wa uongezaji wa Virutubisho kwenye vyakula ngazi ya jamii ambapo utekelezaji wake ulishaanza katika Mikoa ya Iringa, Njombe, Arusha na Dar es Salaam. Mpango huo unalenga uwekaji wa virutubishi katika unga wa mahindi unaozalishwa na wajasiriamali wadogo na kusagwa kwenye viwanda vya kati na vidogo.

Mheshimiwa Spika, Sekta binafsi inashirikishwa kikamilifu katika mapambano dhidi ya utapiamlo nchini. Mwezi Mei 2013, Serikali itakabidhi tani nane za madini joto kwa Muungano wa Wasindikaji wa Chumvi katika maeneo mbalimbali nchini kama sehemu ya mchango wa Serikali wa kuimarisha Sekta Binafsi katika mapambano dhidi ya Utapiamlo. Serikali pia imeimarisha Maabara za uwekaji madini joto katika chumvi kwa kununua na kugawa vitendanishi katika Maabara 13 za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kupanua wigo wa wananchi wanaopata vyakula vyenye virutubishi. Natoa wito kwa Viongozi katika ngazi zote, kusimamia juhudhi hizo za Serikali na kuhakikisha zinaendelezwa katika maeneo yao. Aidha, nawasihi Wafanyabiashara wote wenye viwanda vya chakula kutekeleza jukumu hilo kikamilifu. Kwa wale ambao hawajakamilisha taratibu za ufungaji wa mashine za kuongeza virutubishi wafanye hivyo mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Upatikanji wa Maji Nchini, (Huduma za Maji Vijijini) Serikali inatekeleza Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 inayolenga kuboresha huduma ya maji Mijini na Vijijini kwa kushirikisha wananchi na Sekta Binafsi.

Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali iliweka lengo la kutoa huduma ya maji kwa asilimia 65 Vijijini katika umbali usiozidi mita 400. Ili kuongeza kasi ya kufikia lengo hilo, katika mwaka 2013/2014, Serikali iliongeza Bajeti ya maji kwa Shilingi Bilioni 184 kwa ajili ya kuendeleza miradi mbalimbali ya maji.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mradi wa Maji kwa Vijiji Kumi kila Halmashauri upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo ujenzi wa ukarabati wa miradi ya maji 248 katika Vijiji 270 umekamilika. Pia jumla ya vituo 10,393 vya kuchotea maji vinavyohudumia watu 2,598,250 vimejengwa.

Ujenzi wa miundombinu ya maji kwenye Vijiji 613 upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na miradi katika Vijiji 374 inafanyiwa tathmini ya zabuni. Aidha, katika kipindi hicho, vyombo vya watumiaji maji 373 vimeundwa.

Vile vile, katika kipindi cha miezi sita ya utekelezaji wa miradi ya maji chini ya BRN kinachoishia Desemba 2013, wanavijiji 2,390,000 wamefikishiwa huduma za maji safi na salama, ikilianganishwa na wanavijiji 300,000 hadi 500,000 waliokuwa wakipatiwa huduma za maji safi Vijijini kabla ya mpango huo kuanza.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inatekeleza Awamu ya Pili ya Mradi wa Maji ya Chalinze ambao utatoa huduma ya maji kwa Vijiji 47 vyenye watu 197,684 katika Wilaya za Bagamoyo, Pwani. Hadi kufikia Desemba 2013, utekelezaji wa mradi ulikuwa umefikia ailimia 88.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Serikali inaendelea na ujenzi wa mabwawa katika maeneo mbalimbali hususan maeneo kame kwa lengo la kuwapatia wananchi huduma ya maji kwa matumizi ya nyumbani na mifugo. Ujenzi wa mabwawa ya Iguluba (Iringa Vijijini na Wegero

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Butiama, Mara na ukarabati wa bwawa la Ingodini – Longido Arusha umekamilika. Ujenzi wa mabwawa ya Kawa (Nkasi, Rukwa), Sasajila (Chamwino, Dodoma), Mwanjoro (Meatu, Shinyanga) na Kidete (Kilosa, Morogoro) umekamilika kwa zaidi ya asilimia 75.

Mabwawa yaliyookamilika kwa wastani wa Asilimia 50 ni Habiya (Itilima, Simiyu), Sekeididi (Kishapu, Shinyanga) na Matwiga (Chunya, Mbeya).

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wananchi kulinda vyanzo vya miundombinu ya maji. Vile vile natoa wito kwa Viongozi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia vyema Vyombo vya Watumia Maji ili miradi hii iwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Maji Mijini, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika miji mikuu ya mikoa zinatoa huduma ya maji kwa wakazi wake kwa wastani wa asilimia 80.

Katika Jiji la Dar es Salaam, upatikanaji wa huduma ya maji utaongezeka zaidi mara baada ya upanuzi na ujenzi wa bomba kuu la maji kutoka Ruvu Juu na Ruvu Chini kukamilika. Kazi ya kulaza bomba la maji kutoka mtambo wa Ruvu Chini hadi Dar es Salaam lenye urefu wa kilomita 555.5 umekamilika kwa asilimia 60.5 na kazi ya kupanua mtambo wa Ruvu juu na kulaza bomba hadi Dar es Salaam imeanza mwezi Februari, 2014.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali itaanza kutekeleza Mpango Maalum wa Kuhifadhi na Kutunza Vyanzo vya Maji wa Miaka Mitano (2014/2015 – 2018/2019). Ili kuimarisha ushirikishwaji wa wadau katika shughuli za uhifadhi, utunzaji na ulinzi wa rasilimali za maji, Serikali itaendelea kutekeleza Mradi wa Maji kwa Vijiji Kumi kwa kila Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Utamaduni na Michezo: Utamaduni; katika mwaka 2013/2014, Serikali imeendelea na urasimishaji wa tасnia za filamu na bidhaa zake kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika ili kuiongezea Serikali mapato na kulinda kazi za wasanii. Moja ya hatua zilizochukuliwa ni kufanyika kwa operesheni ya kufuatilia matumizi ya stempu za kodi za Mamlaka ya Mapato Tanzania ambapo zaidi ya stempu milioni moja za bidhaa za filamu zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, jumla ya operesheni nane za kufuatilia filamu zilizoingia sokoni kinyume na taratibu zimefanyika na jumla ya filamu 301 zilibainika kuingia sokoni kinyume na taratibu na wahusika kuchukuliwa hatua. Natoa wito kwa mamlaka husika kuhakikisha kuwa zoezi hili linafanyika nchi nzima na linakuwa endelevu. Vile vile, natoa rai kwa wananchi kununua bidhaa za filamu zenye viwango zinazothibitishwa na uwepo wa stika maalum. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, Michezo; katika mwaka 2013/2014, Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa maendeleo ya michezo, imetekeliza Mradi wa Kimataifa wa Kukuza Ari ya Michezo wenye lengo la kuimarisha ushiriki wa vijana na watoto katika michezo bila kujali jinsia ama uwezo. Kutokana na juhudhi hizo, katika mashindano ya Kombe la Dunia kwa Watoto wa Mitaani yaliyofanyika nchini Bazil mwezi Aprili 2014, Timu yetu ya Watoto wa Mitaani ya Mkoani Mwanza imetwaa Kombe la dunia la Watoto wa Mitaani.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Vijana hawa kwa kuiletea nchi yetu heshima kubwa. Vijana hawa wanapaswa kuendelezwa ili waweze kutuwakilisha vyema katika mashindano mengine ya Kimataifa.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Aidha, mafanikio hayo yawe chachu ya kuendeleza michezo mingine nchini. Ni muhimu tukakumbuka kwamba, vipaji vya michezo viko vingi na vimejificha.

Kinachotakiwa ni kufanyika jitihada za dhati kuviiuba na kuvitumia. Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ishirikiane kwa karibu na Maafisa Utamaduni wa Halmashauri zote nchini kubuni mkakati maalum wa kuibua vipaji vya michezo kuanzia ngazi ya Kitongoji.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeendelea kufanya vema katika medani ya kimataifa kufuatia kazi nzuri aliiyoifanya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutunukiwa tuzo tarehe 9 Aprili, 2014 kwa kuwa kiongozi mwenye mchango mkubwa zaidi katika maendeleo Baraza Afrika kwa mwaka 2013 huko Jijini Washington, Marekani. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, tuzo hiyo ya heshima kubwa inayotolewa kwa viongozi wa Afrika ambao hutoa mchango mkubwa zaidi wa kiuchumi na kijamii kila mwaka kwa watu hao hutolewa na jarida maarufu la Kimataifa la *African Leadership Magazine Group*. Tuzo hiyo imetolewa kutokana na mwelekeo wake thabiti na wenyе mafanikio makubwa kwa masuala ya utawala bora. (Makofii)

Vilevile napenda kumpongeza Dkt. Stagomena Lawrence Tax kwa kushinda kinyang'anyiro cha Katibu Mtendaji wa Jumuia ya Nchi za Kusini mwa Afrika SADC mwezi Agosti, 2013. Namtakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yake na kuendelea kupeperusha vyema bendera ya nchi yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, tarehe 1 hadi 2 Julai, 2013, Watanzania walipokea ugeni mkubwa wa kiongozi mkubwa wa kiongozi wa Taifa la Marekani Rais Barack Obama aliyeambatana na mamia ya wafanyabishara. Kupitia ziara hiyo Marekani ilizundua mpango wa umeme Afrika (*Power Africa*) ambao utaongeza kwa mara mbili upatikanaji wa umeme katika Bara la Afrika. Tanzania ni mionganoni mwa nchi zitakazonufaika na mpango huo unaolenga kuzalisha zaidi ya megawati 8,000 za umeme katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Serikali ya Amerika imeahidi kutoa zaidi ya dola za Marekani bilioni saba. Kampuni za Marekani, Ulaya, Asia na Afrika ziliahidhi kutoa zaidi ya dola za Marekani bilioni tisa kwa ajili ya mradi huo kwa miaka mitano ijayo. Nchi yetu pia kuipitia ziara hiyo ilipata fursa ya kujitangaza na kujiweka katika nafasi nzuri ya kukuza uchumi, biashara, utalii na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji mzuri wa malengo ya maendeleo ya milenia ambayo yatafikia ukomo mwaka 2015 umeifanya nchi yetu izidi kung'ara kimataifa na hivyo kuwa kati ya nchi 30 zitakazounda kikundi kazi kitakachoandaa Malengo ya Maendeleo Endelevu yatakayotekelezwa baada ya mwaka 2015. Aidha, katika Mkutano wa Jukwaa la Uchumi uliofanyika Mjini Davos, Uswisi mwezi Februari 2014, Mpango wa *World Economic Forum* wa kuvutia uwekezaji katika miundombinu muhimu ulijadiliwa ambapo Bandari ya Dar es Salaam ilichaguliwa kuwa mionganoni mwa bandari zitakazonufaika na mpango huo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, tayari timu ya wataalam imefika nchini kufanya tathmini ya awali ya mradi huo. Aidha, kongamano maalum lilihusisha nchi kadhaa zinazohusika na mpango wa uchukuzi wa Ukanda wa Kati lilifanyika tarehe 15 Aprili, 2014. Kongamano hilo ilizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali imeendelea na mapambano dhidi ya rushwa kwa kutoa elimu kuhusu rushwa, athari zake na wajibu wa wananchi katika mapambano dhidi ya rushwa kupitia semina, midahalo, maonyesho ya kitaifa, vipindi vya radio na televisheni pamoja na machapisho. Aidha, tuhuma 3,872 zikiwemo tuhuma mpya 679 zilichunguzwa ambapo hadi sasa uchunguzi wa tuhuma 580 umekamilika. Majalada manne ya

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

tuhuma za rushwa kubwa yalifkishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa hatua za kisheria. Katika mwaka 2014/2015, TAKUKURU itaendelea kuchunguza tuhuma 3,193 zilizopo na mpya zitakazojiteze na kuendesha kesi 635 zilizopo Mahakamani na zile zitakazoendelea kufunguliwa. Vilevile itaendelea na uchunguzi wa tuhuma zitokanazo na taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetekeleza Awamu ya Kwanza ya Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa uwazi. Lengo ni kuendesha shughuli zake kwa uwazi zaidi ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi, kusikiliza wananchi, kupambana na rushwa na kujenga dhana ya kuaminika kwa wananchi. Katika mwaka 2013/2014, Serikali imechapisha bajeti yake kwa lugha rahisi ya Kiswahili na Kingereza na kuiweka katika tovuti ya Wizara ya Fedha ili iweze kusomwa na wananchi wote. Aidha, imeanzisha tovuti ya Serikali (*Government Porto*) yenye anuani ya <http://www.egov.go.tz/> na Kituo Maalum cha Mawasiliano kwa masuala ya mtandao nchini pamoja na kuimarisha tovuti ya ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itaanza kutekeleza Awamu ya Pili ya Mpango huo kwa kufanya shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutunga Sheria ya Uhuru wa Habari, kukamilisha na kuimarisha mfumo wa kuweka wazi taarifa na takwimu kwenye tovuti.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeendelea kukumbwa na maafa ambayo yameleta athari kwa wananchi na mali zao. Katika mwaka 2013/2014, ukame umesababisha upungufu wa chakula kwa watu 828,063 katika Wilaya 54 za Mikoa 14 nchini. Serikali ilitoa tani 26,663 za chakula cha msaada chenye thamani ya shilingi bilioni 15.2 pamoja na shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kukisafirisha hadi kwa walengwa. Mafuriko makubwa pia yametokea katika maeneo mengi hususan Mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, Pwani, Mbeya na Tanga, Kilimanjaro, Lindi na Dodoma, Iringa, Kagera na Mara na kusababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali na miundombinu. Katika kukabiliana na athari zilizojiteze, Serikali na wadau mbalimbali imetoa misaada ya dharura ya kibinadamu kwa waathirika na imechukua hatua za kurejesha miundombinu ya maji. Nitumie fursa hii kulipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania, TANROADS na Wakandarasi, wadau mbalimbali pamoja na wananchi wote kwa kazi kubwa waliyoifanya na misaada waliyoitoa kwa waathirika wa maafa yaliyojiteza. Napenda kurudia wito wangu kwa wananchi wote wanaoishi katika maeneo hatarishi na hasa mabondeni, watii maagizo ya Serikali kuondoka katika maeneo hayo na kuhamia katika maeneo yaliyoainishwa ambayo ni salama kwa maisha yao. Aidha, natoa wito kwa wananchi wote kufuata sheria ili kuepuka uvunjifu wa amani na kusababisha maafa kutokana na mapigano hasa ya kugombea ardhi na malisho.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya kuijengea jamii uwezo wa kukabiliana na maafa ikiwemo kupokea na kugawa misaada wakati wa maafa yametolewa katika ngazi za Wilaya na Mikoa katika Mikoa ya Mara, Geita, Singida, Simiyu, Shinyanga, Manyara, Kilimanjaro, Dodoma, Tabora na Arusha. Pia mipango ya kuijandaa kukabili maafa katika Halmashauri za Wilaya ya Maswa, Bariadi, Meatu, Mwanga na Same imandalishi. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itafanya tathmini ya maafa yanayoweza kutokea na uwezo wa kuyakabili pamoja na mipango ya kuijandaa kukabiliana na maafa katika Halmashauri za Wilaya ya Mtwara Mjini, Mtwara Vijijini, Masasi, Mvomero na Kilosa. Vilevile itaanza ujenzi wa Kituo cha Dharura cha Utendaji na Mawasiliano katika eneo la Mabwepande Wilayani Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudu kubwa zinazofanywa na Serikali dhidi ya uingizaji na utumiaji wa dawa za kulevyta, tatizo hili bado linaendelea kuwa kubwa kutokana na wanaojihusisha na dawa hizo kubuni mbinu mpya za kukwepa mkono wa Serikali. Katika mwaka 2013/2014, Serikali imetekeleza mapambano dhidi ya dawa hizo kwa kuelimisha umma kuhusu madhara ya dawa hizo. Serikali pia imepanua huduma za matibabu kwa watumiaji wa dawa za kulevyta kwa kutumia dawa ya methadone. Huduma za tiba hizo zinapatikana katika kliniki

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

zilizopo katika Hospitali za Muhimbili, Mwananyamala na Temeke. Vilevile, imeendesha operesheni zilizowezesha kilo 12,820 za mirungi kukamatwa, ekari 127 za mashamba ya bangi na kilo 3,445 za mbegu za bangi na magunia 1,107 ya bangi kavu kuteketezwa. Pia, kilo 236.5 za Heroin na kilo tatu za Cocaine zilikamatwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma na huduma za matibabu kwa watumiaji wa dawa za kulevyta. Serikali pia itaendelea kuwachukulia hatua kali wahalifu wote wanaojihusisha na biashara haramu ya dawa za kulevyta. Vilevile, ili kuondoa mianya inayojitokea katika kupambana na uhalifu utokanao na biashara ya dawa za kulevyta, Serikali itakamilisha kutunga Sheria mpya ya Kuzuia na Kupambana na dawa za kulevyta itakayowezesha kuimarisha mapambano dhidi ya tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali imeandaa Mpango Kazi wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira wa mwaka 2013 hadi 2018, utakaoziwezesha sekta zote kujumuisha masuala ya mazingira kwenye majukumu yao na mipango yao ya maendeleo. Sambamba na hatua hiyo, Serikali iliratibu utekelezaji wa miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabia nchi. Moja ya miradi hiyo ni Mradhi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi wenyewe thamani ya dola za Marekani milioni 2.5 unaofadhiliwa na Serikali ya Japan. Fedha hizo zimetumika kuanzisha miradi ya majaribio ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika Wilaya za Misenyi (Kagera), Mbanga (Ruvuma), Igunga (Tabora) na Zanzibar. Mradi mwingine ni mradi wa Vijiji vya Mfano wa Mazingira (ECO-Village) wenyewe thamani ya Euro milioni 2.2 unaofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya chini ya utaratibu ujulikano kama Climate Change Alliance Initiative. Hadi sasa mradi umeainisha vijiji vya mfano na kutekeleza miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika Mikoa ya Morogoro, Kigoma, Dodoma na Pemba. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea kutoa elimu ya hifadhi ya mazingira kwa umma kuhusu sera, sheria na Mikataba ya Kimataifa kuhusu mazingira pamoja na kuendelea kuhamasisha kampeni ya upandaji miti nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali imeanza kutekeleza Mkakati wa Tatoo wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI wa mwaka 2013 hadi 2018. Mkakati huo una shabaha ya kufikia malengo ya kimataifa ya Sifuri Tatoo, ikimaanisha kutokuwa na maambukizi mapya, kutokuwa na vifo vitokanavyo na UKIMWI na kuondokana kabisa na unyanyapaa na ubaguzi. Hadi Desemba 2013, kati ya watu 1,261,931 walioandikishwa kuwa wanaishi na VVU, watu 669,730 walianzishiwa dawa. Aidha, ili kurahisha upimaji wa VVU, Serikali imeipatia Mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Katavi na Rukwa mashine kubwa ya kupima kiwango cha kinga yaani CD4. Serikali pia imeidhinisha kuanzishwa kwa Mfuko wa UKIMWI utakaojulikana kama AIDS Trust Fund. Kuanzishwa kwa Mfuko huo kutawezesha kupunguza utegemezi wa wahisani kwenye shughuli za UKIMWI kwa wastani wa 40%.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea kuimarisha kampeni za uraghishaji zinazolenga mabadiliko ya tabia ili kuachana na mila na desturi hatarishi. Vilevile, Serikali imepanga kuimarisha kampeni za kinga kwa vijana wenyewe umri wa miaka kuanzia 15 hadi 24 dhidi ya maambuziki ya VVU kwa kutoa elimu. Juhudi zaidi zitaelekezwa kwenye Mikoa 10 yenye maambukizi zaidi ya wastani wa kitaifa wa 5.1%. Mikoa hiyo ni Njombe, Iringa, Mbeya, Shinyanga, Ruvuma, Dar es Salaam, Rukwa, Katavi, Pwani na Tabora. Aidha, Serikali itakamilisha maandalizi ya Sheria ya Mfuko wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu. Katika mwaka 2013/2014, Serikali imeendeleza miundombinu muhimu katika Manispaa ya Dodoma, ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 47.55 kwa kiwango cha lami katika maeneo ya Kisasa, Chang'ombe, Kikuyu, Area A pamoja na eneo la uwekezaji la Njedengwa umekamilika. Aidha, ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita 6.4 katika eneo la Nkuhungu na Mwangaza umekamilika. Serikali pia imefungua barabara zenye urefu wa kilomita 105 kwenye maeneo

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

yaliyopimwa ya Miganga, lyumbu na Ndachi. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itajenga mitaro ya maji ya mvua katika maeneo ya llazo, Kisasa na Ipagala na kupima viwanja vipyta 1850. Pia, Serikali itaandaa mpango wa matumizi ya ardhi katika maeneo ya Mkonze Mashariki, C-center, Nkuhungu na maeneo yanayozunguka Chuo Kikuu Cha Dodoma.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kwa muhtasari nimeelezea baadhi ya shughuli ambazo zimetekelizwa na Serikali katika mwaka 2013/2014. Nimetoa mwelekeo wa kazi zitakazotekelizwa katika mwaka 2014/2015. Kwa kuhitimisha, naomba tu kusisitiza yafuatayo:-

Moja, uchumi wetu unakua kwa kasi nzuri, kwa mfano katika mwaka 2011 ulikuwa kwa 6.4%, mwaka 2012 ulikuwa kwa 6.9% na mwaka 2013 ulikuwa kwa 7%. Ukuaji huu ni mkubwa ikililinganishwa na nchi nyingine za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ambapo wastani wa ukuaji wa uchumi kwa nchi hizo ulikuwa asilimia 4.6 mwaka 2011, asilimia 3.5 mwaka 2012 na asilimia 4.5 mwaka 2013. Takwimu zinaonesha pia kwamba kiwango cha ukuaji wa uchumi wa Tanzania ni cha juu ikililinganishwa na wastani wa ukuaji wa uchumi kwa nchi za Afrika Mashariki. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, uchumi wa Kenya ulikuwa kwa asilimia 4.4 mwaka 2011, asilimia 4.6 mwaka 2012 na asilimia 5.0 mwaka 2013. Uchumi wa Uganda ulikuwa kwa asilimia 6.6 mwaka 2011, asilimia 4.6 mwaka 2012 na asilimia 6.3 mwaka 2013. Takwimu hizo zinadhishirisha kwamba uchumi wetu unaendelea kuimarika ikililinganishwa na nchi nyingine, jambo tunalopaswa kujivunia wote. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, mabadiliko makubwa yanayoonekana nchini katika sekta za mawasiliano, ujenzi, viwanda na biashara ni matokeo ya ukuaji huu wa uchumi. Tunahitaji kufanya kazi tu kwa bidii na maarifa ili kuhakikisha kwamba ukuaji huu unakuwa endelevu na kuelekeza juhudhi zaidi katika sekta nyingine hasa kilimo, ufugaji na uvuvi kwani ndizo zinazotegemewa na Watanzania wengi. (Makofii)

Mbili, tumeadhimisha miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa amani na utulivu. Muungano huu ni wa kipekee na wa kupigiwa mfano duniani kote. Aidha, ni kielelezo kamili cha umoja, mshikamano na upendo mionganoni mwa wananchi, jambo liliowezesha kuwepo kwa amani na usalama. Muungano umetuletea maendeleo makubwa katika miaka 50 ya uhai wake, hivyo ni wajibu wetu kuuendeleza, kuuenzi, kuulinda na kuudumisha Muungano huu kwa nguvu zetu zote. (Makofii)

Tatu, tumeingia katika kipindi muhimu katika historia ya nchi yetu ambapo Bunge Maalum la Katiba limeanza mjadala wa kutunga Katiba. Ni matumaini yangu kuwa Bunge Maalum litakamilisha kazi ya kuandaa Rasimu ya tatu itakayopelekwa kwa wananchi kwa ajili ya kupigiwa kura ya maoni. Ninawashi wananchi wawe watulivu katika kipindi hiki maalum na kufuutilia kwa makini mjadala wa Katiba kwa kupima mawazo yanayotolewa wakati wa mjadala ili hatimaye kupiga kura ya maoni vema. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu kuwa Katiba mpya itakayopatikana itatusaidia kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa kupata muafaka wa kitaifa wa uendeshaji wa nchi yetu katika miaka mingi. Sote tumeshuhudia juhudhi za Serikali katika kuimarisha upatikanaji na usambazaji wa nishati nchini, mradi wa ujenzi wa kusafisha gesi asilia na bomba la kusafirisha gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam unaoendelea kujengwa utasaidia sana kuongeza umeme wa gharama nafuu kwenye gridi ya Taifa. Natoa wito kwa

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wananchi wote kushirikiana na Serikali kufanikisha miradi hiyo kwa kulinda miundombinu yake pamoja na kutumia fursa za kiuchumi zinazotokana na uwepo wa miradi hiyo. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu, nimwombe Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa atoe maelezo ya mapitio ya kazi zilizofanyika mwaka 2013/2014 na mwelekeo wa kazi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunivumilia kwa kipindi chote na ahsante sana. (Makof)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Hawa Ghasia nitakupa dakika 45.

### **MAELEZO YA WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU MAPITIO YA KAZI ILIZOTEKELEZWA MWAKA 2013/2014 NA MWELEKEO WA KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kuwasilisha majukumu ya kiutendaji ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kipindi cha mwaka 2013/2014 na mwelekeo wa Bajeti ya mwaka 2014/2015.

Katika kitabu cha maelezo yangu, aya ya pili, ukurasa wa pili hadi ukurasa wa nne nimeorodhesha majukumu ya kiutendaji ya ofisi yangu, mikoa na mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kuititia utekelezaji wa Program ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa imeendelea kugatua majukumu, fedha, watumishi na rasilimali nyingine kutoka Serikali kuu kwenda Serikali za Mitaa na kwenye ngazi za msingi.

Mheshimiwa Spika, kuititia program hii mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa fedha na mfumo wa usimamizi wa rasilimali watu umewekwa kwenye Halmashauri 133 na taratibu zinaendelea ili kuweka mifumo hiyo katika Halmashauri 34 mpya zilizoanzishwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali kuititia program ya maboresho katika sekta ya fedha awamu ya nne umefanya mapitio makubwa ya mfumo wa kuzipatia rukuzu ya maendeleo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili uendane na mahitaji yaliyopo sasa. Mapitio hayo yanahusu maeneo matatu yafuatayo: Mwongozo wa uendeshaji wa mfumo, mwongozo wa upimaji wa Halmashauri ili kupata ruzuku ya maendeleo na kuandaa utaratibu wa upimaji na tathmini ya mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zinazotawala uendeshaji wa demokrasia kwenye ngazi za vijiji, mitaa na vitongoji muda wa kukaa madarakani ni miaka mitano. Muda huo unamalizika mwezi Oktoba 2014 tangu viongozi wa vijiji, mitaa na vitongoji wa sasa walipochaguliwa mwaka 2009. Wakati utakapofika tutatoa taarifa rasmi ili kila mdau aweze kujandaa vema ili ashiriki kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2013/2014, shughuli za maandalizi zilizotekelzwa ni pamoja na maandalizi ya masanduku ya kupiga kura, kuititia kanuni za uchaguzi, kuandaa

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

fomu na nyaraka mbalimbali za uchaguzi na uhakiki wa Majimbo ya uchaguzi huo ambayo ni vijiji, mitaa na vitongoji. Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI inaratibu uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika ngazi za vijiji, mitaa na vitongoji ambapo mwaka 2014/2015 unatarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2014.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwaomba wadau wote wa uchaguzi, vyama vya siasa, Wabunge na wananchi kushiriki kikamilifu kwenye mchakato wa maandalizi na baadaye kushiriki kwenye upigaji wa kura ili tuwapate viongozi watakaosimamia shughuli za Serikali na kuimarisha demokrasia katika ngazi ya msingi.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha utumishi katika Serikali za Mitaa, mwaka 2013/2014, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara za kisekta imewapanga watumishi 43,279 ili waajiriwe na mamlaka za Serikali za Mitaa wakiwemo wa sekta ya elimu 36,338, kilimo 1,388, mifugo 953 na afya 4,600. Serikali imepanga kuajiri watumishi 6,340 zaidi wa sekta ya afya kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Halmashauri zinarudishiwa madaraka ya kuajiri watumishi wake na hivyo kuongeza uwajibikaji wa watumishi kwa Halmashauri zao, Serikali imekamilisha maandalizi hivyo kuanzia Julai 2014, Halmashauri zitaanza kuajiri watumishi wa kada za chini zilizoonyeshwa kwenye maelezo yangu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali ilianzisha maeneo mapya ya utawala ikiwemo Mikoa minne na Wilaya 19. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali ilitenga shilingi bilioni 18 kwa ajili ya ujenzi na makazi. Ujenzi wa majengo hayo unatekelezwa na Wakala wa Majengo ya Serikali (TBA) na kusimamiwa kwa karibu na Mikoa yenye na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya uendelezaji wa maeneo mapya hadi hapo kazi ya ujenzi itakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya mipaka katika maeneo mbalimbali imeendelea kujitokeza hapa nchini kutokana na kutokuwepo kwa tafsiri sahihi ya mipaka baina ya maeneo ya utawala kama ilivyo kwenye matangazo ya Serikali yaliyoanzisha maeneo husika. Serikali imekwishaagiza Mikoa, Halmashauri, Tarafa, Kata na Vijiji kutekeleza wajibu wao kwa kushughulikia migogoro ya mipaka na kupatiwa ufumbuzi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu. Aidha, maamuzi yanayofikiwa katika vikao halali vya utatuzi wa migogoro hiyo yaheshimiwe na kutekelezwa na kila upande.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na ongezeko la makusanyo ya mapato katika mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka vyanzo vya ndani kwa miaka minne mfululizo kuanzia 2010/2011 hadi 2013/2014 kama inavyoelezwa katika aya ya 13 ya maelezo yangu.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri 20 zilizofanya vizuri katika makusanyo ya mapato ya ndani ikilinganishwa na makadirio katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo imeonyeshwa katika Jedwali Na.1 ambapo Halmashauri 20 zilizofanya vizuri, kwa Halmashauri za Wilaya ni Muheza, Kilwa, Sikunge, Urambo, Tabora DC, Hai, Manyoni, Nzega, Kilombero na Mpanda. Kwa upande wa Miji ni Kibaha na Njombe. Kwa Manispaa za Dar es Salaam ni Temeke na Kinondoni. Kwa Manispaa nydingine ni Iringa Manispaa, Lindi, Moshi na Mtwara. Kwa upande wa Majiji ni Jiji la Dar es salaam na Arusha. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ambazo zimefanya vibaya au ambazo hazikukusanya vizuri ni Morogoro, Monduli, Kilindi, Chato, Ngorongoro, Mpwapwa, Longido, Handeni, Chamwino na ya mwisho kabisa katika makusanyo kwa upande wa Halmashauri ni Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ambayo imekusanya wastani wa asilimia 23.07. Kwa upande wa miji ni Mji

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wa Mpanda na Babati ndiyo ambayo imekusanya kwa kweli kidogo ukilinganisha na miji mingine. Kwa upande wa Manispaa ni Dodoma, Musoma, Singida, Tabora na Sumbawanga. Kwa upande wa Majiji, Jiji ambalo limekusanya chini ya asilimia 40 ni Jiji la Mbeya. Majiji mengine ambayo hayakufanya vizuri ni Mwanza na Tanga.

Mheshimiwa Spika, katika suala la ukusanyaji wa mapato kwa mwaka 2014/2015, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekadiria kukusanya shilingi bilioni 457.8 kutokana na vyanzo vyake vya ndani. Kiasi hiki ni ongezeko la asilimia 23 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2013/2014. Ili kufanikisha lengo hili, hatua mbalimbali zinachukuliwa na Serikali ili kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato hayo kama ilivyoelezwa katika aya ya 15 na ukurasa wa 16 wa maelezo yangu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI inalo jukumu la kuhakikisha kuwa miji ya Tanzania inakuwa na maendeleo endelevu kupitia miradi ya Tanzania *Strategic Cities* na *Urban Local Government Strengthening*. Wizara yangu itaendelea kuboresha miundombinu ya mjni na uimarishaji wa uwezo wa Halmashauri kusimamia vema mapato yao ya ndani. Jukumu hili nimelieleza katika aya ya 17 hadi aya ya 23 ya maelezo yangu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ilifanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi iliyobiuliwa kuendeleza Jiji la Dar es Salaam. Changamoto zilizopo katika ukuaji wa Jiji la Dar es Salaam ni kuongezeka kwa taka ngumu, ujenzi holela wa makazi, usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zote nne za Mkoa wa Dar es Salaam zimehusika katika kutayarisha mapendekezo ya miradi ya kipaumbele itakayotekerezwa kwa kushirikisha wananchi na sekta binafsi. Miradi saba iliyobiuliwa ni ujenzi na ukarabati wa barabara za mitaa zitakazounganishwa na barabara kuu ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka, kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na utupaji wa taka ngumu na miradi ya ubunifu ya ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi. Vilevile miradi mingine ni pamoja na kuimarisha usafiri wa reli na majini, kuboresha mfumo na miundombinu ya taasisi, ukarabati na ujenzi wa mifumo ya maji ya mvua na uboreshaji wa makazi holela. Kazi hii inatarajiwaa kukamilika katika mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2014, watoto 1,261,476 wenyewe umri wa kwenda shule walitarajija kuandikishwa darasa la kwanza ambapo walioandikishwa ni 1,166,497 sawa na asilimia 92.5.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa katika ngazi ya elimu ya sekondari, shule 1,200 za sekondari zinaimarisha miundombinu yake. Shule 264 kati ya hizo zikiwemo shule mbili kila Halmashauri 132 zilipelekewa jumla ya shilingi bilioni 56. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 30 zimetolewa na Serikali ya Tanzania na shilingi bilioni 26 zimetolewa na Benki ya Dunia. Upembuzi yakinifu unaendelea ili kuendelea na ukarabati na ujenzi wa shule 936 zilizobaki.

Mheshimiwa Spika, katika masuala la michezo napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA itafanyika Julai, 2014 mjni Kibaha kama ilivyopangwa. Naomba kutoa taarifa kwamba mwaka 2014, Tanzania imepewa heshima ya kuwa mwenyeji

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wa Mashindano ya Umoja wa Michezo ya Sekondari katika Jumuia ya Afrika Mashariki. Michezo hiyo itafanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Oktoba, 2014.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, Serikali ilianzisha Mpango wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa katika sekta saba ikiwemo sekta ya elimu. Kupitia mpango huu sekta ya elimu inatekeleza mikakati tisa ifuatayo ikiwemo sita inayoteklezwa na TAMISEMI ambayo ni upangaji wa shule kwa ufaulu, motisha kwa shule zilizofanya vizuri, usambazaji wa vitabu, kitabu cha uongozi wa shule, ufundishaji wa kusoma, kuandika na kuhesabu, ufundishaji rekebishi kwa wanafunzi wa shule za msingi, ufundishaji rekebishi kwa wanafunzi wa shule za sekondari, motisha kwa Walimu, ujenzi wa shule na ruzuku ya uendeshaji kwa shule.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI inatambua changamoto ya madeni ya Walimu na watumishi wengine katika mamlaka za Serikali za Mitaa. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali imeweka mikakati mbalimbali kudhibiti madeni yasiyohusiana na mishahara ikiwa ni pamoja na kutenga fedha za likizo, matibabu, uhamisho na mafunzo, kutohamisha walimu iwapo hakuna fedha, kulipa fedha za likizo na uhamisho zinazopelekwa kwenye Halmashauri kupitia fedha za matumizi mengineyo. Kwa madeni yanayohusiana na mishahara, Serikali inatumia mfumo wa LAWSON kulipa madeni ya mishahara moja kwa moja kupitia mishahara ya mtumishi husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inaendelea kuhakiki na kulipa madeni ya watumishi wote wakiwemo Walimu yanayohusiana na mishahara kila hali ya fedha inaporuhusu. Hadi Februari 2014 shilingi bilioni 19 sawa na asilimia 31 ya madeni ya mishahara yaliyopokelewa yamelipwa na mchanganuo unaonekana katika Jedwali Na.3.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kujenga hospitali mpya na kuzifanya ukarabati hospitali za Mikoa ambazo sasa zinakuwa za rufaa kwa lengo la kuboresha huduma ya afya kote nchini. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali ilitenga shilingi bilioni 2.95 kwa ajili ya ukarabati na shilingi bilioni 8.46 kwa ajili ya ujenzi. Katika mwaka huo pia Serikali kwa kushirikiana na wadau wa Mfuko wa Maendeleo ya Afya ilitenga shilingi bilioni 87 kwa ajili ya Halmashauri na shilingi bilioni 3.7 kwa ajili ya Mikoa ili kuongeza dawa na vifaa tiba, kuboresha mifumo ya kutolea huduma za afya, mafunzo na uendeshaji wa ofisi. Utekelezaji wa kazi za ujenzi pamoja na masuala mengine ya afya umeelezwa vema katika aya ya 34 hadi 38 ya maelezo yangu.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza huduma ya TEHAMA, watalaam katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wameongezeka kutoka 76 mwaka 2012/2013 hadi 133 mwaka 2013/2014. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imewezesha utengenezaji wa tovuti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa saba iliyo chini ya Mradi wa Uendelezaji Miji ya Kimkakati. Aidha, ofisi imetengeneza mfumo wa kielectroniki wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa unaojulikana kama *Local Government Revenue Collection Information Systems* ambao umefanyiwa majaribio katika Jiji la Arusha na kuonyesha mafanikio makubwa katika kuongeza ukusanyaji wa mapato. Lengo kuu ni kuweka mfumo huu katika Halmashauri zote 164 kwa awamu kwa kuanzia mwaka wa fedha 2014/2015.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya TEHAMA inayozunganganisha Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa katika computer kuu (server) Dodoma ilitumia aina nne za teknolojia ambazo ni; mkongo, broadband radio, satellite na nyaya za shaba. Dhamira ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni kuongeza ufanisi kwa kuziunganisha Halmashauri zote kwenye Mkongo wa Taifa katika mwaka 2014/2015. Maelezo ya zaidi kuhusu TEHAMA yanaonekana katika aya ya 36 hadi 43 ya maelezo yangu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, shilingi bilioni 151.3 kutoka Mfuko wa Barabara zilitengwa kwa ajili ya matengenezo, ukarabati na ujenzi wa barabara na madaraja. Hadi kufikia Machi 2014 jumla ya shilingi bilioni 135.9 zilikuwa zimepokelewa na kupelekwa Halmashauri ambapo shilingi bilioni 55.5 zilikuwa zimetumika katika kukamilisha utekelezaji wa Mpango Kazi wa mwaka 2012/2013 na shilingi bilioni 80.4 kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa mwaka 2013/2014. Hadi kufikia Desemba kazi zilizofanyika katika kipindi hicho ni kama inavyoonekana katika aya ya 44 ya maelezo yangu.

Mheshimiwa Spika, katika azma ya kuhakikisha kuwa barabara za vijiji zinaendelea kuboreshwa. Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMESEMI kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wakiwemo EU, USAID na DFID katika mwaka wa fedha 2013/2014, itatekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara ikiwa ni pamoja na kutengeneza madaraja katika baadhi ya Halmashauri nchini kama nilivyoeleza katika maelezo yangu aya ya 46 hadi aya ya 49.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Halmashauri zilitengewa jumla ya shilingi bilioni 67.9 kwa ajili ya utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs). Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 35.3 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya uwekezaji ambayo haikukamilika katika kipindi cha utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi wa ASDP. Shilingi bilioni 16.4 ni kwa ajili ya kuboresha huduma za ugani na shilingi bilioni 16.2 ni kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 2014 shilingi bilioni 37.2 zilikuwa zimepelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 16 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kuimarisha huduma za ugani kama nilivyoeleza katika aya ya 52 hadi aya ya 53 ya maelezo yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la migogoro, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imechukua hatua ya kufuatilia migogoro ya wakulima na wafugaji na kubaini kuwa chanzo cha migogoro hiyo ni kukosekana kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji, mabadiiliko ya tabianchi yanayosababisha kuwepo kwa ukame na hivyo kuwafanya wafugaji kuhama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, baadhi ya wakulima na wafugaji kutotii sheria kwenye vijiji vyenye mipango bora ya ardhi na baadhi ya viongozi kwenye ngazi mbalimbali kutuhumiwa kupokea rushwa na kuwaruhusu wakulima au wafugaji kulima au kufuga kwenye maeneo yasiyoruhusiwa.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ni kuhimiza kuwepo kwa mipango bora ya ardhi kwenye maeneo ya vijiji, kuweka juhudzi za makusudi za kuwashimiza wananchi kuzingatia sheria zilizowekwa kuhusu mipango ya matumizi ya ardhi na kuwashukulia hatua za kinidhamu na kisheria viongozi wanaothibitika kupokea rushwa.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, shilingi milioni 851 zilipelekwa kwenye Halmashauri 65 na shilingi 42,500,000 katika Sekretarieti za Mikoa 17 zinazotekeleza mkakati wa kufufua na kuendeleza viwanda vya ngozi. Hadi kufikia Januari 2014, utekelezaji ulifanyika kama ilivyoelezwa katika kitabu cha maelezo yangu aya ya 57 hadi 58.

Mheshimiwa Spika, nimetoa pia maelezo ya utekelezaji wa Programu ya Maji Vijijini pamoja na Programu ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu kama inavyojeleza katika aya ya 59 hadi aya ya 61 ya maelezo yangu.

Mheshimiwea Spika, katika mwaka 2013/2014, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imeshughulikia urekebishaji wa muundo wake ili uweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Lengo ni kuwa chombo kinachojitegemea na chenye uwezo wa kutoa mikopo zaidi kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Wizara inaendelea na maandalizi muhimu ili kukamilisha taratibu zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kutafuta fedha za mtaji. Maelezo zaidi kuhusu Bodi hiyo yako katika aya ya 62 hadi aya ya 64 ya maelezo yangu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa umeandikisha wanachama 24,740 na kufanya idadi ya wanachama kuongezeka kutoka 104,840 Juni 2013 na kufikia 141,702 Machi 2014. Mfuko pia umekusanya jumla ya shilingi bilioni 387.44 kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na michango ya wanachama, mapato kutokana na vitega uchumi na marejesho ya vitega uchumi vilivyoiva.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Mfuko utaendelea kulipa mafao na pensheni za Wastaifu kila mwezi kwa mujibu wa sharia. Matarajio ya Mfuko ni kuongeza thamani ya rasilimali zake kutoka shilingi bilioni 789.84 za sasa hadi shilingi bilioni 971.5 ifikapo Juni 2015. Ongezeko hili ni pamoja na jengo la Kitega Uchumi linalojengwa kwa ubia na Jiji la Mwanza ambalo ujenzi wake unatarajia kukamilika na kuanza kupangishwa mwezi Augosti 2014. Miradi mingine inayotekeliza na Mfuko imeelezwa katika aya ya 65 hadi aya ya 66 ya maelezo yangu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Elimu Kibaha limeendelea kutimiza malengo ya kuanzishwa kwake ya kupambana na maadui ujinga, umaskini na maradhi. Ili kutimiza malengo hayo, Shirika limetumia rasiliamali na vitendea kazi vyake kwa ufanisi na hivyo kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, Shirika liliendelea kutekeleza majukumu yake kama ilivyopanga. Shughuli zilizotekeliza na Shirika na kazi zilizopangwa kutekeleza na Shirika nimezieleza katika aya ya 66 hadi 72 ya maelezo yangu.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kimeendelea na mpango wake wa kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika ngazi ya na Astashahda na Stashahada. Chuo pia kimeimarisha uwezo wake kwa kushirikiana na Taasisi zingine zikiwemo Shirika la Maendeleo la Japan (JICA), Taasisi ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa Korea ya Kusini na Shirika la Maendeleo la Ubelgiji.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Chuo kilidahili wanafunzi wapya 1623 kwa kozi nane na kufikisha jumla ya wanafunzi 2547. Vilevile Chuo kiliendesha mafunzo ya muda mfupi kwa wanachuo na Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wapatao 474. Kazi nyine zilizotekelawa na zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2014/2015, zimeelezwa katika aya ya 73 hadi 79 ya maelezo yangu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wakala wa Usafiri wa Haraka uliendelea na ujenzi wa barabara zenyet urenfu wa kilomita 20.9 sanjari na ujenzi wa awamu ya kwanza. Wakala hivi sasa unaendelea na ukamilishaji wa usanifu wa kina wa mfumo wa DART awamu ya pili na ya tatu zitakazokuwa na urenfu wa kilomita 42.3.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa vituo vikubwa vitano katika maeneo ya Kimara, Ubungo, Morroco, Kariakoo na Kivukoni unaendelea. Kituo kikuu cha mabasi Kivukoni kimekamilika kwa 95% na kipo katika hatau za mwisho za marekebisho. Vituo vya Ubungo, Kimara, Morocco na Kariakoo ujenzi unaendelea sambamba na ujenzi wa barabara. Aidha, ujenzi wa vituo vidogo 27 kwa ajili ya kuhudumia mabasi 65 kwa sasa kwa kila mwelekeo unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika mwaka 2014/2015 imeelezwa vyema katika aya ya 89 iliyoko katika ukurasa wa 64 hadi 68. Baadhi ya kazi muhimu zitakazotekelawa ni pamoja na kuziwezesha Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa kuzingatia dhana ya upelekaji madaraka kwa umma, kufanya ufuatiliaji na fathmini ya utekelezaji wa shuguhuli mbalimbali Mikoa na kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuratibu na kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kuratibu shughuli za usimamizi na uendeshaji wa elimu ya msingi na sekondari. Kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni kama zinavyoonekana kwenye kitabu cha maelezo yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, kwa miongozo na maelekezo yake ya mara kwa mara ambayo mara zote yamerahisisha utekelezaji wa majukumu yangu. Majukumu yote niliyoyaeleza yametekelezwa kwa ushirikiano wa hali ya juu na viongozi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Taasisi zake. Napenda kuwashukuru kwa juhudhi zao kubwa wanazozionyesha katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa.

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu za pekee ninazielekeza kwa Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwa ushirikiano na ushauri wao wanaonipa wakati wote. Aidha, napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu Bwana Jumanne Sagini, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara, Vitengo, Wakuu wa Taasisi na watumishi wote kwa pamoja na mshikamano wao katika kutekeleza majukumu na kazi za Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa miongozo yao ambayo kwa aina ya pekee imesaidia sana katika kuboresha utendaji wa Ofisi yetu. Vilevile nikushukuru Mheshimiwa Spika na Wabunge wote kwa ushirikiano wenu hapa Bungeni. (Makof)

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wote wa Jimbo la Mtwara Vijijiini kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Aidha, kwa namna ya pekee ninaishukuru familia yangu kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imejipanga kusimamia utekelezaji wa dhana ya utawala bora, Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (*D by D*) na usimamizi wa Rasiliamali watu na fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI itaendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Taasisi zake katika kuleta tija na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kushirikiana kwa karibu na Halmashauri zao katika kusimamia ukusanyaji wa mapato, matumizi ya rasilimali na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuwawezesha wananchi kupata huduma bora za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (Makofii)

**SPIKA:** Mawaziri wengine msije mkarudia habari ya kuwashukuru watu. Kwa mujibu wa Kanuni zetu, hatupotezi muda kwa kuwashukuru, wako kazini na sisi wote tuko kazini.

### **MAELEZO YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU MAPITIO YA KAZI ZILIZOTEKELEZWA MWAKA 2013/2014 NA MWELEKEO WA KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kuwepo katika Bunge lako Tukufu nikiwa mwenye afya njema. Naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Hotuba nzuri iliyotoa mwelekeo na malengo ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2014/2015. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano wao katika kuongoza eneo hili la Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. OWM-TAMISEMI itaendelea kuzingatia ushauri na maelekezo ya Kamati kwa lengo la kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi.

2. **Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba sasa kuwasilisha majukumu ya kiutendaji ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI), katika kipindi cha mwaka 2013/2014 na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka 2014/2015.

#### **Majukumu ya Kiutendaji:**

3. **Mheshimiwa Spika**, ili kufanikisha majukumu ya Kisera Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inatekeleza majukumu ya kiutendaji yafuatayo:-

- (i) Kuratibu utekelezaji wa upolekaji Madaraka kwa Umma (*D by D*);
- (ii) Kuratibu na kusimamia Tawala za Mikoa ili ziweze kuziwezesha Halmashauri katika kutekeleza wajibu wake;
- (iii) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Vijijiini na Mkakati wake;
- (iv) Kusimamia Wakala wa Usafiri wa Haraka katika Jiji la Dar es Salaam na Taasisi nyingine;

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(v) Kuratibu usimamizi na uendeshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari nchini kuitia Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

(vi) Kusimamia utekelezaji wa Programu na miradi iliyopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mikoa majukumu yao ni pamoja na:-

(i) Kusimamia na kuratibu shughuli zote za maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Mkoa husika;

(ii) Kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

(iii) Kuhakikisha kwamba kunakuwepo amani na utulivu katika Mikoa;

(iv) Kufuutilia utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali zinazotekelwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(v) Kuratibu usimamizi na uendeshaji wa elimu ya msingi na sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizo katika Mkoa husika; na

(vi) Kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora.

**Mheshimiwa Spika**, utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, unaongozwa na majukumu ya msingi yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha kuwa kunakuwepo na amani na utulivu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(ii) Kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora;

(iii) Kuhakikisha kuwa Serikali za Mitaa zinatoa huduma za kuridhisha na kuaminika, katika wakati muafaka na zenyе ubora kwa wananchi;

(iv) Kuhakikisha kuwa zinasimamia vema utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na kusimamia matumizi ya fedha zinazopelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(v) Kuwaunganisha wadau wote wa maendeleo walioko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kutumia vema rasilimali watu na fedha kwa manufaa ya Jamii iliyopo katika Mamlaka hizo.

**UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA 2013/2014 NA MWELEKEO WA BAJETI YA MWAKA 2014/2015**

### Utawala Bora

**4. Mheshimiwa Spika**, OWM-TAMISEMI inasimamia utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (Decentralization by Devolution) kwa lengo la kupunguza umaskini kwa kuimarisha huduma za jamii na utawala bora katika ngazi ya Serikali za Mitaa. Sera hii inatekelezwa kuititia Programu ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa.

**5. Mheshimiwa Spika**, OWM-TAMISEMI kuititia utekelezaji wa Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa imeendelea kugatua majukumu kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa na kutoka ngazi za juu za Serikali za Mitaa kwenda ngazi za msingi za Serikali za Mitaa. Aidha, Serikali imeendelea kugatua rasilimali fedha, rasilimali watu na vitendea kazi ili kuziwezesha mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**6. Mheshimiwa Spika**, katika Programu hii, Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Fedha (*Intergrated Financial Management System/Epicor*) umewekwa kwenye Halmashauri 133 na taratibu zinaendelea ili kuweka mfumo huo katika Halmashauri 34 mpya zilizoanza mwaka 2012. Kwa sasa, OWM – TAMISEMI ina uwezo wa kuona na kufuatilia taarifa za malipo mbalimbali yanayofanyika katika ngazi za Halmashauri. Aidha, Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Rasilimali Watu (*Local Government Human Resource Management Information System - LGRHS*) umewekwa ili kurahisisha usimamizi na utunzaji wa kumbukumbu za rasilimali watu.

**7. Mheshimiwa Spika**, katika utawala bora suala la usimamizi wa fedha ni muhimu ikizingatiwa kuwa fedha za ruzuku ya maendeleo zimekuwa zikipelekwa katika Halmashauri kwa kutumia vigezo maalum. Katika mwaka 2013/2014 Serikali kuititia maboresho katika Sekta ya fedha awamu ya nne chini ya Wizara ya Fedha, imefanya mapitio katika fomula zinazotumika katika migao ya fedha ili kuzingatia zaidi mgawanyo wa rasilimali ndani ya Halmashauri husika na kati ya Halmashauri moja na nyininge. Aidha, OWMTAMISEMI imeanza mchakato wa kufanya mapitio makubwa ya mfumo wa kuzipatia ruzuku ya maendeleo Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGDG) ili uendane na mahitaji yaliyopo sasa. Mapitio hayo yamekwishaanza katika maeneo matatu yafuatayo: Mwongozo wa Uendeshaji wa Mfumo; Mwongozo wa Upimaji wa Halmashauri ili kupata Ruzuku ya Maendeleo; na kuandaa Utaratibu wa Upimaji na tathmini ya mfumo huo. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2014/2015 kazi ya kufanya mapitio na kuandaa mfumo mpya itaendelea.

### Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

**8. Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zinazotawala uendeshai wa demokrasia kwenye ngazi za Vijiji, Mitaa na Vitongoji, muda wa kukaa madarakani ni miaka mitano. Muda huo unamalizika mwezi Oktoba mwaka 2014 tangu walipochaguliwa viongozi wa sasa mwaka 2009. Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI inaratibu uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika ngazi za Vijiji, Mitaa na Vitongoji ambapo kwa mwaka 2014/2015 unatarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2014. Kwa mwaka 2013/2014 shilingi **bilion 5** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maandalizi. Shughuli zinazotekelezwa ni pamoja na:- Maandalizi ya masanduku ya kupigia kura, kuititia kanuni za uchaguzi, kuandaa fomu na nyaraka mbalimbali za uchaguzi, na uhakiki wa majimbo ya uchaguzi huu ambayo ni vijiji, mitaa na vitongoji.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kuwaomba wadau wote wa uchaguzi (vyama vya siasa, wabunge na wananchi) kushiriki kikamilifu kwenye mchakato wa maandalizi na baadaye kushiriki kwenye upigaji kura ili tuwapate viongozi watakaosimamia shughuli za Serikali na kuimarisha demokrasia katika ngazi za msingi.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

### **Watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa:-**

9. **Mheshimiwa Spika**, ili kuboresha utumishi katika Serikali za Mitaa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta imeendelea kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakuwa na watumishi wa kutosha, wenyе sifa za kitaaluma ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Hivyo, katika mwaka wa 2013/2014 watumishi 43,279 wameajiriwa katika Sekta za Elimu 36,338, kilimo 1,388 mifugo 953 na Afya watumishi 4,600. Serikali imepanga kuajiri watumishi 6,340 zaidi wa sekta ya afya kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha.

10. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa Halmashauri zinarudishiwa madaraka ya kuajiri watumishi wake na hivyo kuongeza uwajibikaji wa watumishi kwa Halmashauri zao, mwaka 2013 Bunge lilifanya marekibisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 8/2002 ili kuruhusu ajira ya kada 22 za chini zifanywe na Halmashauri. Kada hizo ni Mchapa Hati II, Msaidizi wa Maktaba II, Mkaguzi wa Mji II, Muandazi Waiter II, Mhudumu Jikoni, Maendeleo ya Jamii Msaidizi III, Dereva II, Dereva Mitambo II, Katibu Mahususi III, Msaidizi wa Kumbukumbu II, Mapokezi, Msaidizi wa Ofisi, Mlinzi, Fundi Sanifu Msaidizi, Afisa Mtendaji Kijiji III, Afisa Mtendaji Mtaa II, Afisa Mtendaji Mtaa III, Mlezi wa Watoto Msaidizi, Nahodha II, Polisi Msaidizi, Mhudumu wa Boti II, Muundaji wa Boti II. Maandalizi ya kugatua madaraka hayo yamekamilika na kuanzia Julai, 2014 Halmashauri zitaanza kuajiri watumishi wa kada hizo.

### **Uendelezaji wa Maeneo Mapya ya Utawala**

11. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Serikali ilianzisha maeneo mapya ya utawala ikiwemo Mikoa minne (4) na Wilaya kumi na tisa (19). Taratibu za uanzishwaji wa maeneo haya zilikamilika na Mikoa hii ilikwishaanza rasmi. Kazi inayoendelea ni uendelezaji wa maeneo haya kwa maana ya ujenzi wa majengo yanayotakiwa, kuajiri watumishi wa kutosha na kuweka vitendea kazi. Katika mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali ilitenga **shilingi bilioni 18** kwa ajili ya ujenzi wa Makazi. Ujenzi wa majengo hayo unatekelezwa na Wakala wa Majengo ya Serikali (TBA) na kusimamiwa kwa karibu na Mikoa yenye na OWM-TAMISEMI. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 jumla ya **shilingi bilioni 9.5** zimetengwa kuendeleza ujenzi huo. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya uendelezaji wa maeneo mapya hadi hapo kazi ya ujenzi itakapokamilika.

### **Utatuzi wa Migogoro ya Mipaka**

12. **Mheshimiwa Spika**, migogoro ya mipaka katika maeneo mbalimbali imeendelea kujitokeza hapa nchini. Migogoro hiyo inajitokeza kati ya Mikoa na Mikoa, Wilaya na Wilaya, Tarafa na Tarafa, Kata na Kata na Kijiji na Kijiji. Mingi ya migogoro hiyo husababishwa na kutokuwepo kwa tafsiri sahihi ya mipaka baina ya maeneo ya utawala kama ilivyo kwenye matangazo ya Serikali yaliyoanzisha maeneo husika. Serikali katika kuhakikisha migogoro hiyo hajitokezi imeziagiza mamlaka za kiutawala katika ngazi ya Mikoa, Halmashauri, Tarafa, Kata na Kijiji zitekeleze wajibu wao kwa kuhakikisha kuwa masuala yanayohusiana na migogoro ya mipaka yanashughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu na wazingatie maamuzi yanayofikiwa katika vikao halali vya utatuzi. Aidha, OWM -TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeanza kuhakiki mipaka ya Halmashauri na Wilaya zote nchini ili kurekebisha matatizo ya mipaka yaliyobainishwa.

### **Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa**

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

13. **Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na ongezeko la makusanyo ya mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka vyanzo vya ndani (Own Sources) kwa miaka mine mfululizo kuanzia mwaka 2010/2011. Katika mwaka 2010/2011 makisio yalikuwa **shilingi bilioni 173.1** na makusanyo halisi yalikuwa **shilingi bilioni 158.3** sawa na asilimia **92** ya makadirio. Mwaka 2011/2012 makadirio yalikuwa **shilingi bilioni 310.96** makusanyo **shilingi bilioni 195.52** sawa na asilimia **62.9** ya makadirio, mwaka 2012/2013 makadirio yalikuwa **shilingi bilioni 324.4** makusanyo yakawa **shilingi bilioni 240.9** sawa na asilimia **73.4** ya makadirio. Mwaka 2013/2014 makadirio yalikuwa **shilingi bilioni 370.6** na hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014 mapato yaliyokwisha kukusanya ni **shilingi bilioni 192.1** sawa na asilimia **52 ya** makadirio. Mtiririko huu unaonesha kuwa makadirio ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa mwaka 2012/2013 yameongezeka kwa **shilingi bilioni 197.5** sawa na asilimia **150.8** yakilinganishwa na yale ya mwaka 2009/2010; wakati makusanyo halisi yameongezeka kwa **shilingi bilioni 123.1** sawa na asilimia **104.5**. Hali hii inaonesha kuwa bado kuna fursa ya kuongeza mapato ya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika Jedwali Na 1 zimeonyeshwa Halmashauri ishirini zilizofanya vizuri katika makusanyo ya mapato ya ndani ikilinganishwa na makadirio katika kipindi cha miaka mitatu ya 2011/2012 hadi 2013/2014.

**Jedwali 1: Halmashauri 20 Zilizofanya Vizuri Katika Makusanyo ya Mapato ya Ndani Ikilinganishwa na Makadirio kwa Wastani wa Miaka Mitatu**

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Uchambuzi wa takwimu za Jedwali Na. 1 unaonesha kuwa Halmashauri hizi ziliweza kuvuka asilimia 50 ya malengo yao ya ukusanyaji. Aidha, ipo haja ya kuimarisha ukadiriaji wa malengo ya ukusanyaji hasa kwa Halmashauri zilizozidi asilimia 100.

Jedwali Na. 2 linabainisha Halmashauri ishirini ambazo hazikufanya vema katika ukusanyaji wa mapato yao ya ndani

### **Jedwali 2: Halmashauri 20 Zilizofanya Vibaya Katika Makusanyo ya Mapato ya Ndani Ikilinganishwa na Makadirio kwa Wastani wa Miaka Mitatu**

14. **Mheshimiwa Spika**, katika suala la ukusanyaji wa mapato, Halmashauri zimekuwa na changamoto mbalimbali zikiwemo zinazohusiana na mkinzano wa sheria, għarama katika kutengeneza mifumo bora ya ukusanyaji wa mapato na nyingine za kiusimamizi. Pamoja na changamoto hisz, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekadiria kukusanya **shilingi bilioni 457.8** kutomha na vyanzo vyake vyāni. Kiasi hiki ni ongezeko la asilimia 23 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2013/2014. Ili kufanikisha lengo hili, hatua mbalimbali zimechukuliwa na zinaendelea kuchukuliwa na Serikali ili kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato hayo.

15. **Mheshimiwa Spika**, Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kupitja Sheria ya Serikali za Mitaa Sura 290 ili iweze kuzipa Halmashauri uwezo wa kutunga Sheria Ndogo za ukusanyaji wa

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

mapato. Mapitio hayo yatazingatia urahisi wa usimamizi wa ukusanyaji kodi, ushuru na ada mbalimbali ambapo mchakato umekwishaanza. Jitihada zingine zitaangalia njia nyepesi na rahisi za malipo zinazotumia teknolojia ya habari na mawasiliano ili kupunguza kero zikiwemo umbali kwa walipaji na kuongeza tija katika ukusanyaji wa mapato. Aidha, utafiti wa vyanzo vya mapato umefanyika katika Halmashauri 30 na matokeo yake yatasaidia kubuni vyanzo vipyta vya mapato kwa kuzingatia fursa na uwezo wa kiuchumi wa kila Halmashauri. Baadhi ya vyanzo vipyta vinavyoangaliwa ni kodi ya majengo kwa Halmashauri za Wilaya, ushuru wa mifugo, ushuru wa minara ya simu na ushuru wa nyumba za kulala wageni uliofutwa katika Sheria ya Utalii ya mwaka 2011.

16. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2014/2015 kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kwa kuanzia tutaweka mfumo wa i-TAX katika Halmashauri za Wilaya katika Mikoa kumi (10) ili kurahisisha ukusanyaji, utunzaji kumbukumbu za walipakodi na utoaji wa taarifa sahihi za ukusanyaji wa mapato kwa wakati. Mafunzo yatatolewa kwa watumishi wa ngazi zote za usimamizi katika kuongeza uwezo wa kuandaa mipango na kukadiria vyanzo vya ndani vya Halmashauri kulingana na hali ya uchumi wa eneo husika. Aidha, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Manunuvi ya Umma (PPRA) unafanyika utafiti wa vyanzo vya mapato ambavyo ukusanyaji wake umebinafsishwa ili kupata namna bora ya kuziwezesha Halmashauri kubinafsisha bila ya kuwa na shaka (risk) ya kupotea kwa mapato. Baada ya utafiti huo kukamilika Serikali itaandaa mwongozo rahisi wa kuziwezesha Halmashauri kusimamia vizuri vyanzo vya mapato ya ndani ambavyo ukusanyaji wake umebinafsishwa.

### Usimamizi wa Maendeleo Mijini

17. **Mheshimiwa Spika**, OWM-TAMISEMI inalo jukumu la kuhakikisha kuwa Miji ya Tanzania inakuwa na maendeleo endelevu. Katika kipindi cha 2013/2014 ufuatiliaji umefanyika katika maeneo 17 yanayojumuisha Miji, Mamlaka za Miji Midogo na Miji inayochipukia ili kutambua hali halisi ya ukuaji na uendelezaji wa Miji hiyo na changamoto ambazo ni kikwazo katika uendelezaji wake. Changamoto zilizobainishwa ni pamoja na upungufu wa wataalam wa sekta ya ardhi, ukosefu wa mipango kabambe ya uendelezaji miji, ofisi, vitendea kazi na ufinyu wa bajeti. Hata hivyo miji midogo ina fursa ya uwepo wa ardhi kwa ajili ya maandalizi ya matumizi bora ya ardhi ili kuharakisha maendeleo. Utambuzi huo ukikamilika utasaidia kuandaa mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo ili kuiwezesha miji kukua na kuendelezwa kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu.

18. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014 mchakato wa kuboresha mfumo wa utoaji wa vibali vya ujenzi na ukaguzi wa majengo yanayojengwa mijini umeanza ili kuhakikisha usalama wake hususan majengo ya ghorofa. Ufuatiliaji umefanyika katika Halmashauri za Miji yote ili kupata taarifa sahihi za utoaji wa vibali vya ujenzi na usalama wa majengo. Aidha, taasisi ambazo zinapewa dhamana ya kusimamia ujenzi katika Miji zitatakiwa kufuata mfumo huo unaotegemewa kuanza kutumika 2014/2015. Halmashauri za Miji zimekuwa zikikabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kuwezesha uendelezaji wa Miji hususan upangaji na upimaji wa viwanja. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, mawasiliano yanaendelea kufanyika kuititia taasisi za fedha nchini ili kuwezesha Halmashauri kupata mikopo ya kupima viwanja vingi kwa mahitaji mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya wakazi wa kipato cha chini na kati na hivyo kupunguza ujenzi holela katika miji.

### Mradi wa Uendelezaji wa Miji ya Kimkakati (Tanzania Strategic Cities Project – TSCP)

19. **Mheshimiwa Spika**, katika dhana ya kusimamia maendeleo ya miji, kuna miradi inayotekeliza kwa lengo la kuendeleza miji Tanzania. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Uendelezaji Miji ya Kimkakati Tanzania (Tanzania Strategic Cities Project- TSCP) ambaa ulianza

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kutekelezwa kwenye Miji saba (7) na CDA- Dodoma ambayo ni Jiji la Arusha, Mbeya, Mwanza, Tanga, Manispaa za Dodoma, Kigoma Ujiji, Mtwara Mikindani na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma chini ya mkopo wa Benki ya Dunia wa **Dola za Marekani milioni 163** na msaada wa Serikali ya Denmark wa **Dola za Marekani milioni 12.5**. Mradi ulianza mwaka 2010/2011 na ultegemewa kukamilika mwaka 2014/2015. Hata hivyo, wakati mradi unafikia ukomo, Serikali imeiomba Benki ya Dunia pamoja na Serikali ya Denmark nyongeza ya fedha kwa ajili ya kukamilisha baadhi ya kazi muhimu zilizojitekeza za kuimarisha miundombinu na Taasisi ambazo ni pamoja na uandaaji wa Mipango Kabambe ya miji husika na uthamini wa majengo kwa ajili ya kukadiria kodi za majengo. Benki ya Dunia imekubali kuongeza **Dola za Marekani milioni 50** na Serikali ya Denmark itaongeza **Dola za Marekani milioni 6.0**. Hivyo, mradi huu utaongezewa muda hadi mwaka 2016/2017. Kati ya fedha hizo za nyongeza Halmashauri ya Manispaa ya Illemela ambayo ilianzishwa kutoka Halmashauri ya Jiji la Mwanza wakati mradi umeshaanza nayo itakuwa ni sehemu ya utekelezaji wa mradi huu.

20. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa uimarishaji wa Taasisi, Miji imewezeshwa kwa kupatiwa vitendea kazi, baadhi ya ofisi zimekarabatiwa na watumishi wamepatiwa mafunzo katika maeneo mbalimbali ya kitaalamu. Vilevile, kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi mfumo wa taarifa za kijiografia (Geographical Information System - (GIS) umeandaliwa kwa kutumia picha za anga (satelite images) ambazo zimeboreshwa (Digitized and rectified). Taarifa hizi zimeunganishwa katika mfumo ulioanzishwa wa Kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### **Mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Mamlaka za Serikali za Miji (Urban Local Government strengthening Project – ULGSP)**

21. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014 Serikali pia ilianza utekelezaji wa mradi wa kuimarisha miundombinu na kuimarisha uwezo wa kutoa huduma katika miji 18 (Urban Local Government Strengthening Project ) ambayo ni Halmashauri za Manispaa kumi na moja (11) na Halmashauri za Miji saba (7). Manispaa zinazohusika ni Bukoba, Iringa, Lindi, Morogoro, Moshi, Musoma, Shinyanga, Singida, Songea, Sumbawanga, na Tabora. Miji inayohusika ni Babati, Bariadi, Geita, Kibaha, Korogwe, Mpanda na Njombe. Aidha, kazi zilizofanyika katika kipindi hiki cha Julai hadi Machi, 2013/2014 ni usanifu wa miradi ya miundombinu itakayotekelzwa kwa gharama ya **shilingi bilioni 5.8** Miradi itakayohusika imechaguliwa na Halmashauri zenyewe.

22. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015 kazi za ujenzi na ukarabati zinategemewa kuanza katika miji yote kwa **Dola za Marekani milioni 44.3** isipokuwa Halmashauri za Manispaa ya Bukoba iliyokosa kigezo cha kutoendesha vikao muhimu vyta kisheria vya kuitisha bajeti ya mradi na Manispaa ya Tabora iliyopata hati isiyoridhisha ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. OWM-TAMISEMI inakusudia kuingilia kati mapema ili kuhakikisha upungufu huo unaondolewa na kuwezesha Halmashauri hizo kupata fedha kwa mwaka 2015/2016.

### **Mradi wa Kuendeleza Jiji la Dar es Salaam (Dar es Salaam Metropolitan Development Project – DMDP)**

23. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2013/2014, OWM-TAMISEMI ilifanya upembizi yakinifu na usanifu wa miradi iliyobuniwa kuendeleza Jiji la Dar es Salaam /Dar es Salaam Metropolitan Development Project (DMDP). Changamoto zilizopo katika ukuaji wa Jiji la Dar es Salaam ni kuongezeka kwa taka ngumu, ujenzi holela wa makazi, usafiri na usafirishaji. Halmashauri zote nne za Mkoa wa Dar es Salaam zimehusika katika kutayarisha mapendekezo ya miradi ya kipaumbele itakayotekelzwa kwa kuwashirikisha Wananchi na Sekta Binafsi. Miradi saba iliyoibuliwa ni ujenzi na ukarabati wa barabara za mitaa zitakazounganishwa na barabara

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kuu za Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na utupaji wa taka ngumu na miradi bunifu ya ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP). Vilevile, miradi mingine ni pamoja na kuimarisha usafiri wa reli na majini, kuboresha mfumo na miundo ya Taasisi, ukarabati na ujenzi wa mifumo ya maji ya mvua na uboreshaji wa makazi holela. Kazi hii itagharimu **shilingi bilioni 7.9** na inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2014/2015.

### **Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu ya Msingi**

**24. Mheshimiwa Spika**, OWM TAMISEMI inaendelea na jukumu la Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu Msingi kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM). Malengo ya Mpango huu ni kuimarisha ubora wa elimu kwa kuongeza uandikishaji watoto Darasa la Kwanza, kuajiri walimu zaidi, kuongeza miundombinu ya shule, kutoa fedha za uendeshaji wa Shule (Capitation Grant) na kutoa mafunzo kwa watendaji katika ngazi mbalimbali. Mpango huo umetekelizwa kuanzia mwaka 2001 na umefanyika katika vipindi cha miaka mitano mitano. Hivi sasa, Serikali inatekeleza awamu ya tatu ya MMEM ilioanza mwaka 2011/2012 na itakamilika mwaka 2015/2016.

**25. Mheshimiwa Spika**, mwaka 2014 watoto 1,261,476 wenyе umri wa kwenda shule walitarajiwa kuandikishwa Darasa la kwanza. Aidha, walioandikishwa ni 1,166,497 sawa na asilimia 92.5 wakiwemo wavulana 580,078 na wasichana 586,419. Takwimu hizi zinaonyesha kuwa bado ipo haja ya kuongeza uhamasishaji wa wazazi/walezi kuandikisha watoto wao shule. Hivyo, naomba nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, wazazi na walezi kuhakikisha kuwa watoto wote waliofikia umri wa kwenda shule wanaandikishwa.

**26. Mheshimiwa Spika**, wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza mwaka 2007 walikuwa 1,175,482 wakiwemo wavulana 584,659 na wasichana 590,828. Wanafunzi waliofanya Mtihani wa Taifa Darasa la saba mwaka 2013 ni 844,938 sawa asilimia 72 ya walioandikishwa wakiwemo wavulana 398,886 na wasichana 446,052. Hii inamaana kwamba wanafunzi 330,544 sawa na asilimia 28 hawakuhitimu darasa la VII. Naomba kutumia fursa hii tena kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, viongozi wa Mikoa, viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, wazazi na walezi wasimamie ipasavyo mahudhurio ya watoto shulenii ili wamalize mzunguko wa elimu ya msingi.

**Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na upungufu wa walimu wa shule za msingi, mwaka 2014 Serikali imeajiri walimu wa Cheti 17,928. Aidha, Serikali imepeleka **shilingi bilioni 4.8** kwenye Halmashauri zote nchini ili kuwalipa walimu hao posho na nauli.

**27. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014 hadi mwezi Machi, 2014 jumla ya **shilingi bilioni 21.1** zilipelekwa kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa kama ruzuku ya uendeshaji wa shule (Capitation Grant). Fedha hizo ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vyia kujifunzia na kufundishia, ukarabati wa miundombinu, utawala na kuendesha mitihani ya ndani. Serikali ilitenga shilingi bilioni 59.7 kwa ajili ya ununuzi wa vitabu kutoptokana na vidia ya Rada. Hadi sasa vitabu 20,406,792 vyenye thamani ya shilingi bilioni **56.3** vimenunuliwa na kusambazwa katika shule 15,735 nchini. Aidha, shilingi bilioni **3.4** kilichobaki, ununuzi na usambazaji utakamilika mwezi Julai, 2014. Aidha, shilingi bilioni **12.0** za fidia ya RADA zitatumika katika ununuzi wa madawati yatakayosambazwa katika Halmashauri zote nchini. Hadi sasa, Madawati 93,740 yameshanunuliwa na usambazaji wake katika Halmashauri zote nchini umeanza mwezi Mei. Kiasi hicho ni sawa na nusu ya madawati yaliyopangwa kununuliwa kwa fedha za RADA. Zabuni ya ununuzi huu imeshatangazwa ambapo usambazaji wa madawati utaanza kutekelezwa mwezi Julai 2014.

**Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu ya Sekondari.**

28. **Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha elimu kwa upande wa sekondari, Serikali ilibuni Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) kuanzia mwaka 2004 kwa lengo la kuinua kiwango cha utoaji wa elimu ya sekondari na ubora wake (access and quality). Mpango huu pia unatekelezwa kwa miaka mitano mitano. Hivi sasa tuko katika awamu ya pili ambayo ilianza mwaka 2010/2011 na itakamilika mwaka 2014/2015.

**Mheshimiwa Spika**, Katika utekelezaji wa Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) katika Sekta ya elimu, shule 1,200 za sekondari zinakamilisha ujenzi. Shule **264** kati ya hizo zikiwemo Shule mbili (2) kwa Halmashauri 132 zilipelekewa jumla ya shilingi **bilioni 56**. Kati ya fedha hizo shilingi **bilioni 30** zinatolewa na Serikali ya Tanzania na **bilioni 26** zimetolewa na Benki ya Dunia. Upembuzi yakinifu unaendelea ili kuendelea na ukarabati na ujenzi wa **shule 936** zilizobaki.

**Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na upungufu wa walimu wa shule za sekondari, mwaka 2014 Serikali imeajiri walimu wa stashahada 5,416 na wa shahada 12,994. Aidha, Serikali imepeleka **shilingi bilioni 7.1** kwenye Halmashauri zote nchini ili kuwalipa walimu hao posho na nauli.

29. **Mheshimiwa Spika**, katika masuala ya michezo napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mwezi Agosti, 2013 vijana wa Tanzania walishiriki michezo iliyofanyika Uganda katika mpira wa miguu, riadha na mpira wa meza. Aidha, michezo mingine ya UMISSETA na UMITASHUMTA itafanyika Julai 2014 Mjini Kibaha kama ilivyopangwa. Naomba kutoa taarifa kupitia Bunge lako Tukufu kwamba mwaka 2014 Tanzania imepewa heshima ya kuwa mwenyeji wa mashindano ya Umoja wa Michezo ya Sekondari katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Michezo hiyo itafanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Oktoba 2014.

30. **Mheshimiwa Spika**, mwaka 2013/2014 serikali ilianzisha mpango wa matokeo makubwa sasa (BRN) chini ya mpango huu, sekta ya elimu inatekeleza mikakati tisa (i) Upangaji wa shule kwa ufaulu (ii) Motisha kwa shule zilizofanya vizuri (ii) Kitabu cha Uongozi wa shule (Toolkit) (iv) Ufundishaji wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kkk (3Rs) (v) Ufundishaji rekebishi kwa wanafunzi wa Shule za Msingi (vi) Ufundishaji rekebishi kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari (vii) Motisha kwa walimu (viii) Ujenzi wa shule (ix) Ruzuku ya uendeshaji wa shule. Kati ya maeneo hayo OWM-TAMISEMI inatekeleza maeneo sita ambayo ni: (i) Utoaji wa ruzuku ya uedeshaji wa shule (Caption), (ii) ujenzi wa miundombinu ya shule za Sekondari, (iii) kutoa mafunzo rekebishi kwa wanafunzi wa shule za msingi (Step Primary), (iv) kutoa mafunzo rekebishi kwa wanafunzi wa shule za sekondari (Step Sekondari), (v) usambazaji wa kiongozi cha usimamizi wa shule (Toolkit) (vi) kutoa motisha kwa walimu (Teacher motivation).

**Malipo ya Madeni ya Walimu kwa Mwaka 2013/14.**

31. **Mheshimiwa Spika**, OWM- TAMISEMI inatambua changamoto ya madeni ya walimu yasiyohusika na mishahara na watumishi wengine katika mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu. Ili kukabiliana na changamoto hii Serikali imeweka mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na; kutenga fedha za likizo, matibabu, uhamisho na mafunzo; kutohamisha walimu iwapo hakuna fedha; kulipa fedha za likizo na uhamisho zinazopelekwa kwenye Halmashauri kupitia fedha za Matumizi Mengineyo; kutumia Mfumo wa LAWSON kulipa madeni ya mishahara moja kwa moja kupitia mshahara wa mtumishi husika, na tangu Julai, 2013 hakuna madeni mapya ya mishahara yanayozalishwa kutokana na matumizi ya mfumo huu wa elektroniki.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

32. **Mheshimiwa Spika**, Serikali pia inaendelea kuhakiki na kulipa madeni ya walimu kila hali ya fedha inaporuhusu. Hadi Februari 2014 shilingi **bilioni 19** sawa na **31%** ya madeni ya mishahara yaliyopokelewa yamelipwa.

Mchanganuo wa malipo umeoneshwa katika Jedwali lifuatalo;

Jedwali 3: **Mtiririko aa Malipo ya Madeni ya Walimu 2013/14 Yaliyohakikiwa**

### Usimamizi wa Huduma za Afya Ngazi ya Mkoa na Halmashauri

33. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kujenga hospitali mpya na kuzifanyia ukarabati hospitali za Mikoa ambazo sasa zinakuwa za Rufaa kwa lengo la kuboresha huduma za afya kote nchini. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 Serikali ilitenga shilingi **bilioni 2.95** kwa ajili ya ukarabati na shilingi **bilioni 8.46** kwa ajili ya ujenzi. Mikoa 5 inajenga hospitali mpya (Mara, Manyara, Mbeya, Shinyanga na Singida). Ujenzi wa hospitali ya Singida unaendelea na majengo yaliyokamilika ni pamoja na jengo la huduma za wagonjwa wa nje, jengo la huduma za uchunguzi kwa kutumia mionzi, jengo la kuhifadhi chanjo, jenereta la dharura, kuunganishwa kwenye umeme wa "grid" ya taifa pamoja na maji. Ujenzi wa hospitali ya Mkoa

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wa Mbeya uko katika hatua za ukamilishaji. Katika hospitali za Mikoa ya Mara na Shinyanga ujenzi unaendelea. Serikali itaendelea kutenga fedha kadri zitakavyopatikana ili maeneo ya kutolea huduma za afya kwa wananchi yaendelee kuboreshwa.

34. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 OWM-TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau wa Mfuko wa Pamoja wa Afya, Halmashauri zilitengewa shilingi **bilioni 87** na Mikoa shilingi **bilioni 3.7** ili kuongeza upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, kuboresha mifumo ya kutolea huduma za afya, mafunzo na uendeshaji wa ofisi. Hadi Desemba, 2013 Serikali ilipeleka shilingi **bilioni 43** kwenye Halmashauri na shilingi **bilioni 1.8** kwenye Mikoa kwa ajili ya kazi hizo.

35. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2012/2013 Halmashauri zilitengewa **shilingi bilioni 35.6** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM). Kati ya fedha hiyo **shilingi bilioni 15** ni fedha za nje na **shilingi bilioni 20** ni fedha za ndani. Hadi Juni 2013 **shilingi bilioni 25** zilipelekwa katika Halmashauri mbalimbali ikiwa **shilingi bilioni 10** fedha za ndani na **shilingi bilioni 15** fedha za nje. katika mwaka 2013/2014 fedha za sekta ya afya zilitengwa na kufungamanishwa kwenye ruzuku ya maendeleo ya Serikali za Mitaa (CDG), ambapo hadi Machi, 2014 **shilingi bilioni 41** zilipelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi kufikia mwaka 2013/14 mtandao wa kutolea huduma za afya nchini uliongezeka na kufikia Hospitali 218, vituo vya afya 578 na zahanati 5,478 sawa na ongezeko la Hospitali 39, vituo vya afya 112 na zahanati 1,067 ikilinganishwa na mtandao uliokuwepo mwaka 2012/13.

36. **Mheshimiwa Spika**, kupitia Mkakati wa Tatu wa Sekta ya Afya ushiriki wa Sekta Binafsi katika utoaji huduma za Afya za msingi umeimarishwa. Aidha, kila kituo cha kutolea huduma za afya kimeunda Kamati za uendeshaji na uongozi na katika hospitali za Wilaya zimeundwa Bodi za afya kwa lengo la kuimarisha ushiriki wa moja kwa moja wa wananchi katika uendeshaji na umiliki wa vituo vya kutolea huduma za afya na ustawi wa jamii.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na ongezeko la vituo vya kutolea huduma, OWM-TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imekamilisha Ikama mpya ya watumishi wa Sekta ya Afya kwa Hospitali za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Ikama mpya iliyokamilika Novemba, 2013 imezingatia hali halisi ya mazingira ya sasa ya mahitaji ya huduma za afya na mwingiliano wa taaluma zinazohitajika (skill mix) katika kutoa huduma stahiki za afya. Napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba, tayari Ikama hiyo imesambazwa kwa Makatibu Tawala wa Mikoa yote hapa nchini pamoa na Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili waitumie katika kujaza nafasi za watumishi kwa nia ya kukidhi mahitaji ya kuwahudumia wananchi na kukabiliana ipasavyo na adui maradhi, kuimarisha huduma za kinga, usafi wa mazingira sambamba na utoaji wa elimu ya afya na lishe bora kwa wananchi wa vijiji na mijini.

37. **Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha kila mwananchi anapata tiba sahihi wakati wote wananchi wanaendelea kuhamasishwa kuijunga na Mfuko wa Afya ya Jamii ili wajihakikishie kupata tiba wakati wote. Viwango vya kuijunga vimepangwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo za Hamashauri husika. Serikali pia huchangia kwa kiasi hicho hicho ambacho kimepatikana kwa njia ya michango ya wananchi (matching funds/tele kwa tele). Aina ya uanachama katika Mfuko huu ni kaya (baba, mama, na watoto wasiozidi umri wa miaka 18). Aidha, idadi ya wanakaya itategemea Sheria Ndogo ilioanzisha Mfuko. Mifuko hii inaendeshwa kwenye Halmashauri zote na katika kila kilipo kituo cha afya na zahanati. Ili kurahisisha utunzaji sahihi wa fedha za Serikali na kuweka kumbukumbu sahihi za matumizi ya fedha kila Zahanati na Kituo cha Afya na Hospitali zimefungua akaunti kwa ajili ya makusanyo ya fedha kutoka michango na ada za matibabu. Natoa wito kwa wananchi kutambua na kuijunga kwani mifuko hiyo ni ukombozi wa kujihakikishia tiba katika kaya zao.

38. **Mheshimiwa Spika**; kwa kutambua ukubwa wa tatizo la VVU/UKIMWI na malaria kitaifa, Serikali imeielekeza Mikoa na Halmashauri kubuni mbinu zitakazowezesha kuendelea kupambana na maambukizi ya VVU/UKIMWI na Malaria ili kuongeza kasi ya kupungua kwa maambukizi ya VVU/UKIMWI na kufikia malengo ya kitaifa ambayo ni maambuizi mapya vya VVU/UKIMWI kufikia 0 na maambukizi ya mama na mtoto kufikia 0 na kutokomeza malaria. Jithada hizi zitafanywa kwa kutumia fedha za Serikali, wadau wa maendeleo na mashirika ya maendeleo. Serikali pia itatumia Viwadudu vitakavyozalishwa na kiwanda cha Kibaha ili kuongeza kasi ya kutokomeza malaria. Aidha ongezeko la vituo vya kutoleaa huduma za afya na ongezeko la watumishi litawezesha Mikoa na Halmashauri kupunguza vifo vya mama na mtoto ili kufikia viwango vya kitaifa.

#### **Huduma ya TEHAMA**

39. **Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza huduma ya TEHAMA wataalam katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wameongezeka kutoka 76 mwaka 2012/2013 hadi kufikia 133 mwaka 2013/14. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, OWM-TAMISEMI imewezesha utengenezaji wa tovuti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 7 iliyochini ya Mradi wa Uendelezaji Miji ya Kimkakati (TSCP). Aidha, Ofisi imetengeneza Mfumo wa Kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa unaojulikana kama "**Local Government Revenue Collection Information System**" ambao umefanyiwa majaribio katika Jiji la Arusha na umeonyesha mafanikio makubwa katika kuongeza ukusanyaji mapato. Lengo kuu ni kuweka mfumo huu katika Halmashauri zote 164 kwa awamu kuanzia mwaka wa fedha 2014/2015. Hata hivyo kwa kuanzia, mfumo huu utawekwa katika Halmashauri 24.

40. **Mheshimiwa Spika**, OWM-TAMISEMI imeendelea kusimamia na kutoa msaada wa kitaalam na kiufundi katika mfumo wa kusimamia mapato na matumizi (**Integrated Financial Management System – (IFMS)**) katika Mikoa 21 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 133 sambamba na kutoa mafunzo ya matumizi ya IFMS kwa Wahasibu 142 nchini. Kazi ya uwekaji wa miundombinu ya TEHAMA na mfumo wa IFMS katika Mikoa mipy 4 na Halmashauri mipy 35 imepangwa kukamilika katika kipindi cha 2014/15.

41. **Mheshimiwa Spika**, miundombinu ya TEHAMA inayozunganisha Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa katika Kompyuta Kuu (Server) Dodoma ilitumia aina nne za teknolojia ambazo ni mkongo (Halmashauri 50), **Broadband Radio** (Halmashauri 14), **Satellite** (Halmashauri 14) na teknolojia ya **nyaya za shaba** (Halmashauri 82). Hata hivyo, teknolojia ya nyaya za shaba katika Halmashauri 44 imebadilishwa kwenda teknolojia ya mkongo ili kuongeza ufanisi wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA ukiwepo mfumo wa IFMS. Dhamira ya OWM-TAMISEMI ni kuongeza ufanisi kwa kuzunganisha Halmashauri zote kwenye mkongo wa Taifa katika mwaka 2014/2015.

42. **Mheshimiwa Spika**, mfumo wa IFMS ulioanza kutumika 2012/2013 umeleta mabadiliko katika kusimamia matumizi ya fedha za Serikali, taarifa za matumizi ya fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapatikana kwa urahisi katika Kompyuta Kuu Dodoma. Matumizi ya mfumo huu umezisaidia Halmashauri kufanya matumizi ya fedha kulingana na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako tukufu.

43. **Mheshimiwa Spika**, OWM-TAMISEMI imeweka miundombinu ya mfumo mpana wa mawasiliano (**Wide Area Network – WAN**) ambao unaiunganisha Mikoa 21 na Halmashauri 133. Vilevile, Wizara na Taasisi nyingine za Serikali zinazotumia mfumo huo ni pamoja na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (OR-MUU) na Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA). OWM TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kuimarisha miundombinu ya

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mfumo wa TEHAMA ili kuhakikisha usalama wa mfumo na miundombinu yake, kwa lengo la usimamizi mzuri wa rasilimali na kuongeza ufanisi wa shughuli za Serikali kwa kutumia mfumo huo.

### **Mfuko wa Barabara**

44. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2013/2014 **shilingi bilioni 151.3** kutoka Mfuko wa Barabara zilitengwa kwa ajili ya matengenezo, ukarabati na ujenzi wa barabara na madaraja. Hadi kufikia Machi, 2014 jumla ya shilingi billion **135.9** zilikuwa zimepokelewa na kupelekwa Halmashauri ambapo shilingi bilioni **55.5** zilikuwa zimetumika katika kukamilisha utekelezaji wa mpango kazi kwa mwaka 2012/2013 na **shilingi bilioni 80.4** kwa ajili ya utekelezaji wa mpango kazi kwa mwaka 2013/2014. Hadi kufikia Desemba kazi zilizofanyika katika kipindi hicho ni pamoja na matengenezo ya kawaida ambapo **km 2,300** zimetegenezwa kati ya km 8,400 zilizopangwa kwa mwaka na ya **shilingi bilioni 2.3** zimetumika kati ya **shilingi bilioni 8.0** zilizopangwa, matengenezo ya muda maalumu ambapo km 10 za lami zimekarabatiwa na km 459.5 za changarawe zimekarabatiwa kwa kutumia **shilingi bilioni 4** kati ya **shilingi bilioni 19.7** zilizopangwa. Matengenezo ya maeneo korofi (spot improvement) ambapo km 739.7 zimetengenezwa kati ya km 2,808.8 zilizopangwa kwa mwaka na **shilingi bilioni 3.0** zimetumika kati ya **shilingi bilioni 8.89** zilizopangwa. Pia, katika ukarabati na ujenzi wa barabara na madaraja km 8.4 za lami na km 80.25 za changarawe zimejengwa kwa kutumia **shilingi bilioni 1.6** kati ya shilingi billion **10.0** zilizopangwa. Madaraja manne yanayoendelea kujengwa hadi Disemba 2013 yameshaghari mu **shilingi milioni 89.7**.

45. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Bodii ya Mfuko wa Barabara imetenga **shilingi bilioni 225.5** kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara na madaraja, kuwajengea uwezo wahandisi, na usimamizi na ufuatiliaji. Fedha za Mfuko wa Barabara pekee hazikidhi mahitaji ya matengenezo na ujenzi wa barabara za Wilaya, hivyo Serikali itaendelea kutafuta vyanzo vingine vya fedha.

46. **Mheshimiwa Spika**, katika azma ya kuhakikisha kuwa barabara za vijiji zinaendelea kuboreshwa, OWM-TAMISEMI kwa kushirikiana na Jumuiya ya Ulaya (EU) inatekeleza mradi wa matengenezo ya barabara vijiji katika Halmashauri za Wilaya sita katika Mikoa ya Iringa, Morogoro na Ruvuma. Halmashauri hizo ni na Iringa, Mufindi, Ulanga, Kilosa, Songea na Mbanga. Mradi huu umegawanyika katika maeneo makuu mawili ambayo ni ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa km 149 kwa gharama ya **Euro milioni 17** na kujenga uwezo wa wataalam wa barabara katika Halmashauri husika.

47. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Misaada ya Kimaendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha changarawe ambapo km 1,000 zitafanyiwa matengenezo. Kwa kuanzia, km 178 zitatengenezwa kwenye Halmashauri nne za Kongwa, Mvomero, Kiteto na Kilombero. Lengo la mradi huu ni kurahisisha usafirishaji wa mazao kutoka mashambani kupelekwa kwenye masoko.

48. **Mheshimiwa Spika**, Mbilia mwagine wa maendeleo aliyejitokeza kushirikiana na Serikali ni Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Serikali ya Uingereza (DFID) ambalo linafadhili programu ya uboreshaji wa barabara vijiji. Programu hii ya miaka minne kuanzia mwaka wa fedha 2013/2014 hadi 2016/2017 itaboresha maeneo makubwa mawili ambayo ni kujenga barabara na madaraja kwenye maeneo korofi ili kuondoa vikwazo vya barabara vijiji na pili kujengea uwezo wa wahandisi. Jumla ya Halmashauri kumi na nne zitakazohusika katika programu hii ni Kilosa, Morogoro, Mbarali, Misenyi, Bukoba, Babati, Kondoa, Kongwa, Iringa, Mufindi, Igunga, Magu, Hai na Kasulu. Programu hii itagharimu jumla ya **shilingi bilioni 16.7**.

49. **Mheshimiwa Spika**, OWM-TAMISEMI kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza (DFID) kuititia "African Community Access Programme" (AFCAP)

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

inakusudia kuanzisha kituo cha utafiti wa vifaa (mali ghafi) vya ujenzi wa barabara, utafiti wa ubora wa kazi za barabara zinazojengwa, utafiti wa teknolojia rahisi na bora zinazoweza kutumika katika ujenzi wa barabara, kwa mfano; barabara za mawe, zege na za tabaka la lami((asphalt concrete, double surface dressing, otta seal) ili barabara zinazojengwa ziweze kudumu muda mrefu.

Aidha nitumie fursa hii pia kuwaomba wadau mbalimbali katika Sekta ya Barabara kuwekeza na kuanzisha Karakana za ukodishaji wa mitambo ya kujenga barabara kikanda, ili kusaidia wakandarasi wengi kupata mitambo ya kukodi na hivyo kuwawezesha kwenda kuomba kazi kwenye maeneo ya pembezoni mwa nchi.

### Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP)

50. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 Halmashauri zilitengewa jumla ya shilingi **bilioni 67.9** kwa ajili ya utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs). Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 35.3** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya uwekezaji ambayo haikukamilika katika kipindi cha utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi wa ASDP, shilingi **bilioni 16.4** ni kwa ajili ya kuboresha huduma za ugani, na shilingi **bilioni 16.2** ni kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya umwagiliaji.

51. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2014, shilingi **bilioni 37.2** zilikuwa zimepelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kati ya fedha hizo shilingi **bilioni 16.4** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kuimarisha Huduma za Ugani ambayo ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa vituo vya rasilimali za Kilimo vya Kata (Ward Agricultural Resource Centres-WARCs), kuimarisha Mashamba Darasa (Farmers' Field Schools-FFSs) na kujenga uwezo wa Halmashauri katika kutoa huduma bora za Ugani. Aidha, shilingi **bilioni 15.9** ni kwa ajili ya ujenzi wa skimu za umwagiliaji, na shilingi **bilioni 4.9** kwa ajili ya miradi ya uwekezaji.

52. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hicho Halmashauri zimeendelelea kutekeleza na kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo ya kilimo kwa kutumia fedha za bakaa ya mwaka 2012/2013 ambapo hadi kufikia Januari 2014, jumla ya malambo **32** yamejengwa na mengine kukarabatiwa kwa ajili ya maji ya mifugo. Masoko ya msingi ya mifugo **43**, machinjo **53**, na vituo vya kukusanya maziwa **21** vimejengwa ambapo vikundi vya wafugaji **523** na zaidi ya wakulima **173,271** wamenufaika. Majosho **229** na vituo **33** vya tiba za mifugo vimejengwa na mifugo zaidi ya **5,525,102** imepatiwa chanjo dhidi ya magonjwa mbalimbali.

53. **Mheshimiwa Spika**, eneo linalomwagiliwa limeongezeka kutoka hekta **264,388** hadi **463,615** hali ambayo imewezesha kuongezeka kwa mazao kama mpunga kwa wastani wa tani **2** hadi **6** kwa hekta na mahindi wastani wa tani **0.7** hadi **4.7** kwa hekta. Maghala ya kuhifadhi mazao **255** na masoko ya mazao **23** yamejengwa. Pia mashine **2,311** za kukoboa na kusaga naafaka zimenunuliwa ambapo zaidi ya wakulima **715,125** wamenufaika. Barabara mliso zenye urefu wa kilomita **103** na madaraja **5** yamejengwa na kuwanufaisha wakulima zaidi ya **40,202**. Ng'ombe zaidi ya **47,184**, Kuku **7,225** na Mbuzi **5,422** wamenunuliwa, wameboreshwa na kugawiwa kwa wafugaji wadogo. Aidha, kilo **50,343** za mbegu bora za mazao zimegawiwa kwa vikundi **4,214** na kusambazwa kwa wakulima wengine. Wafugaji wamepatiwa madume bora ya ng'ombe yapatayo **2,993**, mbuzi **1,487** na majogoo **8,643** kwa lengo la kuongeza uzalishaji ambapo wakulima zaidi ya **9,821** wamenufaika.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Wataalam wa huduma za Ugani, idadi imeongezeka kutoka **3,326** mwaka 2006/2007 na kufikia **10,891** katika kipindi cha 2013/2014 na kati yao **6,925** ni Wataalam wa Kilimo na **3,966** wa Mifugo kwa lengo la kuboresha huduma za

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ugani. Aidha, taratibu za kuajiri Maafisa Ugani **1,050** wa ngazi ya cheti na 334 wa ngazi ya stashahada unaendelea ambapo watapangiwa kwenye Halmashauri.

54. **Mheshimiwa Spika**, OWM TAMISEMI imechukua hatua ya kufuatilia migogoro kati ya wakulima na wafugaji ili kujua chanzo cha migogoro hiyo kwa kushirikiana na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na kwa kupata taarifa kutoka Mikoa yote. Katika kufuatilia imebainika kuwa chanzo cha migogoro hiyo ni:-i) kukosekana kwa mipango bora ya ardhi kwenye vijiji, ii) mabadiliko ya tabia nchi yanayosababisha kuwepo kwa ukame na hivyo kuwafanya wafugaji kuhama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, iii) baadhi wakulima na wafugaji kutotii sheria kwenye vijiji vyenye mpango bora ya ardhi na iv) baadhi ya viongozi kwenye ngazi mbalimbali kutuhumiwa kupokea rushwa na hivyo kuwaruhusu wakulima au wafugaji kulima au kufuga kwenye maeneo yasiyorohuswi.

**Mheshimiwa Spika**, hatua zilizochukuliwa na OWM-TAMISEMI ni kuhimiza kuwepo kwa mipango bora ya ardhi kwenye maeneo ya vijiji, kuweka juhudzi za makusudi za kuwahimiza wananchi kuzingatia sheria zilizowekwa kuhusu mipango na matumizi ya ardhi na kuwachukulia hatua za kinidhamu viongozi wanaothibitika kupokea rushwa.

55. **Mheshimiwa Spika**, chini ya program ya uendelezaji wa kilimo nchini, jumla ya matrekta 6,100 na matrekta ya kukokotwa na mikono (Power tillers) 4,051 yamenunuliwa. Aidha, vituo **3** vya kutolea huduma za mafunzo kwa zana za kilimo vimejengwa na kufikia jumla ya vituo **200** ambapo zaidi ya wakulima **187,321** wamenufaika. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 kiasi cha **shilingi billioni 23** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya umwagiliaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

56. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa kilimo, OWM-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara za kisekta itazisimamia Halmashauri 28 katika kutekeleza mpango wa Matookeo Makubwa Sasa (BRN) ambapo skimu za umwagiliaji **78** zitafufuliwa, kukarabatiwa na kujengwa. Maghala **275** yatajengwa na kurabatiwa na mashamba makubwa **25** ya uwekezaji kwa ajili ya kilimo cha mpunga na miwa yatalimwa. Aidha OWM-TAMISEMI itakuwa na jukumu kubwa la kuwajengea uwezo wakulima, kupeleka wataalamu, kuanda miongozo ya kisheria ya Umoja wa Umwagiliaji na kuajiri wakandarasi na kuwasimamia kwa lengo la kutoa huduma bora kwa jamii katika maeneo husika.

### Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Viwanda vya Ngozi

57. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2013/2014 **shilingi 851,000,000** zilipelekwa kwenye Halmashauri **65** na **shilingi 42,500,000** katika Sekretariati za Mikoa 17 zinazotekeliza mkakati wa kufufua na kuendeleza viwanda vya ngozi. Hadi kufikia Januari, 2014 jumla ya wafugaji **6,728**, wachinjaji na wachunaji **2,662**, wawambaji na wachambuzi **1,050** wa madaraja ya ngozi, wafanyabiashara za ngozi **441**, Madiwani na Viongozi wengine wa Serikali **4,480** wamehamasishwa na kupewa mafunzo kuhusu shughuli za mkakati huo. Aidha, Fremu **13** za kukaushia ngozi zimejengwa na machinjio **6** yamekarabatiwa na **5** yamejengwa.

58. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/2015 shilingi **676,000,000** zimetengwa katika Halmashauri **65** na shilingi **17,000,000** zimetengwa katika Sekretarieti za Mikoa **17** zinazotekeliza Mkakati huu wa ngozi.

### Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RWSSP)

59. **Mheshimiwa Spika**, jumla ya shilingi **bilioni 316.5** zilipangwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu ya Maji Vijijini ambapo hadi mwezi Desemba, 2013 jumla ya shilingi **bilioni 139**

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

zimepelekwa kwenye Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa. Aidha, jumla ya shilingi **bilioni 73.29** zimetumika hadi kufikia Machi, 2014 zikiwa ni sehemu ya bakaa ya mwaka wa fedha 2012/2013. Katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Halmashauri zimeendelea kutekeleza na kukamilisha miradi mbalimbali ya Maendeleo ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira. Katika kutekeleza programu hii, jumla ya vituo **6,222** vya huduma za maji vimejengwa na wananchi wapatao **1,555,500** wananufaika na huduma ya Maji Vijiiji. Pia, jumla ya wananchi **110,131** wamehamasishwa juu ya usafi wa mazingira na matumizi ya vyoo bora. Aidha, jumla ya vituo vya kunawia mikono **73,595** vimejengwa na Vijiiji **1,019** vinapata huduma ya usafi wa mazingira kutoka kwa watoa huduma.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuendeleza mafanikio yaliyopatikana, Serikali katika mwaka 2014/2015 itaendelea kutoa elimu juu ya usimamizi wa programu ya maji na kutoa mwongozo kuhusu “**unit cost**” katika miradi ya maji kwa watumiaji ili kuchangia gharama za uendeshaji.

### Programu ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu (PFM)

60. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Programu ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu chini ya ufadhili wa Serikali ya Denmark ilitengewa shilingi **milioni 400** kwa ajili ya uratibu na utekelezaji katika baadhi ya Halmashauri za Wilaya za Mikoa ya Iringa, Mbeya, Morogoro, Lindi na Njombe. Hadi mwezi Machi 2014, shilingi **milioni 271.1** zilitolewa kwa ajili ya uratibu na utekelezaji wa program hiyo. Kati ya fedha hizo, shilingi **milioni 83** ni kwa ajili ya uratibu ngazi ya OWM-TAMISEMI, shilingi **milioni 35.8** Sekretarieti za Mikoa husika na **shilingi milioni 152.3** zilipelekwa katika Halmashauri zinazotekeliza program hiyo.

61. **Mheshimiwa Spika**, kazi ya kupitia upya andiko la Programu ya Taifa ya Misitu na Nyuki iliyokuwa inafanywa na Serikali ya Finland kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania imekamilika mwezi Desemba, 2013. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kiasi cha shilingi **milioni 388.1** kilitengwa kwa ajili ya uratibu na utekelezaji wa shughuli za Usimamizi Shirikishi wa Misitu katika baadhi ya Halmashauri za Mikoa ya Kagera, Kigoma, Morogoro, Lindi, Rukwa, Ruvuma na Tanga. Hata hivyo, fedha hizo hazikuweza kutolewa.

**Mheshimiwa Spika**, mwaka wa fedha 2014/2015 **shilingi milioni 437** zimetengwa kwa ajili ya uratibu na utekelezaji wa shughuli za Usimamizi Shirikishi wa Misitu katika baadhi ya Halmashauri za Mikoa ya Kagera, Kigoma, Morogoro, Lindi , Rukwa, Ruvuma na Tanga.

### TAASISI ZILIZO CHINI YA OWM-TAMISEMI:

**Mheshimiwa Spika**, OWM-TAMISEMI inaratibu na kusimamia taasisi 5 zilizo chini yake ambazo ni Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa, Shirika la Elimu Kibaha, Chuo cha Serikali za Mitaa - Hombolo na Wakala wa Usafiri wa Haraka Dar es Salaam (DART).

### Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa

62. **Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ni kuhakikisha kwamba Halmashauri zinaendelea kupata na kunufaika na mikopo. Katika mwaka 2013/2014 Bodi imeshughulikia urekebishaji wa muundo wake ili uweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Lengo ni kuwa chombo kinachojitegemea na chenye uwezo wa kutoa mikopo zaidi kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hatua iliyofikiwa ni pamoja na Mtaalamu Mshauri M/S Konsalt LTD kuwasilisha ripoti ya Uchambuzi wa marekebisho ya Muundo wa Bodi kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kutolea maoni. Wadau walioshirikishwa katika mchakato huu ni pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, OWMTAMISEMI, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Tume ya Mipango, Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(ALAT), Mikoa, Halmashauri, Kamati za Kudumu za Bunge za TAMISEMI, Hesabu za Serikali za Mitaa na Katiba, Sheria na Utawala. Wadau wote waliunga mkono mapendekezo ya kubadili muundo wa Bodi kuwa Benki ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (*Local Government Development Bank*). Katika kufanikisha azma hii mtaji wa **shilingi bilioni 44.8** unatakiwa kukusanya ambapo Mamlaka za Serikali za Mitaa zitatakiwa kuchangia **shilingi bilioni 5.2**, Serikali Kuu **shilingi bilioni 17** na Taasisi za Kifedha, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Washirika wa Maendeleo **shilingi bilioni 22**. Waraka wa Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kupata idhini ya Serikali umeandalowi.

63. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014 Bodi ilikadiria kukusanya michango ya Akiba ya **shilingi milioni 435**. Hadi Machi, 2014 shilingi **milioni 91.7** zimechangwa sawa na asilimia 21 ya makadirio. Aidha, mikopo ya shilingi **milioni 800** ilikadiria kurejeshwa kutoka kwenye Halmashauri **13**. Hadi Machi, 2013/2014 **shilingi milioni 410.6** sawa na asilimia 51.3 ya makadirio zilirejeshwa. Bodi ilikadiria kutoa mikopo ya **shilingi bilioni 2.5**. Hadi Machi, 2014 mikopo ya **shilingi bilioni 1.2** imetolewa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Mbinga na Mwanga. Tangu Bodi ianzé 1986 mikopo ya **shilingi bilioni 7.4** imetolewa sawa na asilimia 16.6 ya maombi yaliyowasilishwa ya **shilingi bilioni 44.7**.

64. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Bodi itaendelea na mpango wa kukamilisha kubadili muundo wake wa kuwa Benki ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa, kutoa mikopo kwenye Halmashauri, kukusanya mtaji wa Benki, kufuatilia madeni ya michango na marejesho ya mikopo na riba kwenye Halmashauri.

### **Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa**

65. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014 Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF) umeandikisha wanachama wapya 24,740 na kufanya idadi ya wanachama kuongezeka kutoka 104,840 Juni 2013 na kufikia 141,702 Machi, 2014. Mfuko umekusanya jumla ya **shilingi bilioni 387.44** kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na michango ya wanachama, mapato kutokana na vitega uchumi na marejesho ya vitega uchumi vilivyokomaa.

66. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015 Mfuko utaendelea kulipa mafao na pensheni za wastaafu kila mwezi kwa mujibu wa Sheria. Matarajio ya Mfuko ni kuongeza thamani ya rasilimali zake kutoka shilingi **bilioni 789.84** za sasa hadi shilingi **bilioni 971.50** ifikapo Juni, 2015. Ongezeko hili ni pamoja na Jengo la kitega uchumi linalojengwa kwa ubia na Jiji la Mwanza. Jengo hilo linagharimu jumla ya **Shilingi bilioni 60**. Ujenzi unatarajia kukamilika mwezi Agosti, 2014 na kuanza kupangishwa. Aidha, ujenzi wa jengo la ghorofa 10 la ofisi za makao makuu ya mfuko mjini Dodoma unatarajiwa kukamilika Desemba, 2014 kwa gharama ya **shilingi bilioni 47**. Vilevile, ujenzi wa jengo la ghorofa 30 la Millennium Tower umekamilika kwa gharama ya shilingi **bilioni 63**. Jengo hili litatumika kama kitegauchumi cha mfuko.

### **Shirika la Elimu Kibaha**

67. **Mheshimiwa Spika**, Shirika la Elimu Kibaha limeendelea kutimiza malengo ya kuanzishwa kwake ya kupambana na maadui ujinga, umaskini na maradhi. Ili kutimiza malengo hayo, Shirika limetumia rasilimali na vitendea kazi vyake kwa ufanisi na hivyo kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi.

68. **Mheshimiwa Spika**, mwaka 2013/2014 Shirika lilikuwa na lengo la kuhudumia wagonjwa 450,000 katika Hospitali Teule ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani (Tumbi) ambapo hadi Machi, 2014 jumla ya wagojwa waliohudumiwa ni 454,000. Shirika pia lilienga kutoa Elimu ya utabibu kwa wanachuo 120, ambapo hadi Machi, 2014 wanachuo 118 walipatiwa mafunzo

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

hayo. Aidha, kumekuwa na mafanikio ya ukusanyaji wa mapato hospitalini kwa wastani wa **shilingi 450,000/=** kwa siku na kufikia wastani wa kat i ya **shilingi 2,500,000 na 3,000,000/=** kwa siku kutokana na juhud i za kutumia TEHAMA katika ukusanyaji wa mapato. Pia, katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2013/ 2014 Shirika limehudumia wahanga wa ajali za barabarani 1,854, zilizotokana na pikipiki, magari na watembea kwa miguu.

69. **Mheshimiwa Spika**, Shirika lilikuwa na lengo la kutoa elimu na malezi bora kwa wanafunzi 2,734, (yaani wanafunzi wa Sekondari 1,712 na wanafunzi wa shule za msingi 1,022). Katika mwaka 2013/2014 wanafunzi 2,813 walipatiwa elimu na malezi bora. Kiwango cha ufaulu wa kidato cha IV kwa matokeo ya mwaka 2013 kilikuwa ni wastani wa asilimia 91.3 kwa shule zote tatu za sekodari (Kibaha Wavulana, Tumbi na Kibaha Wasichana), kwa darasa la saba shule ya Msingi ufaulu ni asilimia 94. Pia, Shirika lilikuwa na lengo la kuendelea kutoa huduma za maktaba kwa wananchi 50,000. Hadi kufikia Machi, 2014 wananchi 49,330 wamenufaika na huduma ya maktaba.

70. **Mheshimiwa Spika**, Shirika liliendelea kutoa mafunzo katika fani mbalimbali kupitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha. Fani hizo ni pamoja na kilimo na mifugo, uashi na useremala, umeme na magari, upishi na ushonaji, uungaji na uundaji vyuma pamoja na udereva ambapo wanachuo 420 walipatiwa mafunzo hayo. Aidha, Shirika lilitoa elimu ya nadharia na vitendo juu ya ufugaji bora wa kisasa wa ng'ombe wa maziwa kwa wananchi 80.

71. **Mheshimiwa Spika**, malengo ya Shirika kwa mwaka 2014/2015 ni pamoja na kuendelea na uendeshaji wa Hospitali Teule ya Rufaa ya Mko a wa Pwani Tumbi kwa kuhudumia wagonjwa 450,000, kutoa mafunzo ya Maafisa Tabibu 120; kutoa elimu ya awali, msingi, sekondari na malezi bora kwa wanafunzi 2,784; kutoa elimu katika fani mbalimbali katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha; kutoa huduma za Maktaba kwa wananchi 50,000, kutunza mazingira ikiwa ni pamoja na kupanda na kuitunza miti 1,680 ambayo imepandwa tayari; kutoa elimu ya nadharia na vitendo juu ya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa; ukarabati wa miundombinu ya Shirika; na kuendelea na utekelezaji wa mpango wa matumizi ya ardhi ya Shirika. Shirika litaendelea na kazi ya upanuzi wa hospitali ya Tumbi.

72. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Shirika la Elimu Kibaha limetengewa **shilingi bilioni 11** Kati ya fedha hizo mishahara ni **shilingi 8,882,383,000.00**, matumizi mengineyo **Shilingi 1,977,917,000.00** na **shilingi 150, 000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Aidha, Shirika kupitia Katibu Tawala wa Mko a wa Pwani limetengewa shilingi **bilioni 1** kwa ajili ya upanuzi wa Hospitali Teule ya Rufaa ya Mko a wa Pwani. Aidha, Shirika limejiwekea mkakati wa kuongeza mapato ya ndani hasa kupitia Hospitali Teule ya Tumbi kwa kuboresha mfumo wa TEHAMA kwenye makusanyo.

### Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo

73. **Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Chuo cha Serikali za Mitaa ni pamoja na kutoa mafunzo ya uendeshaji wa Serikali za Mitaa kwa viongozi na watumishi walio katika ngazi mbalimbali za Serikali za Mitaa; kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ya taaluma ya Serikali za Mitaa; kutoa mafunzo juu ya mabadiliko yanayohusu Serikali za Mitaa kulingana na Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa na kutoa ushauri kwa Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, mashirika na watu binafsi juu ya masuala yote yanayohusu Serikali za Mitaa.

74. **Mheshimiwa Spika**, Chuo kimeendelea na mpango wake wa kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa kozi nane katika ngazi ya astashahada na stashahada. Kozi hizo ni

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Astashahada na Stashahada ya Uhasibu na Fedha, Utawala katika Serikali za Mitaa, Maendeleo ya Jamii na Usimamizi wa Rasilimali Watu katika Serikali za Mitaa.

75. **Mheshimiwa Spika**, Chuo kinashirikiana na taasisi nyingine katika kuboresha na kujenga uwezo katika nyanja mbalimbali za kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Taasisi hizo zinajumuisha Shirika la Maendeleo la Japan (JICA), Taasisi ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa Korea Kusini (LOGODI), na Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (BTC). JICA inajenga uwezo wa wahadhiri katika eneo la uandaaji wa mitaala, kufanya tathmini na kusimamia ubora wa mafunzo ya watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ushirikiano kati ya Chuo na Shirika la Maendeleo la Ubelgiji katika eneo la kujenga uwezo wa manunuzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (Enhancement of Procurement Capacity of Local Government Authorities Project), umeweza Chuo kunufaika kwa kupata mitaala ambayo itatumika kutoa mafunzo ya muda mfupi ya manunuzi ya umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

76. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, Chuo kilidahili wanafunzi wapya 1,623 kwa kozi nane zilizotajwa hapo juu na kufikisha jumla ya wanafunzi 2,547. Vilevile, Chuo kiliendesha mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi na Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa 474. Mafunzo hayo yaliyohusu Stadi za Uongozi, Utawala Bora, Mafunzo elekezi ya awali, Uongozi wa Kimkakati, mahusiano kati ya Watendaji wa Halmashauri na viongozi wa kuteuliwa, utunzaji wa kumbukumbu na uwajibikaji wa kijamii.

77. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Chuo kilipewa **shilingi 550,000,000** kwa ajili ya kukamilisha zoezi la kulipa fidia kwa wananchi 83 ambaao maeneo yao yalichukuliwa kwa ajili ya upanuzi wa Chuo.

78. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Chuo kimepanga kudahili wanachuo wapya 1,830, kwa kozi zote nane zinazotolewa kwa sasa, kufanya tafiti mbili (2) katika maeneo yanayohusu Serikali za Mitaa, kununua basi kubwa lenye uwezo wa kubeba abiria sitini (60), kununua vitabu 800 na kompyuta za maabara 50, kuajiri watumishi wapya 48 na kuendelea na ujenzi wa kituo cha afya.

79. **Mheshimiwa Spika**, Chuo kimechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na wadau mbalimbali (TEA, TBA, NHC) ili kuweza kujenga mabweni, madarasa na nyumba za watumishi kwa lengo la kuondoa matatizo hayo. Chuo kinaendelea na jitihada za kutoa mafunzo ya muda mfupi na ushauri ili kuongeza kipato na kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini.

### **Wakala wa Usafiri wa Haraka Dar es Salaam (DART)**

80. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ilianzisha Wakala wa Usafiri wa Haraka (DART) kwa madhumuni makuu matatu ambayo ni kusimamia utekelezaji na uendeshaji wa mfumo wa mabasi yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam; kuweka mpangilio makini wa matumizi ya barabara kuu na ndogo kwa watumiaji wote ili kupunguza msongamano; na kuhakikisha kuwepo kwa menejimenti ya Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka yenyе kuleta tija na ufanisi. Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam unatekelezwa katika awamu sita zenyе kilometra 130.3 kwa awamu zifuatazo; awamu ya kwanza barabara ya Morogoro, Kawawa kaskazini Msimbazi hadi Kivukoni (20.9Km); awamu ya pili Kilwa, Kawawa Kusini (19.3km); awamu ya tatu barabara ya Nyerere, Uhuru, Bibi Titi, Azikiwe (23.6 km); awamu ya nne barabara ya Bagamoyo Sam Nujoma (16.1km); awamu ya tano barabara ya Mandela, Barabara mpya (22.8km); na awamu ya sita barabara ya Old Bagamoyo, na barabara mpya mbili (27.6 km).

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

81. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14 Wakala wa Usafiri wa Haraka (DART) uliendelea na ujenzi wa barabara zenyе urefu wa Km 20.9. Gharama za ujenzi wa mfumo huu awamu ya kwanza ni dola za Marekani million 325.37. Serikali hadi sasa imechangia shilingi bilioni 23.5 kwa ajili ya ulipaji wa fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu awamu ya kwanza. Sanjari na ujenzi wa awamu ya kwanza, Wakala hivi sasa unaendelea na ukamilishaji wa usanifu wa kina wa mfumo wa DART awamu ya 2 & 3 zitakazokuwa na urefu wa Km 42.3.

82. **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa vituo vikubwa vitano (5) katika maeneo ya Kimara, Ubungo, Morocco, Kariakoo na Kivukoni unaendelea. Kituo kikuu cha Mabasi Kivukoni kimekamilika kwa asilimia 95 na kipo katika hatua za mwisho za marekebisho. Vituo vya Ubungo, Kimara, Morocco na Kariakoo ujenzi unaendelea sambamba na ujenzi wa barabara. Aidha ujenzi wa vituo vidogo 27 kwa ajili ya kuhudumia mabasi 65 kwa saa kwa kila mwelekeo unaendelea. Pia ujenzi wa vituo mliso (Feeder Stations), vinaendelea kujengwa katika maeneo ya Shekilango, Kinondoni A, Mwinjuma, na Magomeni ambako ujenzi umefikia asilimia 28.

83. **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa karakana (bus depot) mbili za kupaki mabasi unaendelea katika eneo la Ubungo na Jangwani. Karakana hizo zitakuwa za kisasa kwa ajili ya kukagua, kusafisha na kutengeneza mabasi. Ujenzi wa Karakana ya Jangwani umefikia asilimia 70 ya utekelezaji. Aidha, ujenzi wa Karakana ya Ubungo bado haujaanza kutohuna eneo kushindwa kupatikana kwa wakati uliopangwa.

84. **Mheshimiwa Spika**, Wakala wa DART kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam unafanya maandalizi ya kuboresha barabara mliso (Feeder Roads). Wakala umeainisha barabara mliso na kuziwasilisha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni na Ilala ili ziwekwe katika vipaumbele vya utekelezaji hasa kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Jiji la Dar es salaam "Dar es Salaam Metropolitan Development Project (DMDP) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

85. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka 2013/14 Wakala uliendelea na ulipaji wa fidia kwa waliokuwa wakazi wa Kariakoo Gerezani Jumla ya wakazi 71 kati ya 106 wamekwisha chukua fidia zao. Maeneo mengine yaliyohusika na ulipaji wa fidia ni Kituo Kikuu cha Mabasi cha Ubungo, Magomeni Bondeni na Manispaa ya Ilala Kata ya Mchafukoge.

86. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi unahusisha Sekta binafsi kupitia utaratibu wa "Public Private Partnership" (PPP). Sekta binafsi intarajiwа kuwekeza kiasi cha Dola za Marekani 100 milioni kwa ajili ya ununuzi wa mabasi, ukusanyaji wa nauli na utunzaji wa fedha ili kuwa tayari mfumo utakapoanza Septemba, 2015. Wakala umemwajiri Mshauri mwelekezi "Transaction Advisor" ambaye ni kampuni ya Rebel group ya Uhlanzi kukamilisha taratibu za kuwapata wawekezaji kupitia sekta binafsi.

87. Aidha, Wakala unaendelea na maandalizi ya mkutano wa wawekezaji uliopangwa kufanyika mwezi Juni, 2014. Aidha Mshauri Mwelekezi wa Biashara amefanya zoezi la kuwaandikisha wamiliki wa daladala na madereva kuanzia tarehe 31 Machi 2014 ili kuwahamasisha kuanzisha makampuni ili baadaye washiriki katika kutoa huduma ya mabasi katika utekelezaji mradi wa DART.

88. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2014/15 Wakala wa Usafiri wa Haraka utaendelea kufuatilia kwa karibu maendeleo ya ujenzi wa miundombinu ya mfumo wa DART kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara wa Tanzania (TANROADS) kwa kutekeleza yafuatayo; kukamilisha maandalizi ya upatikanaji wa watoa huduma katika mfumo wa DART (mabasi, ukusanyaji wa nauli na utunzaji wa fedha) ambao unasimamiwa na "Transaction Advisor";

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ujenzi wa kituo cha kuongozea mawasiliano (control centre) na ujenzi wa Ofisi ya Wakala wa DART katika eneo la kituo kikuu cha mabasi cha Ubungo; maandalizi ya utoaji wa huduma za awali (interim services) katika eneo la Kimara Mwisho hadi Kivukoni mwishoni mwa mwaka 2014; kuendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Mawasiliano wa Wakala ipasavyo ili kuwawezesha wadau wote waelewe mfumo wa DART.

### **Mpango wa Utekelezaji kwa mwaka 2014/2015**

89. **Mheshimiwa Spika**, Kazi zitakazofanyika katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 kwa upande wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa, na Halmashauri ni kama ifuatavyo:

#### **Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

- (i) Kuziwezesha Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa kuzingatia dhana ya upelekaji madaraka kwa Umma;
- (ii) Kujenga uwezo wa watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuwapatia vitendea kazi na mafunzo mbalimbali ili waweze kuongeza ufanisi kazini;
- (iii) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali Mikoani na kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- (iv) Kuratibu na kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa;
- (v) Kuratibu utekelezaji wa dhana ya Matokeo Makubwa sasa hususan miradi ya maji, kilimo na elimu inayotekeliza kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- (vi) Kuratibu shughuli uendeshaji wa shughuli za Elimu ya Msingi na Sekondari;
- (vii) Kusimamia matumizi ya rasilimali za umma kwa kuimarisha uwajibikaji, mifumo ya TEHAMA na utoaji wa taarifa kwa wananchi;
- (viii) Kugharamia shughuli za Taasisi za Shirika la Elimu Kibaha, kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, kuimarisha Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na Wakala wa Usafiri wa Haraka Dar es Salaam (DART);
- (ix) Mfuko wa Barabara utaendelea kuziwezesha Halmashauri kuzifanyia matengenezo barabara za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara;
- (x) Kuendelea kulipia fidia ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF);
- (xi) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Sera, Programu za maboresho na miradi iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(xii) Kuratibu shughuli za masuala mtambuka kama vile kudhibiti UKIMWI, rushwa na uharibifu wa mazingira.

### **Mikoa**

- (i) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya Mikoa mipyä iliyoanzishwa pamoja na Wilaya mpyä;
- (ii) Kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yao kwa kusimamia na kufuatilia shughuli mbalimbali za maendeleo;
- (iii) Kuratibu uchaguzi wa Serikali za Mitaa;
- (iv) Kuendelea na ukamilishaji wa Miradi yote iliyokwishaanza hususan ujenzi na ukarabati wa ofisi na nyumba za Wakuu wa Mikoa, Wilaya na hospitali za Mikoa;
- (v) Kuendesha vikao vya kisheria na vya kazi kama vile Kamati za Ushauri za Mikoa na Wilaya (RCC, DCC na ICF);na
- (vi) Kushughulikia masuala mtambuka kama vile maafa, UKIMWI na usimamizi wa mazingira.
- (vii) Kuratibu na kusimami utekelezaji wa Mpango wa Matokeo Makubwa sasa (BRN).

### **Mamlaka za Serikali za Mitaa**

- (i) Kukamilisha miradi ya maendeleo iliyokwishaanza;
- (ii) Kuboresha na kuongeza mtandao wa barabara za vijijini;
- (iii) Kuendesha zoezi la uchaguzi wa Serikali za Mitaa;
- (iv) Kukamilisha ujenzi wa Shule za Sekondari ikiwa ni pamoja na ujenzi wa hosteli na maabara na kupanua baadhi ya shule kwa ajili ya kuongeza kidato cha tano na sita; Kuandaa na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi mijini na vijijini na kudhibiti migogoro ya ardhi; na
- (v) Upangaji, ufuatiliaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo inayohusiana na Sekta mbalimbali katika maeneo yao pamoja na shughuli za Matokeo Makubwa Sasa (BRN).

### **Shukurani**

90. **Mheshimiwa Spika**, Napenda kumshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda (Mb) kwa miongozo na maelekezo yake ya mara kwa mara ambayo mara zote yamerahisisha utekelezaji wa majukumu yangu.

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu yote niliyoyaeleza yametekelizwa kwa ushirikiano mkubwa wa viongozi wote wa OWM TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Napenda kuwashukuru kwa juhudhi zao kubwa wanazozionyesha katika kutekeleza majukumu tuliyopewa dhamana na Taifa. Shukurani zangu za pekee nazielekeza kwa Naibu Mawaziri Mhe. Aggrey Mwanri (Mb) na Kassim Majaliwa (Mb), Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa ushirikiano na ushauri wanaonipa wakati wote. Aidha, napenda nitoe shukurani zangu za dhati

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwa Katibu Mkuu Bwana Jumanne Sagini, Naibu Makatibu wakuu, Wakuu Dkt. Deo Mtasiwa, Bw. Zuberi Samataba na Bw. Kagyabukama E. Kiliba Wakuu wa Idara, Vitengo, Wakuu wa Taasisi na Makatibu Tawala wa Mikoa, Mameya na Wenyeviti wa Halmashauri, Wakurugenzi wa Halmashauri, Madiwani na watumishi wote kwa umaja na mshikamano katika kutekeleza majukumu ya kazi katika maeneo yao.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na wajumbe wote wa kamati kwa miongozo yao ambayo kwa aina ya pekee imesaidia sana katika kuboresha utendaji wa Ofisi yetu. Vilevile, nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika na wabunge wote kwa ushirikiano wenu hapa Bungeni kwani ushauri na maelekezo yenu yametusaidia sana katika utekelezaji wa kazi zetu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wote wa jimbo langu la Mtwara Vijijini kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Aidha, kwa namna ya pekee naishikuru familia yangu kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

### **Hitimisho**

91. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/2015 OWM - TAMISEMI imejipanga kusimamia utekelezaji wa dhana ya Utawala bora, Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D) na usimamizi wa rasilimali watu na fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, OWM - TAMISEMI itaendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi zake katika kuleta tija na ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kushirikiana kwa karibu na Halmashauri zao katika kusimamia ukusanyaji wa mapato, matumizi ya rasilimali na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuwawezesha wananchi kupata huduma bora za kiuchumi na kijamii na kuharakisha Maendeleo yao na nchi kwa ujumla.

### **ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, malizia.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2014/2015, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake inaliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Sh.105,527,024,000/=. Kati ya fedha hizo, Sh.80,765,029,000/= ni matumizi ya kawaida na Sh.24,761,995,000/= ni za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Taasisi zake inaombewa jumla ya Sh.479,224,062,000/=. Kati ya fedha hizo Sh.273,065,895,000 ni za matumizi ya kawaida na Sh.206,158,167,000/= ni za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinaombewa jumla ya Sh.267,909,390,000/=. Kati ya fedha hizo Sh.202,310,286,000/= ni za matumizi ya kawaida na Sh.65,509,104,000/= ni za miradi ya maendeleo. Halmashauri zote zinaombewa jumla ya Sh.4,231,442,974,000/=. Kati ya fedha hizo Sh.3,090,370,308,000/= ni matumizi ya kawaida na Sh.682,602,044,000/= ni za miradi ya maendeleo. Aidha, jumla ya Sh.458,470,622,000/= ni mapato ya ndani ya Halmashauri zote.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano inaombewa jumla ya Sh.132,696,894,000/= kwa ajili ya Mfuko wa Bunge ambapo Sh.123,941,455,000/= ni za matumizi ya kawaida na Sh.8,755,439,000 ni za miradi ya maendeleo.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2014/2015 ya jumla ya Sh.5,084,103,450,000/= kwa ajili ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na jumla ya Sh.132,696,894,000/= kwa ajili ya Mfuko wa Bunge ikiwa ni matumizi ya kawaida na fedha za maendeleo za ndani na nje kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii yapo majedwali ambayo yanafanunua kwa kina makadirio ya matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofii)

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**SPIKA:** Ahsante. Hoja hiyo imeungwa mkono. Nimshukuru na kumpongeza Waziri Mkuu pamoja na Waziri wa Nchi kwa hotuba zao zenye urefu na kama mlivyoona ya Waziri wa Nchi, inabidi muisome tena vizuri kwa sababu inahusu Serikali ambazo ninyi ni wahuksika sana katika Majimbo yenu na katika Mikoa yenu.

Sasa naomba nitambulische wageni ambaa Waziri Mkuu alitakiwa awashukuru ni hawa wafuataa:-

Yupo Dkt. Florence Turuka, yeye ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ndugu Jumanne Sagini ni Katibu Mkuu TAMISEMI, Ndugu Regina Kikuli ni Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, yupo huyu? Kwa sababu ni mwanamke ndiyo maana imebidi asimame. (Makofii)

Yuko Ndugu Kagyabukama Kiliba, Naibu Katibu TAMISEMI, Dkt. Deo Mtasiwa, Naibu Katibu Mkuu, TAMISEMI (Afya), Ndugu Zuberi Samataba, Naibu Katibu Mkuu, TAMISEMI (Elimu). (Makofii)

Wako Wakuu Mikoa kutoka Tanzania Bara, ninaomba wasimame wote, ahsanteni sana. Wako Makatibu Tawala kutoka Tanzania Bara, kama wako wasimame, ahsanteni sana. (Makofii)

Yupo Mheshimiwa Jaji Francis Mtungi, Msajili wa Vyama vya Siasa, karibu sana. Huyu anawahusu wote mlioko hapa. (Makofii)

Yuko Dkt. Fatma Mrisho, Mwenyekiti Mtendaji TACAIDS, Ndugu Julius Malaba, Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Ndugu Pascas Muragili, Kaimu Mkurugenzi Mkuu (CDA), ni mwenyeji wetu, Injinia Asteria Mlambo, Mtendaji Mkuu wa DART, Ndugu Anacret Kashuliza, Katibu Mtendaji, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, ahsante yuko upande huu. (Makofii)

Yupo Ndugu Eliud Sanga, Mtendaji Mkuu LAPF, Ndugu Joseph Mriri, Kaimu Mkuu wa Chuo cha Hombolo, Dkt Cyprian Mpemba, Mkurugenzi wa Shirika la Elimu Kibaha, Ndugu Apolonia Chagata, Kaimu Katibu, Bodi ya Serikali za Mitaa. Wapo Wakurugenzi wa Idara mbalimbali Ofisi ya Waziri Mkuu, wengine wamekaa pale na wako Wakurugenzi tisa wa Idara mbalimbali Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninawashukuruni sana kwa kazi mliyofanya. (Makofii)

Mheshimiwa Machali, hili linashughulikiwa kiofisi. Alikuwa anakumbushia kwamba kesho, unajua Ofisi ya Waziri Mkuu tutaingia kwenye makadirio yote, ya kwake na ya Mkoaa, kwa hiyo aliakuwa anauliza vitabu vya makadirio hawajavipata, hilo nadhani litafanyika kiofisi.

## Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Waheshimiwa Wajumbe, najua tuna dakika kama ishirini ili kumaliza lakini ningependa nahirishe shughuli ili muende kusoma. Kesho tutaanza na Kamati zilizohusika na mambo haya na Wasemaji wa Kambi ya Upinzani. Kwa idadi yao ni wengi kwa hiyo muda utatumika, kwa hiyo tuwe wavumilivu kwa sababu watakuwa wanatupa *inside*. Kikubwa kama nilivyosema Bunge letu ni fupi sana, tutumie muda huo kuchambua vitu muhimu kuliko kuleta vichagisho vya maneno visivyokuwa muhimu kwa wananchi. Nadhani tutafanya kazi nzuri zaidi tukifanya hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, napenda kuahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Sasa 1.36 Usiku Bunge *lilahirishwa hadi siku ya Jumatano, Tarehe 7 Mei, 2014, Saa Tatu Asubuhi*)